

**Maswali**  
**Kuhusu**  
**Mafundisho ya**  
**Mormoni**

**(Questions About Mormon Doctrine)**

**Shane Fisher**

**Kimechapishwa na**  
**World Evangelism Publications**  
**Winona, MS**

**Kimechapishwa 2022  
2nd updated edition**

**Ikiwa una swali lolote, maoni, au hoja yoyote  
kuhusu kitabu hiki wasiliana na mwandishi kwa:  
worldevangelism1962@gmail.com**

**kitabu hiki hakiuzwi. Kinatolewa bure na kusamba-  
zwa na kanisa la Kristo.**

**(This book is NOT for sale. It is freely distributed  
and given by the churches of Christ.)**

**Kimechapwa na  
World Evangelism Publications**

**Nakala kwa lugha ya Kiswaili na  
Swahili Gospel Team**

**Mawasiliano:**

**Tanzania, Malawi, Zambia, Rwanda, Burundi & DRC  
Peter Kamatula. +255 (0) 764 792 979  
Shadrack S. Msambaza. +255 (0) 765 098 981**

**Uganda**

**Oyoo Nixson Morris. +256 782 918 861**

**Kenya**

**Mboya F. Awego. +254 (0) 796 963 468 / +255 (0)  
790 408 043**

# Ujumbe wa Mchapishaji

**Betty Burton Choate**

Kwa miongo kadhaa ambayo sisi, timu ya Uinjilisti Ulimwenguni, tumeandika, kuchapisha, na kusambaza vitabu kote ulimwenguni. Kwa kawaida tumeshughulikia vyema uenezaji wa kweli ya Biblia.

Mshiriki mpya wa timu hiyo, Shane Fisher, alionyesha nia yake ya kuandika vitabu dhidi ya dini mbalimbali za uwongo. Somo la kwanza kati ya haya linahusu mafundisho ya “Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho” - Kanisa la Mormoni. Ndugu Fisher amenukuu sana kutoka katika Kitabu cha Mormoni na Maagano na Fundisho, na kulinganisha na Maandiko ya Biblia, na mantiki, kwamba mafundisho haya ni ya uongo.

Tunatoa utangulizi huu kwa maombi kwamba itaongoza kwenye kujifunza zaidi na kusadikishwa ambako kutasababisha kuzaliwa kwa wasomaji waaminifu katika familia ya Mungu, kanisa ambalo Kristo alilifia.

# Utangulizi

Niliandika kitabu hiki kwa moyo wa upendo kwa wale wanaofuata dini hii ya uwongo kwa sababu ninahangaikia sana nafsi yako na mahali utakapokuwa milele. Tafadhali jifunze kifungu kwa kifungu kwa umakini mkubwa, ukisoma Maandiko yanayohusika kutoka katika Biblia. Nimejaribu kuwa wa haki na sahihi kwa kila njia. Sitaki kupotosha msimamo wa mtu yeyote juu ya hoja ya mafundisho. Ikiwa unapenda kujadili mambo zaidi, tafadhali wasiliana nami kwa anwani hii ya barua pepe: **worldangelism1962@gmail.com** [au wasiliana na ndugu hawa; Peter Kamatula +255 764 792 979 au Shadrack S. Msambaza +255 765 098 981].

Kumbuka kwamba Yesu ndiye njia, ukweli na uzima (Yohana 14:6). Alijenga kanisa moja la kweli (Mathayo 16:18) ambalo bado lipo. Kupitia imani yako na utiifu katika Injili, unaweza kuwa mshirika wa kanisa la Kristo leo.

Ninakusihi uwasiliane na mtu aliyekupa kitabu hiki au uwasiliane nami (maelezo kwenye ukurasa wa 2) na tutaanzisha darasa pamoja nawe ili kukuwezesha kujifunza jinsi ya kuwa Mkristo - mtoto wa Mungu!

Shane Fisher  
February 2022

# Yaliyomo

Maswali Kuhusu Kitabu cha Mormoni.....	6
Bibliografia na Kiambatanisho.....	43,44
Mafundisho: Unabii wa Malaki.....	55
Mafundisho: Kifungu kilichopotea.....	56
Mafundisho: Yohana Mtume.....	58
Mafundisho: Ukuhani wa Haruni.....	61
Mafundisho: Ofisi ya Utume.....	67
Mafundisho: Adhabu ya Ufahamu wa Milele.....	71
Mafundisho: “Kijiti cha Efraimu”.....	71
Mafundisho: “Elia” na “Eliya”.....	75
Mafundisho: Zekaria 13:6.....	79
Mafundisho: Karama za Miujiza.....	82
Mafundisho: Lusifa .....	83
Mafundisho: “Esaya” na “Isaya”.....	84
Mafundisho: Mkusanyiko wa Watakatifu.....	84
Mafundisho: Hekalu la Magharibi ya Mbali, MO.....	92
Mafundisho: Unabii wa Vita vya wenyewe kwa wenyewe...	92
Mafundisho: Nyoka na Sumu.....	94
Mafundisho: Neno la Hekima.....	96
Mafundisho: Unabii wa Yoeli.....	99
Mafundisho: Maana ya “Sabaoth”.....	100
Mafundisho: Ukuhani wa Melkizedeki.....	101
Mafundisho: Fundisho la Adamu-Mungu.....	102
Mafundisho: Ufunuo wa siku hizi.....	106
Mafundisho: Nyumba ya Nauvoo.....	107
Mafundisho: Ubatizo wa Wafu.....	107
Mafundisho: Kushikana Mikono na Roho.....	110
Mafundisho: Mitala.....	111
Mafundisho: Tafsiri isiyo sahihi na Unukuzi.....	114
Bibliografia na Kiambatanisho.....	116,120

# Maswali Kuhusu Mafundisho ya Mormoni

**Kitabu cha Mormoni** kinadaiwa kuwa kitabu kingine chenye pumzi ya Mungu pamoja na Biblia. Ikiwa kitabu hicho kimetoka kwa Mungu, basi tunapaswa kukikubali. Walakini, ikiwa hakikutoka kwa Mungu, basi kinapaswa kukataliwa. Tunahitaji kuwa kama Waberoya na kuchunguza kama madai haya ni ya kweli au ya uongo (Matendo 17:10-12). Nimekisoma mara kadhaa na nina maswali mengi kwa Watakatifu wa Siku za Mwisho. Matumaini yangu ni kwamba ndugu (Wakristo) watatumia orodha hii ya maswali kama chombo cha uinjilisti ili kumsaidia Mtakatifu wa Siku za Mwisho kuja kwenye ukweli (Yohana 8:31-32).

**(1) Kwa nini Mungu alichagua kujifunua moja kwa moja kwa Joseph Smith katika Kiingereza cha Elizabeth badala ya Kiingereza cha karne ya kumi na nane (zama alizoishi)?**

Hadithi inaanza na Lehi, Myahudi, aliyeishi Yerusalemu, wakati wa utawala wa Sedekia, mfalme wa Yuda (1 Nefi 1:2–4). Inasemekana ukoo wa familia ya Lehi ulikuwa umejifunza Misri (1 Nefi 3:19).

**(2) Kwa nini walijifunza lugha ya Wamisri?**

**(3) Kwa nini waliandika rekodi hiyo katika lugha ya Kimisri badala ya lugha ya Kiebrania?**

Hapa kuna hoja iliyotolewa katika Mormoni 9:32,33 (401-423 BK): “**Na sasa, tazama, tumeandika haya maandiko kulingana na kujua kwetu, katika herufi ambazo zinaitwa miongoni mwetu Kimisri ‘kilichogeuzwa, ambacho kilitolewa na kugeuzwa nasi, kulingana na njia yetu ya kuongea. Na ikiwa bamba zetu zingekuwa kubwa za kutosha tungeandika katika Kihebrania, lakini Kiebrania**

**kimegeuzwa nasi pia; na ikiwa tungeandika katika Kiebrania; tazama, hamngekuwa na upungufu katika maandishi yetu.)”**

**(4) Je, Mormoni anadai kutokamilika kwa vile haki kuandikwa kwa Kiebrania? Ikiwa ndivyo, hiyo inaendanaje na uvuvio wa kweli unaohitaji kutokuwa na makosa kwani Mungu ndiye mwanzilishi wa ukamilifu (Yohana 10:35; Tito 1:2)?**

Zaidi ya hayo, Wanefi watatu (walioishi katika karne ya kwanza BK) walipaswa kukaa duniani wakitekeleza huduma hadi ujio wa pili wa Yesu Kristo (Ona Mormoni 8:10,11; Etheri 12:17; 3 Nefi 28:4–10).

**(5) Kwa nini hawakujulishwa wapi kumbukumbu zilifichwa na kwa nini Mungu hakuwapa kazi ya kutafsiri rekodi ya Misri iliyofanyiwa marekebisho?**

**(6) Kwa nini kusubiri kwa ujio wa Joseph Smith?**

**(7) Ikiwa Waamerika asili walitoka kwa Walamani, basi kwa nini makabila haya ya Wenyeji wa Amerika hawakuzungumza na/au kuandika katika kwa lugha za Kimitisri au Kiebrania ambazo zingefundishwa kwao?**

Pia tunajifunza Lehi ni nabii ambaye anatabiri kuhusu maangamizi ya Wababeli kwa Yerusalemu (1 Nefi 1:4). Mungu anamwambia Lehi katika ndoto kuitoa familia yake nje ya jiji kwa sababu kuna Wayahudi wanaotafuta kumwua (1 Nefi 2:1) na kwenda nyikani.

1 Nefi 2:4-5 inasema: **“Na ikawa kuwa akatoka na kuelekea nyikani. Na akaacha nyumba yake, na nchi yake ya urithi, na dhahabu yake, na fedha yake, na vitu vyake vya thamani, na hakubeba chochote, isipokuwa jamii yake, na maakuli, pamoja na mahema, na akaelekea nyikani. Na akashuka mipakani karibu na ufuko wa Bahari ya Shamu; na akasafiri nyikani mipakani ambayo imekaribia Bahari ya Shamu; na akasafiri nyikani na**

**jamii yake, ambayo ilikuwa ni mama yangu, Saria, na kaka zangu wakubwa ambao walikuwa ni Lamani, Lemueli, na Samu.”**

Mtafiti mmoja wa Wamormoni alidai kugundua Wadi Tayyib al-Ism kama eneo la mto wa Lamani (1 Nefi 2:8-10) [Potter 1999]. Kutoka Yerusalemu hadi Ghuba ya Akaba, umbali ni kama maili 155. Kutoka hapo hadi Wadi Tayyib al-Ism ni kama maili 74. Hiyo ni maili 229, njia moja!

Simulizi inaendelea kwa Mungu kuja kwa Lehi katika ndoto katika 1 Nefi 3:2-4: **“Na ikawa kuwa akanisemesha, na kuniambia: Tazama nimeota ndoto, ambapo Bwana ameniamrisha kwamba wewe na kaka zako mtarejea Yerusalemu. Kwani tazama, Labani anayo maandishi ya Wayahudi na pia anasaba ya babu zangu, na imechorwa kwenye bamba za shaba nyeupe. Kwa hivyo, Bwana ameniamrisha mimi kwamba wewe na kaka zako mwende nyumbani kwa Labani, mtafute hayo maandishi, na kuyaleta hapa nyikani.”**

**(8) Kwa nini Bwana hakumwamuru Lehi kurudisha bamba za ukoo za shaba huko Yerusalemu kabla hazijajitosa nyikani (1 Nefi 2:1–6; 3:1–10)?**

Katika 2 Wafalme 24:10-18, Biblia inasema: *“Wakati ule watumishi wa Nebukadreza mfalme wa Babeli wakakwea kwenda Yerusalemu, na mji ukahusuriwa. Na Nebukadreza, mfalme wa Babeli, akaufikilia huo mji, hapo watumishi wake walipokuwa wakiuhusuru. Na Yekonia, mfalme wa Yuda, akatoka akamwendea mfalme wa Babeli, yeye na mama yake, na watumishi wake, na wakuu wa watu wake, na maakida wake; mfalme wa Babeli akamchukua mateka katika mwaka wa nane wa kutawala kwake. Akatoa huko hazina zote za nyumba ya Bwana, na hazina za nyumba ya mfalme, akavikata-kata vyombo vyote vya dhahabu ambavyo Sulemani, mfalme wa Israeli, alivifanya katika*



*hekalu la Bwana, kama Bwana alivyosema. Akawachukua mateka watu wa Yerusalemu wote pia, na wakuu wote, na mashujaa wote, watu elfu kumi; na mafundi wote, na wafua chuma wote; hapana mtu aliyebaki, ila waliokuwa wanyonge wa watu wa nchi. Akamchukua Yekonia mpaka Babeli; na mama yake mfalme, na wake zake mfalme, na maakida wake, na wakuu wa nchi, aliwachukua mateka toka Yerusalemu mpaka Babeli. Na mashujaa wote, watu elfu saba, na mafundi na wafua chuma elfu moja, wote pia wenye nguvu, tayari kwa vita, hao wote mfalme wa Babeli aliwachukua mateka mpaka Babeli. Mfalme wa Babeli akamtawaza Matania, ndugu ya baba yake, awe mfalme badala yake, akalibadili jina lake, akamwita Sedekia. Sedekia alikuwa na umri wa miaka ishirini na mmoja ali-poanza kutawala; akatawala miaka kumi na mmoja katika Yerusalemu; na jina la mamaye aliitwa Hamutali, binti Yeremia wa Libna.”*

Matukio ya kitabu cha Mormoni inasemekana yalifanyika katika mwaka wa kwanza wa mfalme Sedekia (1 Nefi 1:4) baada ya 2 Wafalme 24:10-18. Mjomba wa Nefi, Labani, ni tajiri sana kwa sababu alikuwa na hazina.

1 Nefi 4:20 inasema: “**Na baada ya kutenda hivyo, nilielekea kwenye nyumba ya hazina ya Labani. Na nilipoelekea kwenye nyumba ya hazina ya Labani, tazama, nilimwona mtumishi wa Labani ambaye alikuwa na funguo za nyumba ya hazina. Na nikamwamrisha niki-iga sauti ya Labani, kwamba aandamane na mimi hadi nyumba ya hazina.”**

**(9) Kwa nini Labani hakuchukuliwa kwenda uhamishoni?** Biblia inasema kwamba watu maskini zaidi pekee wa nchi ndio waliobaki.

Katika 1 Nefi 2:4, inasema: “**Na ikawa kuwa akatoka na kuelekea nyikani. Na akaacha nyumba yake, na nchi**

**yake ya urithi, na dhahabu yake, na fedha yake, na vitu vyake vya thamani, na hakubeba chochote, isipokuwa jamii yake, na maakuli, pamoja na mahema, na akaelekea nyikani.”**

Wakati Nefi na kaka zake waliporudi kwa Lehi, walimwonesha Lehi mabamba ya ukoo na Lehi aligundua kuwa yeye ni mzao wa Yusufu (haswa Manase - 1 Nefi 5:14; rej. Alma 10:3).

**(10) Kwa nini Lehi - Myahudi ambaye alikuwa ameishi maisha yake yote Yerusalemu (1 Nefi 1:4) hakujua nasaba yake? Alijuaje nchi ya urithi iliyokuwa mali yake kuwa ni ardhi yake ikiwa hajui nasaba yake?**

Ilikuwa muhimu sana kwa Waisraeli kujua habari za ukoo. **Kwanza**, kila kabila lilikuwa limepata urithi wa ardhi (Yoshua 21-22). Kwa Mwisraeli kurithi ardhi katika eneo maalum la kabila ingehitaji ushahidi (wa vinasaba) kwamba alitoka katika kabila hilo. **Pili**, nasaba zilikuwa muhimu kwa sababu zilithibitisha moja ya kigezo cha mwanamume wa Kiyahudi kutumika katika nafasi ya ukuhani (Hesabu 3:8-15). **Tatu**, nasaba ziliwekwa kwa uangalifu ili kufuatilia nasaba ya Masihi ambaye angetoka kwa Daudi (2 Samweli 7:12-14; Mathayo 1; 22:42).\*

1 Nefi 4:38; 5:10b-14a inasema: “**Na ikawa kwamba tukazichukua bamba za shaba na mtumishi wa Labani, na kuelekea nyikani, na kusafiri had kwenye hema la baba yetu... [Nefi, Samu, Lamani, Lemueli-SF] ...baba yangu, Lehi, alichukua yale maandishi ambayo yalikuwa yamechorwa kwenye abamba za shaba, na aliyapekua tangu mwanzo. Na akagundua kwamba yalikuwa na avitabu vitano vya Musa, ambavyo vilieleza historia ya kuumbwa kwa dunia, na pia kwa Adamu na Hawa, ambao ndio wazazi wetu wa kwanza; Na pia amaandishi ya Wayahudi kutoka mwanzo, hadi mwanzo wa utawala wa Zedekia,**

mfalme wa Yuda; Na pia unabii wa manabii watakatifu, tangu mwanzo, hadi mwanzoni mwa utawala wa Zedekia; na pia unabii mwingi ambao ulizungumzwa kutoka kinywa cha Yeremia. Na ikawa kwamba baba yangu, Lehi, pia alipata kwenye bamba za shaba nasaba ya babu zake; kwa hivyo akajua kwamba yeye ni wa kizazi cha Yusu-fu;...”

**(11) Je, hii si idadi kubwa ya fasihi ambayo ingehitaji mabamba mengi ya shaba?**

1 Nefi 4:22-26 inasema: “Na akanizungumzia kuhusu wazee wa Wayahudi, yeye akijua kwamba tajiri yake, Labani, alikuwa nje miongoni mwao usiku ule. Nami nika-zungumza na yeye kama kwamba nilikuwa Labani. Na pia nikamwambia kwamba inanibidi kuchukua michoro, ambayo ilikuwa kwenye bamba za shaba, kwa kaka zangu, waliokuwa nje ya kuta. Na pia nikamwamuru anifuata. Na yeye, akidhania kwamba nilikuwa nikizungumza kuhusu ndugu wa kanisa, na kwamba nilikuwa Labani ambaye nilikuwa nimemwua, kwa hivyo alinifuata.”

**(12) Je, kweli unatarajia mtu mmoja - Nefi - kubeba mabamba haya yote nje ya mji wa Yerusalemu? Nefi ana-manisha nini kwa “ndugu wa kanisa?”**

1 Nefi 5:17-19 inasema: “Na sasa baba yangu alipoona vitu hivi vyote, alijawa na Roho, na akaanza kutoa unabii kuhusu uzao wake—Kwamba hizi bamba za shaba zipelekewe katika mataifa yote, kabila zote, lugha zote, na watu wote wa uzao wake. Kwa hivyo, alisema kwamba hizi bamba za shaba zisiangamie zisiangamie kamwe; wala zisichakazwe na wakati. Na akatoa unabii wa vitu vingi kuhusu uzao wake.”

**(13) Hizi bamba za shaba zisizoharibika ziko wapi leo?** Kulingana na 1 Nefi 7:1–5, Nefi na ndugu zake waliamriwa kwenda Yerusalemu mara ya pili kutafuta wake ili kulea fa-

milia katika nchi ya ahadi.

**(14) Kwa nini Bwana hakumwamuru Nefi na kundi lake kukamilisha kazi hiyo walipokuwa Yerusalemu mape-ma? Kumbuka hii ni safari nyingine ya kwenda na kurudi ya takribani maili 400.**

1 Nefi 7:22–8:2 inasema: **“Na ikawa kwamba tulifika kwenye hema la baba yetu. Na baada ya mimi na kaka zangu pamoja na nyumba yote ya Ishmaeli kufika kwenye hema la baba yangu, walitoa shukrani kwa Bwana Mungu wao; na wakamtolea dhabihu na sadaka za kuteketezwa kwa moto. Na ikawa kwamba tulikuwa tumekusanya jinsi zote za mbegu za kila aina, pamoja na nafaka za kila aina, na pia mbegu za kila aina ya matunda. Na ikawa kuwa wakati baba yangu alipoishi nyikani alituzungumzia..”**

**(15) Ni kwa jinsi gani Nefi na kundi lake wangeweza “kukusanya pamoja kila aina ya mbegu za kila aina,” nafaka na matunda yote nyikani?**

**(16) Kwa nini Lehi anafunua siri ya Kristo kabla ya kujulikana kulingana na mtume Paulo katika karne ya kwanza BK ( Waefeso 3:1-7; Wakolosai 1:24-2:3; 1 Wakorintho 2:7-8; Warumi 16:25-27)?**

Lehi “alitoa unabii” katika 1 Nefi 10:11–14 (inayodhaniwa kuwa iliandikwa kati ya 600-570 KK): **“Na ikawa kwamba baada ya baba yangu kuzungumza maneno haya aliwazungumzia kaka zangu kuhusu injili ambayo itahubiriwa miongoni mwa Wayahudi, na pia kuhusu kufifia kwa Wayahudi katika kutoamini. Na baada ya kumuua Masiya, ajaye, na baada ya kuuwawa atafufuka kutoka kwa wafu, na ajidhihirishe, kupitia nguvu za Roho Mtakatifu, kwa Wayunani. Ndio, baba yangu hata alizungumza mengi kuhusu Wayunani, na pia kuhusu nyumba ya Israeli, kwamba watalinganishwa na mzeituni, ambao matawi yake yatakatwa na kutawanywa kote kote usoni**

**mwa dunia. Kwa hivyo, akasema ni lazima sote tuongozwe pamoja hadi kwa nchi ya ahadi, ili maneno ya Bwana yatimizwe, kuwa tutawanywe kote usoni mwa dunia. Na baada ya nyumba ya Israeli kutawanyika awatakusanyika tena pamoja; au, kwa usemi mwingine, baada ya Wayunani kupokea utimilifu wa Injili, matawi ya asili ya mzeituni, au masazo ya nyumba ya Israeli, yatapandikizwa, au kumfahamu Masiya wa ukweli, Bwana wao na Mkombozi wao.”**

Gary Summers alisema vizuri: “Biblia inatuambia kwamba kuna mambo fulani ambayo hayakujulikana hadi Yesu na mitume walipoyasema. Ni lazima tukumbuke kwamba, ingawa manabii walizungumza juu ya mambo yajayo, hawakuyaelewa. Walichunguza kwa bidii ili kujaribu kujua ni LINI mambo waliyotabiri yangetimizwa, na vile vile maneno yao “yalichomaanisha” (1 Petro 1:10-11). Walishuhudia kabla ya mateso ya Kristo, lakini hawakuelewa ujumbe wao wenyewe (1 Petro 1:12). Kwa hiyo tunawezaje kueleza kwamba Kitabu cha Mormoni kinaweza kufanya muhtasari wa mchakato mzima wa wokovu na hata kuhubiri “ondoleo la dhambi” (maelezo yanayotumiwa tu katika Agano Jipya)?” (Majira ya joto 413). Hoja hii inaweza kutumika katika sura zingine nyingi za kitabu cha Mormoni.

Nefi alipewa maono makuu na Mungu ya siku za mbele. Alimwona Yesu akiwa amezaliwa na bikira (1 Nefi 11:19-21), akibatiwa na Yohana (11:27), miujiza yake (11:31), kusulibiwa (11:33), n.k. Mbali zaidi, Nefi anaona “miungoni mwa Mataifa kuundwa kwa kanisa kuu...kanisa la machukizo” (1 Nefi 13:4,6). Huyu mkuu ni nani na hili kanisa la machukizo? Utambulisho wake unaweza kugundulika katika maelezo ya baadaye katika “unabii” huu.

**Kwanza, Nefi alitabiri “Na nikaangalia na kuona mtu miongoni mwa Wayunani, ambaye alitenganishwa kuto-**

**kana na uzao wa kaka zangu na yale maji mengi; na nika-ona Roho ya Mungu, kwamba ilishuka na kumshawishi mtu huyo; na akasafiri kwa yale maji mengi, hadi akaufikia uzao wa kaka zangu, kwenye nchi ya ahadi.”** (1 Nefi 13:12). Huyu alitambuliwa kama Christopher Columbus.

**Pili**, mistari ya 17-19 ilitabiri vita vya mapinduzi ya kimarekani (1775-1783). “Kanisa kuu la machukizo” lingetakiwa liwe limeshaanzishwa baada ya karne ya kwanza BK. Kwa sababu ya kisa kinachopatikana katika 3 Nefi, kwamba baada ya kupaa kwake Kristo (Mdo. 1:9-11), alishuka kwa watu wa bara la Amerika na kuwatokea Wanefi. Yesu akawaweka wakfu mitume kumi na wawili katika Amerika (1 Nefi 12:6-10; 3 Nefi 19:1-30). Hivyo basi, lile “kanisa kuu la machukizo” lilitakiwa liwe limeanzishwa kati ya karne ya pili na ya kumi na tano. Inawezekana hili likawa linarejelea Ukatoliki wa Kirumi au ukengeufu fulani usiotambulika. Mapema maandiko ya Mormoni yalidai kwamba ni Ukatoliki wa Kirumi huku tafsiri ya Mormoni ya kanisa la sasa ikidai kwamba ni ukengeufu usio na utambulisho maalum. Kwa vyovyote itakavyokuwa, fahamu kuwa “lile kanisa kuu la machukizo”: **“limeondoa kutoka kwa injili ya Mwanakondoo sehemu nyingi ambazo ni wazi na zenye thamani; na pia wamepunguza maagano mengi ya Bwana”** (1 Nefi 13:26).

**(17) Je, Ukatoliki wa Kirumi/Ukengeufu usiotambulika ndio uliharibu Maandiko?**

**(18) Wapi na wakati gani uharibifu huu ulifanyika katika historia ya kuenezwa kwake?**

Tunazo nakala za Agano Jipya kwa maelfu na maelfu na wala hakuna ushahidi wa kupotoshwa kwa fundisho lolote la msingi. Kitabu cha Mormoni kinafanya utetezi wa uongo usioweza kuonesha msingi wa madai yake! Kwa maana hiyo, hakikuvuwiwa na Mungu!

**(19) Ni “Vitu gani” vya thamani katika Biblia vilivyoon-**

## **dolewa na kanisa potofu?**

**(20) Ni ukweli gani mkuu ambao Kitabu cha Mormon kimefunua ambao haukutolewa na Biblia “*unaomkamili-sha mtu kwa kila tendo jema*” (2 Timotheo 3:17)?**

Je, ilikuwa ni: (a) yule mwenye kujitegemea, aliye huru, anayejitegemeza, wa milele na aliye kamili ajulikanaye kama Mungu, (b) Utatu, (c) roho ya mwanadamu na hali yake ya kutokufa, (d) malaika, (e) Uhuru wa kuchagua, (f) sheria za adili zilizotualesha kilicho chema na kibaya, (g) viwango vya kweli vinavyofunua kilicho cha kweli na cha uongo, (h) kujieleza na kuwajibika kwa Mungu, (i) siku ya hukumu na thawabu kwa wenye haki na adhabu kwa waovu, (j) majaliwa ya Mungu, (k) maombi, (l) ufunuo kutoka kwa Mungu, ambao mwanadamu asingeweza kuufikia isipokuwa Mungu mwenyewe atake kumjulisha, (m) kuvuviwa kwa watu waliochaguliwa kwa ajili ya kufunua mapenzi ya Mungu, (n) miujiza kama ushahidi wa uthibitisho wa ufunuo mpya, (o) unabii, (p) dhabihu kwa ajili ya dhambi, (q) kifo cha dhabihu cha Kristo kwa ajili ya wanadamu wote, (r) Kristo kuwa kama Mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu, (s) kiongozi wa mwisho katika ukombozi kutoka katika dhambi, (t) Kristo kutupatia mkusanyiko wa mafundisho sahihi kwa ukujaji wa kiroho, (u) Kristo kama mfano wa mwisho unaotakiwa kufuatwa, (w) Kristo kama sababu ya imani yetu, upendo, na kujitoa kwetu kwake kikamilifu, (x) Kristo kuuva mwili, (y) kufanywa upya na utakaso, (z) masharti na vigezo kwa ajili ya wokovu, imani, kutubu, kukiri, ubatizo katika maji kwa ajili ya ondoleo la dhambi, uaminifu, (aa) maisha ya haki, (bb) maisha ya haki, (cc) maisha ya kila mtu, familia, taifa, na binadamu yafinyangwe na kuchongwa na mapenzi ya Mungu, (dd) urekebishaji wa mawazo yote, matendo, na maisha, katika mahususiano yao yote ya maisha, na duara la utendaji, kama vile ndoa na familia, (ee) kila mtu ainue nafsi yake ka-

tika upendo, haki, na kujitoa dhabihu, (ff) ukuaji usiokoma, (gg)kufufuliwa na kutukuzwa kwa mwili wa mwanadamu, (hh)mfumo wa ukweli thabiti unapaswa kuaminiwa, ibada inayopaswa kufanywa, kanuni zinazopaswa kuongoza njia za kuishi, (hh) na kanisa la Kristo kama taasisi sahihi ambayo Kristo aliijenga katika vizazi vyote hadi kurudi kwake?\*\*\*

Moja kati ya vitu vinavyochanganya katika haya yanayopatikana katika kitabu cha Mormoni ni kwamba yananukuu za Biblia ambazo yumkini zilikuwa bado hazijaandikwa. Inadhaniwa kwamba 1 Nefi iliandikwa kati ya mwaka 600-570 K.K.

**(21) Kwa nini kitabu hiki kina nukuu kutoka katika Biblia (hasa Agano Jipya liloandikwa kati ya mwaka 40-100 B.K) ambazo zilikuwa hazijarekodiwa bado?**

Moja ya mifano hiyo inapatikana katika 1 Nefi 10:7-10: **“Na alizungumza pia kuhusu nabii ambaye angemtangulia Masiya, ili kumtayarishia Bwana njia yake. Ndio, hata ataondoka mbele na kutangaza nyikani: Itayarisheni njia ya Bwana, na yanyosheni mapito yake; kwani miongoni mwenu amesimama yeye msiyemjua; na yeye ni mkuu kunishinda, ambaye mimi sistahili kuilegeza gidamu ya kiatu chake. Na baba yangu alizungumza mengi kuhusu kitu hiki. Na baba yangu akasema atabatiza katika Bethabara, ng’ambo ya Yordani; na pia akasema kuwa atabatiza kwa maji; hata kwamba atambatiza Masiya kwa maji. Na baada ya kumbatiza Masiya kwa maji, itambidi kuona na kushuhudia kwamba alimbatiza Mwanakondoo wa Mungu, ambaye ataondoa dhambi za ulimwengu.”**

Linganisha hili na vifungi kama Mathayo 3:3, na Luka 3:16, na Yohana 1:23, 26-29. **Kwa orodha kamili ya rejea kutoka katika Biblia, tafadhali angalia kiambatanisho katika ukurasa katika ukurasa wa 44.**

**(22) Kwa nini kitabu cha Mormoni kinakubaliana na**



## **mafundisho ya uongo ya Kikalvinisti kuhusu mkengeuko wa urithi?**

2 Nefi 2:21-23 inasema: “...Kwani alitoa amri kwamba lazima wanadamu wote watubu; kwani alionyesha wanadamu wote kwamba walipotea, kwa sababu wazazi wao walivunja sheria. Na sasa, tazama, kama Adamu hangevunja sheria hangeanguka, lakini angeishi katika bustani ya Edeni. Na vitu vyote vilivyoubwa vingebaki katika hali yao ya kwanza baada ya kuumbwa; na vingebaki vivyo hivyo milele, na kuwa bila mwisho. Na hawangezaa watoto; na hivyo wangeishi katika hali ya kitoto, bila shangwe, kwani hawakufahamu dhiki; bila kutenda mema, kwani hawakujua dhambi.”

Biblia inafundisha kwamba dhambi iliingia ulimwenguni kupitia Adamu, lakini watu wote wamepotea kwa sababu wote walimtenda Mungu dhambi.

Warumi 5:12 inasema: “*Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi.*”

**(23) Kwa nini kitabu cha Mormoni kinahimiza kwamba Adamu na Hawa wasingeweza kupata watoto bila kutenda dhambi?** (2 Nefi 2:23). Soma tena 2 Nefi 2:21-23. Hili haliingii akilini kwa sababu moja ya amri za Mungu kwa Adamu na Hawa ilikuwa ni kuzaliana na kuongezeka katika Mwanzo 1:26-27.

**(24) Kwa nini kitabu cha Mormoni kinasema kwamba Adamu na Hawa “walifanya kosa kwa sababu hawakujua dhambi?” Endapo mtu hakutenda dhambi, hili sio jambo jema? Yesu hakutenda dhambi (Ebr. 4:15). Je, hakufanya vizuri?**

**(25) Je, mnenaji anamrejerea Sidney Rigdon (2 Nefi 3:17,18)?** Sehemu inasema: “**Na Bwana aliniambia pia: Ni-**

**tainua uzao wa viuno vyako; na nitampatia mnenaji...**”

**Mafundisho na Maagano 100:9** kinasema: **“Ni muhimu sana kwangu kwamba wewe, mtumishi wangu Sidney, utakuwa msemaji kwa watu hawa; ndiyo, hakika, Nitakuweka katika wito huu, hata kuwa msemaji kwa mtumishi wangu Joseph.”**

Hata maelezo ya chini kuhusu maneno hayo yanarejelea 2 Nefi 3:17,18. Huu ni ushahidi wa ndani unaopendekeza kwa nguvu kubwa kuwa Sidney Rigdon alihusika katika mageuzi ya kubadilisha mswada wa Solomon Spalding kuwa kitabu cha Mormoni.

2 Nefi 5:16,17 inasema: **“Na mimi, Nefi, nilijenga hekalu; na nilijenga kwa umbo la hekalu la Sulemani ila tu halikujengwa na vitu vingi vya thamani; kwani havikupatikana nchini, kwa hivyo, haingejengeka kikamilifu kama hekalu la Sulemani. Lakini umbo la mjengo ulikuwa kama hekalu la Sulemani; na ujenzi wake ulikuwa wa hali ya juu. Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwasababisha watu wangu kuwa na bidii, na kutenda kazi kwa mikono yao.”**

**(26) Ingewezekanaje kwa Nefi na watu wake kujenga jengo kama hekalu la Sulemani?**

Ni miaka 30 imepita tangu familia itoke Yerusalemu (2 Nefi 5:28). Kumbuka kuwa kuna Lehi na mkewe Sariah, wana wa Lehi – Laman, Lemueli, Sam, na Nefi – na hapa tunaambiwa kwamba Lehi alikuwa na mabinti, lakini idadi yao haikutolewa (2 Nefi 5:6). Lehi alikuwa na watoto wawli wa ziada katika nyika - Yakobo na Yusufu (1 Nefi 18:7). Familia ya Ishmaeli iliungana nao, ambayo inahusisha Ishmaeli na mkewe, wawe wawili (ambao tayari walikuwa wameoa na wenye familia) na mabinti watano, waliotarajiwa kuolewa na kizazi cha Lehi (1 Nefi 7:6; 16:7). Mtumwa wa zamani Zoram alikuwa sehemu ya kundi na alimuoa binti wa kwanza wa Ishmaeli (1 Nefi 16:7). Kutokana na kushika kasi kwa kizazi kila familia

ilipata mtoto kila mwaka, na kuwa na idadi ya kutosha ya wafanyakazi waliohitajika kujenga hekalu linalilinganishwa na lile la Sulemani lililochukuwa mika saba na nusu kukamilika.

1 Fa. 5:13-16 inasema: “*Mfalme Sulemani akafanya shokoa ya Israeli wote; nayo shokoa hiyo ilikuwa ya watu thelathini elfu. Akawatuma Lebanoni kwa mwezi, elfu kumi kwa zamu. Mwezi mmoja walikuwako huko Lebanoni, na miezi miwili wakawako kwao. Na Adoramu alikuwa juu ya shokoa. Sulemani alikuwa na wachukua mizigo sabini elfu, na wakatao miti themanini elfu milimani; mbali na maakida yake Sulemani waliokuwa juu ya kazi, elfu tatu na mia tatu, wasimamizi wa watu waliotenda kazi.*”

**(27) Pia, Wayahudi hawa walipataje mamlaka ya kujenga mahali kwa ajili ya jina la Mungu na makao yake ikiwa sehemu sahihi ilikuwa ipo Yerusalemu tayari?**

Kumbukumbu la Torati 12:5-7 inasema: “*Lakini mahali atakapochagua Bwana, Mungu wenu, katika kabila zenu zote, apaweke jina lake, maana, ni makao yake, elekezeni nyuso zenu hapo, nawe wende huko; pelekeni huko sadaka zenu za kuteketezwa, na dhabihu zenu, na zaka zenu, na sadaka ya kuinuliwa ya mikono yenu, na nadhiri zenu, na sadaka zenu za hiari, na wazaliwa wa kwanza wa makundi yenu ya ng’ombe na ya kondoo; na huko mtakula mbele za Bwana, Mungu wenu, nanyi furahini katika yote mtakayotia mikono yenu, ninyi na wa nyumbani mwenu, aliy-okubarikia Bwana, Mungu wako.*” Angalia pia 1 Fa. 8:12-21, 29; 9:3; 11:36; 2 Nya. 6:5-6; 12:13; Yn.4:19-24.

2 Nefi 5:26 inasema: “**Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nili-watenga Yakobo na Yusufu, kwamba wawe makuhani na walimu katika nchi ya watu wangu.**”

**(28) Yakobo na Yusufu (wanatokea katika kabila la Manasse – Alma 10:3) wangewezaje kuwekwa wakfu kuwa makuhani ikiwa hawakutokana na nasaba iliy-**

**oruhusiwa kwa ukuhani katika Israeli – Lawi?** Angalia 2 Nya. 26:16-23 kuona tukio ambalo Uzia alikwenda kinyume na maagizo ya Mungu kwa sababu hakuwa mwana wa Haruni, na hakuruhusiwa kuchoma uvumba.

**(29) Kwa nini 2 Nefi 9:9 (ling. Ether 8:25; Mosia 16:3) inakinzana na 1 Timotheo 2:11-14 katika kuhakikisha kuwa Adamu na Hawa wote walidanganywa wakati Hawa peke yake ndiye aliye danganywa?**

2 Nefi 9:9 inasema: “Na roho zetu lazima zingekuwa kama yeye, na tuwe mashetani, malaika kwa ibilisi, kutengwa na uwepo wa Mungu wetu, na kuishi na baba wa uwongo, katika huzuni, kama yeye mwenyewe; ndio, kwa kile kiumbe kilichodanganya wazazi wetu wa kwanza, ambaye hujigeuza kuwa malaika wa nuru, na huvuruga watotowa watu kuwa na makundi maovu ya siri na ya mauaji na kila aina ya kazi za siri za giza.”

Wazazi wa kwanza wanatambulishwa katika kitabu cha Mormoni kuwa ni Adamu na Hawa (1 Nefi 5:11). Inasema: “Na akagundua kwamba yalikuwa na vitabu vitano vya Musa, ambavyo vilieleza historia ya kuumbwa kwa dunia, na pia kwa Adamu na Hawa, ambao ndio wazazi wetu wa kwanza.”

1 Tim. 2:11-14 inasema: “*Mwanamke na ajifunze katika utulivu, akitii kwa kila namna. Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu. Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye. Wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa.*”

**(30) Kwa nini kitabu cha Mormoni kinasimamia makosa ya watoa nakala wa Biblia toleoo la KJV ikiwa Mungu alivuvia moja kwa moja mchakato ambao kila neno lilisahihishwa kabla Joseph Smith kuanza mchakato wa mwisho wa tafsiri?**

**James Tolle anasema:** “Hakuna ushahidi zaidi ulio dhahiri juu ya asili ya kitabu cha Mormoni zaidi ya matumizi yake makubwa ya nukuu kutoka katika Biblia. Iko wazi kuwa mamia ya vifungu vya kitabu cha Mormoni vimenukuliwa moja kwa moja kutoka katika Biblia; mfano, sehemu kubwa ya Isaya (angalia 2 Nefi 12 hadi 24), hotuba ya mlimani (kama ilivyoandikwa na Mathayo), mistari kadhaa ya maandiko ya Paulo, n.k.

“Jambo la ajabu kuhusu nukuu hizi za Biblia katika kitabu cha Mormoni ni kwamba zimechukuliwa zote kutoka katika Tafsiri ya King James, iliyotafsiriwa na maaskofu wa kanisa la Uingereza karne nyingi baada ya sehemu ya mwisho ya kitabu cha awali cha Mormoni kudhaniwa kuwa kingekuwa kimeandikwa. Fikiria hili! Hapa tuna kitabu ambacho sehemu yake kubwa ilisemekana kwamba iliandikwa kwanza katika lugha safi ya Misri (1 Nefi 1:2) katika mbao zilizoletwa na Nefi kutoka mji wa Yerusalemu miaka mia sita kabla ya Kristo, baadaye kupitia unukuzi wa mara moja, na kwamba kupitia nabii Mormoni katika Kimsri kilichosahihishwa (Mormoni 9:32), na kisha katika karne ya kumi na tisa kwa makusudi kikatafsiriwa kwa kiingereza bila tatizo na Joseph Smith kwa ‘karama na nguvu za Mungu’, ikiwa ni pamoja na nukuu zake zote kutoka katika Biblia zikikubaliana ipasavyo au kwa hakika na tafsiri ya kiingereza ya maandiko matakatifu iliyofanyika katika karne ya kumi na saba kutoka Kiebrania kwenda Kiyunani; ambayo, katika habari ya maandishi ya Kiebrania yamekabidhiwa kutoka kizazi hiki kwenda kizazi kinachofuata, yakiwa yamenakiliwa tena na tena mara mamia. Ikiwa tunakubali madai kwamba nukuu za moja kwa moja za Biblia katika kitabu cha Mormoni zikiwa sahihi au zikiwa zimefanana na zile za tafsiri ya King James zilitafsiriwa bila makosa kwa msaada wa ‘karama na nguvu za Mungu’, basi tunaelekezwa kuhitimisha kwamba

maaskofu wa kanisa la Uingereza walitafsiri nukuu hizi kwa kiingereza kutoka Kiebrania na Kiyunani bila kukosea. Lakini wasomi wa neno wamekubaliana kwamba maaskofu hawa walifanya makosa katika tafsiri yao, ingawa sio makosa makubwa sana ambayo yanabadilisha mafundisho ya msingi. Pia ni ukweli usioweza kukanushwa kwamba baadhi ya makosa hayo yaliletwa katika kitabu cha Mormoni, jambo linalothibitisha bila shaka kuwa lolote mwandishi wa kitabu alilonakili alinakili nukuu moja kwa moja kutoka tafsiri ya King James, na kwamba ‘karama na nguvu za Mungu’ hazikuhusika katika hili” (Tolle 15-17).

**(31) Kwa nini kitabu cha Mormoni kinaonekana kuathiriwa kimazingira na utata wa Freemasoni unaoendana na muktadhaa wa historia ya Marekani ya karne ya kumi na tisa?** 2 Nefi 10:11-15; 26:14-22; Helaiman 6:22,23; 3 Nefi 3:9; 6:28-30; 7:6-10; Esta 8:15-25; 10:33.

2 Nefi 10:3 inasema: **“Kwa hivyo, kama vile nilivyowaambia, lazima inahitajika kwamba Kristo kwani usiku uliopita malaika aliniambia kwamba hili litakuwa jina lake atakuja miongoni mwa Wayahudi, miongoni mwa wale ambao ni waovu zaidi ulimwenguni; na watamsulubu hivyo ndivyo ilimpasa Munguwetu, na hakuna taifa lingine duniani ambalo lingemsulubu Mungu wao.”**

**(32) Kwa nini Nefi anasema kwamba jina la Mwokozi lingekuwa Kristo wakati hili ni neno la Kiyunani lenye maana sawa na lile la Kiebrania - Masihi?**

Moja kati ya alama za uvuvio wa Biblia ni ufupisho wa maneno yake.

**Dave Miller anafafanua:** “Kuna ushahidi wa kutosha unaothibitisha kuwa Biblia imevuviwa na Mungu. Lakini ufupisho wa maneno wenye uangalifu wa Kitabu ni moja kati ya ushahidi wa dhahiri ya kuwa kilitoka kwa Mungu. Katika historia yote, wanadamu wamekuwa wenye maneno

mengi katika kufikisha mawazo na mitazamo yao; kutoka katika matoleo mengi ya ensiklopedia [kitabu chenye taarifa mbalimbali], vitabu vya historia, na vinavyozungumzia maisha ya watu, katika matamko ya viongozi wa dini kupitia mabaraza yao, nidhamu, na theolojia kadha wa kadha. Katika alama za ulinganifu wa mwelekeo huu wa kibinadamu, vitabu vya Biblia ni vifupi sana kiasi cha kushangaza. Fikiria kwa mfano, kwamba Mathayo, Marko, Luka, na Yohana walipewa jukumu zito la kuufahamisha ulimwengu wa nyakati zote juu ya matukio yasio kifani yanayozunguka maisha ya Kristo alipokuwa hapa duniani. Yohana yeye anakubali kwamba kulikuwa na mambo mengi yaliyotokea katika maisha ya Yesuambayo yakilandikwa moja moja, nadhani hata ulimwengu usingetosha kwa vile vitabu vitakavyoandikwa” (Yohana 21:25). Kwa hiyo, ni kitu gani kilitakiwa kuingizwa humo, na kipi kilitakiwa kuachwa katika mazingira ya uandishi yaliyohitaji jitihada kubwa?

“Katika kuripoti matukio katika maisha ya mtu mashuhuri sana katika historia ya ulimwengu, ni mwandishi gani mwanadamu angeweza kuweka pembeni kuzaliwa kwake, kama Marko na Yohana walivyofanya? Ni mwandishi gani angeweza kuiacha pembeni ile miaka thelathini ya kwanza ya maisha ya mtu kama huyu, kama waandishi wanne wa injili walivyofanya (Luka akiwa na tukio moja tu katika maisha ya Yesu akiwa na miaka kumi na miwili)? Ubatizo wa Yesu unaelezwa katika nistari kumi na mwili tu katika Mathayo, na mistari sita tu katika Marko na Luka. Katika matukio kumi na mbili ya kuonekana kwake Yesu baada ya kufufuka, mawili yametajwa na Mathayo, matatu na Marko na Luka, na manne na Yohana. Katika Matendo ya mitume, Luka anatoa ripoti ya pekee iliyovuviwa ya ile miaka thelathini ya kwanza ya historia ya kanisa na kuenea kwa ukristo; na hili analifanya katika sura ishini na nane tu! Kifo cha

mapema cha mtume wa kwanza, Yakobo, ambacho kilisababisha mlipuko mkubwa katika kanisa la awali (kikilinganishwa, tuseme na, kuuwawa kwa raisi John F. Kennedy kwa wamarekani), kimeripotiwa kwa kifupi sana kwa maneno kumi na moja. Kwa maafa ya aina hii, habari zenye kutikisa nchi, iliwezekanaje kwa waandishi hawa kutoa kurasa hizo zenye maneno machache, yaliyoshiba, yenye usahihi wa historia? Majibu? Waliandika chini ya uongozi wa ushawishi (na katika kesi hii, kujizuia) wa Roho Mtakatifu (2 Petro 1:21)” (Miller 1).

### **(33) Je, 2 Nefi 31:1, 2 haikiuki kanuni ya ufupisho wa maneno?**

“Na sasa mimi, Nefi, namaliza kuwatolea unabii, ndugu zangu wapendwa. Na siwezi kuandika isipokuwa tu vitu vichache, ambavyo najua kwa hakika lazima vitatimia; wala siwezi kuandika isipokuwa tu maneno machache ya kaka yangu Yakobo. Kwa hivyo, vitu ambavyo nimeandika vimenitosha, ila tu maneno machache ambayo lazima niyazungumze kuhusu mafundisho ya Kristo; kwa hivyo, nitawazungumzia kwa uwazi, kulingana na unyofu wangu ninapotoa unabii.” Na mifano mingine mingi inaweza kutolewa.

2 Nefi 25:10 inasema: “**Kwa hivyo, walikuwa wameeleze-wa kuhusu maangamizo yatakayowajia, mara tu baada ya baba yangu alipotoka Yerusalemu; walakini, walishupaza mioyo yao; na kulingana na unabii wangu wameangamizwa, ijapokuwa wale waliopelekwa utumwani huko Babilonia.**” Ukizingatia kwamba inasemekana kuwa 1 Nefi ilitukia mnamo mwaka wa kwanza wa utawala wa Sedekia (1 Nefi 1:2) na kuharibiwa kwa Yerusalemu hakukutokea mpaka ile miaka kumi na moja ya utawala wa Sedekia (angalia Yermia 39:2; 52:5).

2 Fal. 25:1-2 inasema: “***Ikawa katika mwaka wa kenda wa***



*kutawala kwake, katika mwezi wa kumi, na siku ya kumi ya mwezi huo, Nebukadreza, mfalme wa Babeli, akaja, yeye na jeshi lake lote, kupigana na Yerusalemu, akapanga hema zake kuukabili; nao wakajenga ngome juu yake pande zote. Basi mji huo ulihusuriwa hata mwaka wa kumi na moja wa mfalme Sedekia.”*

**(34) Je, miaka kenda hadi kumi na moja sio umbali mkubwa kwa neno “mara tu...”?**

2 Nefi 25:19 inasema: “**Kwani kulingana na maneno ya manabii, Masiya atakuja baada ya miaka miasita tangu baba yangu atoke Yerusalemu; na kulingana na maneno ya manabii, na pia neno la malaika wa Mungu, jina lake litakuwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.”**

**(35) Je, hakuna mkanganyiko baina ya 2 Nefi 25:19 na Mathayo 1:22, 25 kwa sababu jina halikutolewa hadi pale malaika Gabriel alipomwambia Mariamu?**

2 Nefi 25:24, 25 inasema: “**Na, ingawa tunamwamini Kristo, tunatii sheria ya Musa, na kutazama mbele kwa uthabiti kwa Kristo, hadi sheria itakapotimizwa. Kwani, ni kwa kusudi hili sheria ilitolewa; kwa hivyo sheria imekufa kwetu, na tumefanywa hai katika Kristo kwa sababu ya imani yetu; lakini bado tunatii sheria kwa sababu ya amri.”**

Moja kati ya malengo ya msingi ya Yesu ilikuwa kutimiza sheria ya Musa na kwa njia hiyo kuiondoa (Mathayo 5:17-18; Waefeso 2:14-16; Wakolosai 2:14-16; Waebrania 10:9-10).

Paulo aliandika katika Warumi 7:1-4: “***Ndugu zangu, ham-jui (maana nasema na hao wajuu sheria) ya kuwa torati humtawala mtu wakati anapokuwa yu hai? Kwa maana mwanamke aliye na mume amefungwa na sheria kwa yule mume wakati anapokuwa yu hai; bali akifa yule mume, amefunguliwa ile sheria ya mume. Basi wakati awapo hai mumewe, kama akiwa na mume mwingine huitwa mzinzi.***

***Ila mumewe akifa, amekuwa huru, hafungwi na sheria hiyo, hata yeye si mzinzi, ajapoolewa na mume mwingine. Kadhalika, ndugu zangu, ninyi pia mmeifia torati, kwa njia ya mwili wa Kristo, mpate kuwa mali ya mwingine, yeye aliyefufuka katika wafu, kusudi tumzalie Mungu matunda.***”

Ni muhimu sana kutambua kwamba hadi Yesu anakufa pale msalabani, sheria ya Musa ilikuwa hai bado. Yesu alipoitimiliza kwa kifo chake, ndipo Wayahudi walipofunguliwa kutoka katika sheria hiyo. Wakafungwa sasa na Agano Jipya, sheria ya Kristo (Gal. 6:2; Waebrania 8:8-10; 10:1-9). Paulo alizungumzia ukweli wa kitheolojia kwamba maagano mawili hayawezi kufanya kazi kwa wakati mmoja au vinginevyo Wayahudi wangukuwa katika hali ya kutenda uzinzi wa kiroho.

**Bales anaandika:** “Kama [Wayahudi] wangukuwa chini ya Agano lake kabla ya sheria [Torati] kuondoka, na kabla hawajaifia Torati, basi wangukuwa wamezini kiroho. Kwa sababu wakiwa bado wamefungamana na ile sheria, wasingeweza kufungamana na Kristo. Baada ya kufafanua hoja yake kwa kutumia kielelezo cha mahusiano ya ndoa, anahitimisha kwa kusema ‘kadhalika’ uhusiano na Agano la Kale ulivunjwa ili kwamba wapate kuungana na Kristo. Ndiyo, ***waliifia torati, kwa njia ya mwili wa Kristo***, (ili kwamba) ***wapate*** kuunganishwa au kuoreshwa kwa Kristo (Warumi 7:4). Kwa hiyo ni dhahiri kwamba kadiri sheria ilipokuwa hai, wao pia walikuwa hai kwa sheria hiyo, wakiishi chini yake; lakini wasingeweza kukombolewa kutoka katika sheria hiyo (Warumi 7:4, 6). Na maadamu wasingeweza kukombolewa kutoka katika sheria, wasingeweza kuungana na Kristo” (Bales 150).

**(36) Ni kwa jinsi gani basi Nefi alisema kwamba sheria ya Musa ilikufa kwao wakati Yesu alikuwa bado hajafa?**

**(37) Pia, ni kwa jinsi gani wangeweza kuifuata sheria ya Musa na Injili kwa wakati mmoja bila kufanya uzinzi**

## **wa kiroho?**

Yakobo 2:27,28; 3:5 (Mormoni) anasema: “**Kwa hivyo, ndugu zangu, nisikilizeni, na mtii neno la Bwana: Kwani hakuna mtu yeyote miongoni mwenu ambaye atakuwa na mke zaidi ya mmoja; wala hatakuwa na masuria; Kwani mimi, Bwana Mungu, nafurahia usafi wa kimwili wa wanawake. Na ukahaba ni chukizo mbele yangu; ndivyo hivi Bwana wa Majeshi anavyosema...Tazameni, Walamani ndugu zenu, ambao mnawachukia kwa sababu ya uchafu wao na laana ambayo imeshika ngozi zao, ni watakatifu zaidi yenu; kwani hawajasahau amri ya Bwana, ambayo ilipewa kwa baba yetu—kwamba waoe mke mmoja pekee, na wasiwe na makahaba, na wasitende usherati miongoni mwao.”**

**(38) Kwanini ufunuo alioutoa Yakobo kuhusu kuwa na mke mmoja bila ya kuwa na Masuria uliondolewa na [kitabu cha ] Fundisho na Maagano 132 (imeripotiwa katika 1843) ambapo mitala ilihalalishwa? Kwa nini sheria ya mitala ilitenguliwa katika [mwaka wa] 1890?**

**(39) Je, hii istiyari ndefu ya Yakobo 5 inanakili mchanganyiko wa mithali ya Luka 13:5-9, kuhusu Mtini (na Mtini mwitu), na kutoka katika Warumi 11:11-36, na Yesu kama mzabibu wa kweli kutoka katika Yohana 15:1-8?**

Katika Yakobo 3:12-13 (inakadiriwa kati ya mwaka 544 na 421 B.K), anasema: “**Na sasa mimi, Yakobo, niliwazungumzia watu wa Nefi vitu vingi zaidi nikiwaonya wasitende uasherati na tamaa,na kila aina ya dhambi, na kuwaelezea matokeo yao. Na haiwezakani kuandika hata asilimia moja ya yale yaliotendwa na watu hawa, ambao waliongezeka kuwa wengi, katika bamba hizi; lakini matendo yao mengi yameandikwa katika zile bamba kubwa, na vita vyao, na mabishano yao, na utawala wa wafalme wao.”**

Yakobo alikuwa mmoja kati ya wana wa Lehi aliyezaliwa nyikani. Katika 2 Nefi 5:34, tunajifunza kuwa miaka 30-70 ilikuwa imepita.

**(40) Ukichukulia idadi ya watu walioorodheshwa walio-kuja katika ulimwengu mpya, kweli tunaweza kuhitimi-sha kuwa hii ni idadi kubwa ya watu? Sehemu moja ya mia ya mambo yao isingeweza kurekodiwa kwa sababu kulikuwa na historia ya kutosha ndani ya miaka sabaini na zaidi ambayo Yakobo aliishi.**

Yakobo 7:27 inasema: “Na mimi, Yakobo, nikafahamu kwamba lazima hivi karibu niende kaburini; kwa hivyo, nikamwambia mwana wangu Enoshi: Chukua hizi bamba. Na nilimwambia vile vitu ambavyo kaka yangu Nefi aliniamuru, na akaahidi kutii zile amri. Na ninamaliza kuandika katika bamba hizi, uandishi ambao umekuwa mfupi; na kwa msomaji nakuaga kwa heri, nikitumaini kwamba ndugu zangu wengi watasoma maneno haya. Ndugu, Mungu awe nanyi [imehitimishwa kwa neno ‘adieu’ katika nakala ya kiingereza].”

**(41) Neno la kifaransa “adieu” lilingiaje katika maandishi haya ya kimisri kilichofanyiwa mabadiliko?**

Mosia 2:3 inasema: “Na pia walichukua malimbuko ya mifugo yao, ili watoe dhabihu na sadaka za kuteketezwa kwa moto kulingana na sheria ya Musa.”

**Tolle anasema maneno haya:** “Katika sheria ya Musa, mzaliwa wa kwanza wa wanyama asingeweza kutolewa kama sadaka ya kuteketezwa na dhabihu. Wazaliwa wa kwanza walikuwa mali ya Bwana moja kwa moja na hawakupaswa kuhesabiwa kama mali ya mtu. Lakini sadaka zote za kuteketezwa zilichaguliwa kutoka katika mali binafsi ya mhusika, au kununuliwa kwa pesa zake mwenyewe kwa kusudi hili, huku wazaliwa wote wa kwanza wa mifugo, ambao tayari ni mali ya Bwana, waliletwa kwa kuhani mkuu,

sio kwa ajili ya kutumika kama sadaka ya kuteketzwa bali ili nyama yake iliwe na kuhani mkuu na familia yake. Soma Kutoka 13: 2,12 ; 22: 29,30 ; Hes. 3: 13; 2 Sam. 24:24; Hesabu 18:15-18” (Tolle 18).

**(42) Kwa nini inasema kwamba walitoa dhabihu sawasawa na sheria ya Musa wakati, kusema ukweli, hawakushika sheria ya Musa katika hili?**

Mosia 20:1-5 inasema: “Sasa palikuwa na pahali katika Shemloni ambapo mabinti za Walamani walikusanyika pamoja kuimba, na kucheza, na kujifurahisha. Na ikawa kwamba siku moja kikundi chao kidogo kilikusanyika pamoja ili waimbe na wacheze. Na sasa makuhani wa mfalme Nuhu, wakiona aibu yakurejea katika mji wa Nefi, ndio, na pia wakiogopa kwamba watu watawaua, kwa hivyo hawakuwarudia wake zao na watoto wao. Na baada ya kungoja nyikani, na baada ya kugundua mabinti za Walamani, walijificha na kuwatazama; Na wakati walikuwa ni wachache tu waliokusanyika pamoja kucheza, waliondoka pahali pao pa siri na kuwashika na kuwapeleka nyikani; ndio, mabinti ishirini na nne wa Walamani waliwapeleka nyikani.”

**(43) Je, Mosia 20:1-5 imetoholewa kutoka Waamuzi 21:16-24?**

Mosia 18:16,17 (147-145 K.K.) inaeleza: “Na hivi ndivyo alivyobatiza kila mmoja aliyeenda mahali pa Mormoni; na walikuwa watu mia mbili na nne; ndio, na walibatizwa katika maji ya Mormoni, na wakajazwa na neema ya Mungu. Na waliitwa kanisa la Mungu, au kanisa la Kristo, kutoka siku ile na kuendelea mbele. Na ikawa kwamba yeyote aliyebatizwa kwa uwezo na mamlaka ya Mungu aliongezwa katika kanisa lake.”

**(44) Ilikuwa je kanisa likawa tayari limeanza katika Mosia 18:16, 17 (147-145 B.K.) ikiwa Yesu alikuwa bado**

**hajalijenga kwa mujibu wa Mathayo 16:18?**

**(45) Je, Mosia 27 (100-92 K.K) ni wizi wa taarifa ya kuongolewa kwa Paulo katika Matendo 9?**

Alma 5:3 inasema: “Mimi, Alma, baada ya kuwekwa wakfu na baba yangu, Alma, kuwa kuhani mkuu wa kanisa la Mungu, yeye akiwa na uwezo na cmamlaka kutoka kwa Mungu ya kutenda vitu hivi, tazama, ninawaambia kwamba alianza kuimarisha kanisa katika nchi ambayo ilikuwa mipakani mwa Nefi; ndio, nchi ambayo iliitwa nchi ya Mormoni; ndio, na alibatiza ndugu zake katika maji ya Mormoni.”

**(46) Kwa nini kuna kuhani mkuu katika kanisa (ambalo halijakuwepo – Mathayo 16:18) wakati Yesu ndiye anayetumika kama Kuhani Mkuu (Waebrania 7)?**

Alma 7:10 inasema: “Na tazama, atazaliwa na Mariamu, huko Yerusalemu ambayo ni nchi ya babu zetu, yeye akiwa bikira, chombo cha thamani na kilichochaguliwa, ambaye atawezeshwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu kupata mimba, na kumzaa mwana, ndio, hata Mwana wa Mungu.”

**(47) Kwa nini Alma 7:10 inasema kwamba Yesu angezaliwa Yerusalemu na si Bethlehemu (Mika 5:2; Mathayo 2:1-6)?**

Alma 5:28 (83 K.K) inasema: “Tazama, mmevuliwa kiburi? Ninawaambia, kama bado, hamko tayari kukutana na Mungu. Tazama lazima mjitayarishe haraka; kwani ufalme wa mbinguni u karibu, na kama huyu hana uzima wa milele.”

Alma 5:50 inasema: “Ndio, hivi anasema Roho: Tubuni, nyinyi kote ulimwenguni, kwani ufalme wa mbinguni umo mkononi; ndio, Mwana wa Mungu anakuja katika utukufu wake mkuu, kwa nguvu zake, fahari, uwezo, na utawala. Ndio, ndugu zangu wapendwa, ninawaambia, kwamba Roho anasema: Tazama utukufu wa Mfalme wa

**ulimwengu wote; na pia Mfalme wa mbinguni hivi kari-buni utametameta miongoni mwa wanadamu.”**

Helaman 5:32 (30 K.K.) inasema: **“Na tazama sauti ilikuja tena, ikisema: Tubuni nyinyi, tubuni nyinyi, kwani ufalme wa mbinguni uko karibu; na msijaribu tena kuwaangamiza watumishi wangu. Na ikawa kwamba nchi ilitetemeka tena, na kuta zikatingisika.”**

Yohana mbatizaji (Mathayo 3:1) na Yesu (Mathayo 4:17) walisema kwamba Ufalme wa mbinguni ulikaribia kwa sababu ulitarajiwa kuja katika kipindi cha miaka mitatu na nusu kutokea muda huo. Hili linaleta maana.

**(48) Hata hivyo, je, inaleta maana kwamba waandishi wa kitabu cha Mormoni walitangaza kuwa ufalme wa mbinguni ulikuwa karibu kwa umbali wa miaka 113 (Alma) na umbali wa miaka 60 (Helaman)?**

Alma 46:14,15 (73-72 K.K.) inasema: **“Kwani ndivyo waumini wa Kweli wa Kristo, waliokuwa ndani ya kanisa la Mungu, walivyoitwa na wale ambao hawakuwa wafuasi wa kanisa. Na wale ambao walikuwa wa kanisa walikuwa waaminifu; ndio, wale wote ambao waliokuwa waumini wa kweli katika Kristo walijichukulia, kwa furaha, jina la Kristo, au Wakristo vile waliitwa, kwa sababu ya imani yao katika Kristo ambaye angekuja.”**

**(49) Je, huku sio kupingana na Matendo 11:26?** Inayo-sema: **“Hata alipokwisha kumwona akamleta Antiokia. Ika-wa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliit-wa Wakristo kwanza hapo Antiokia.”**

**(50) Kwa nini Helaman 12:26 (inadhaniwa kuandikwa katika mwaka wa 6 K.K.) inanukuu Yohana 5:28-29 ambayo ilikuwa haijaandikwa bado?** Inasema: **“Ndio, ambao watawekwa kwa hali yenye taabu isiyo na mwisho, kwa kutimiza maneno ambayo yanasema: Wale ambao wam-**

**etenda mema watakuwa na maisha yasiyo na mwisho; na wale ambao wametenda maovu watapata laana isiyo na mwisho. Na hivyo ndivyo ilivyo. Amina.”**

Cha kufarahisha zaidi, maneno ya chini katika mstari huo yanajaribu kutatua kosa hili kwa kusema kwamba yanatoka katika Danieli 12:2-3. Wewe utakuwa shahidi kwa kuamua ni mstari gani ulinukuliwa; (a) Danieli 12:2: “**Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele**”; (b) Yohana 5:28-29: “**Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu.**”

Helaman 14:20 inasema kuhusu kusulibiwa kwa Yesu: “**Lakini tazama, vile niliwaambia kuhusu ishara nyingine, ishara ya kifo chake, tazama, katika siku hiyo ambayo atapatwa na kifo jua litawekwa giza na kukataa kutoa mwangaza wake kwenu; na pia mwezi na nyota; na haku-takuwa na mwangaza juu ya hii nchi, hata kutokea wakati atakapokufa, kwa muda wa siku tatu, hadi kwenye siku atakayofufuka tena kutoka kwa wafu.**”

**(51) Unawezaje kuunganisha Helaman 14:20 – inayosema giza lilitokea kwa siku tatu, na vitabu vya Injili vina-yosema kuwa giza lilitokea kwa masaa matatu?** Angalia pia 3 Nefi 8:3.

Katika 3 Nefi 9:18, Yesu anawaambia Wanefi (kumbuka: kwa mujibu wa kitabu cha Mormoni watu hawa wanasemekana kuwa watu wa kwanza nchini Marekani waliozungumza Kiyahudi na Kimisri): “**Mimi ndimi nuru na uzima wa ulimwengu. Mimi ndimi Alfa na Omega, mwanzo na mwisho.**”

**(52) Lengo la Yesu lilikuwa nini hasa kuwapa watu**



## **hawa herufi ya kwanza na ya mwisho katika alfabeti za Kiyunani?**

Katika 3 Nefi 11:13-17, inaelezwa: “**Na ikawa kwamba Bwana aliwazungumzia akisema: Inukeni na mje kwangu, ili msukume mikono yenu na muitie kwenye ubavu wangu, na pia kwamba mguse alama za misumari katika mikono yangu na katika miguu yangu, ili mjue mimi ni Mungu wa Israeli,na Mungu wa ulimwengu wote, na nimeuawa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Na ikawa kwamba umati ulienda mbele, na kusukuma mikono yao ubavuni mwake, na wakaona alama za misumari katika mikono yake na katika miguu yake; na hivi walifanya wakienda mbele mmoja mmoja, mpaka walipoenda wote, na waliona na macho yao na kupapasa kwa mikono yao, na walijua ukweli na walishuhudia wenyewe kwamba ni yeye, ambaye manabii waliandika kwamba atakuja. Na wakati walipokuwa wameenda wote na kujishuhudiawenyewe, walipaza sauti kwa toleo moja wakisema: Hosana! Heri liwe jina la Mungu Aliye Juu Sana! Nawaliinama chini miguuni mwa Yesu na kumwabudu.”**

Baadaye tunajifunza idadi ya makadirio ya yale makutano katika 3 Nefi 17:25: “**wanashuhudia; na wanajua kwamba maandishi yao ni ya kweli kwani wote waliona na kusikia, kila mtu binafsi; na idadi yao ilikuwa karibu watu elfu mbili na mia tano; na walikuwa wanaume, wanawake, na watoto.”**

**(53) Kweli tunaweza kukubali kwa dhati kwamba takribani watu 2,500 waliweka mikono yao katika vidonda vya Yesu?** Hata kama mtu alichukua sekunde 30 kumchunguza Yesu, basi ingechukua takribana masaa 21 jumla kwa idadi hiyo! Pia, inatakiwa kuweka wazi kwamba hili linadhaniwa kutukumbusha kuhusu Tomaso (Yohana 20:24-29). Tatizo lingine linalojitokeza katika habari hii katika 3 Nefi ni

kwamba makutano hawakuwahi hata kumwona Yesu au hata kumjua binafsi kabla ya tukio hili. Hata hivyo, Tomaso alitaka kuona vidonda vya Yesu kwa sababu alinfahamu vizuri kwa miaka mitatu na alihitaji ushahidi unaoweza kumshawishi kwamba kuwa huu ulikuwa mwili halisi wa Bwana wake na sio mzimu.

3 Nefi 18:8-13 inasema: **“Na ikawa kwamba baada ya kusema haya maneno, aliwaamuru wanafunzi wake kwamba wachukue divai ndani ya kikombe na wainywe, na kwamba wawapatie umati ili wanywe. Na ikawa kwamba walifanya hivyo, na wakainywa na kushiba; na kuupatia umati, na wakanywa, na wakashiba. Na baada ya wanafunzi kufanya hivyo, Yesu aliwaambia: Mna heri kwa hiki kitu ambacho mmefanya, kwani hii ni kutimiza amri zangu, na hii inashuhudia kwa Baba kwamba mko tayari kufanya yale ambayo nimewaamuru. Na daima mtafanya hivi kwa wale wanaotubu na kubatizwa katika jina langu; na mtafanya hivi kwa ukumbusho wa damu yangu, ambayo nilimwaga kwa ajili yenu, ili mshuhudie kwa Baba kwamba daima mnanikumbuka. Na ikiwa yangu itukuwa na nyinyi. Na ninawapatia amri kwamba mtafanya hivi vitu. Na ikiwa mtafanya hivi vitu daima mna baraka, kwani mmejengwa juu ya mwamba wangu. Lakini yeyote miongoni mwenu ambaye atafanya zaidi au ndogo kuliko haya hajajengwa juu ya mwamba wangu, lakini wamejengwa kwenye msingi wa mchanga; na wakati mvua inateremka, na mafuriko kuja, na pepo kuvuma, na kujipigisha juu yao, wataanguka, na milango ya jahanamu iko tayari kuwapokea.”**

**(54) Kwa kuwa madhehebu ya Wamormoni yalibadilisha kipengele cha meza ya Bwana kwa kutumia maji badala ya divai; je, huoni kuwa hawamtii Mungu sawa sawa na 3 Nefi 18:13?**

3 Nefi 20:23-26 insema: “Tazama, ni mimi ambaye Musa alimzungumzia akisema: Bwana Mungu wenu atainua nabii huyo kutoka miongoni mwa ndugu zenu kama mimi; yeye ndiye mtamsikiliza kwa vitu vyote atakavyowaambia. Na itakuwa kwamba kila nafsi ambayo haitamsikiliza nabii itakatiwa mbali kutoka miongoni mwa watu. Kweli, nawaambia, ndio, na manabii wote kutokea Samweli na wale ambao wanafuata baadaye, kadiri vile wengi wamezungumza, wamenishuhudia. Na tazama, nyinyi ni watoto wa manabii; na nyinyi ni wa nyumba ya Israeli; na ni wa agano ambalo Baba alifanya na babu zenu akisema kwa Ibrahimu: Na kupitia uzao wako, makabila yote ya dunia yatabarikiwa. Baba alinitayarisha mimi kwanza, na kunituma niwabariki nyinyi kwa kugeuza kila mmoja wenu kutoka kwa uovu wake; na hivyo ni kwa sababu nyinyi ni watoto wa agano.”

**(55) Je, Yesu alinukuu kutoka katika hotuba ya Petro katika Matendo 3 (Mdo. 3:23-25)?** 3 Nefi 28:4-12 inaeleza: “Na baada ya kuwazungumzia, alijigeuza kuelekea wale watatu, na kuwaambia: Ni kitu gani ambacho mnataka niwafanyie, wakati nitakapokwenda kwa Baba? Na walihuzunika mioyoni mwao, kwani hawakuthubutu kuzungumza na yeye kitu ambacho walitaka. Na akawaambia: Tazama, najua mawazo yenu, na mmetaka kitu ambacho Yohana, mpendwa wangu, ambaye alikuwa na mimi katika huduma yangu kabla ya mimi kuinuliwa juu na Wayahudi, alichotaka kwangu. Kwa hivyo heri zaidi kwenu kwani kamwe hamtaonja kifo; lakini mtaishi kuona vitendo vyote vya Baba kwa watoto wa watu, hata mpaka vitu vyote vitatimizwa kulingana na mapenzi ya Baba, wakati nitakapokuja kwa utukufu wangu na uwezo wa mbinguni. Na hamtaumia uchungu wa kifo; lakini nitakapokuja katika utukufu wangu mtabadilishwa kwa nuk-

ta moja kutoka hali ya kufa hadi kwa hali ya kutokufa; na ndipo mtabarikiwa katika ufalme wa Baba yangu. Na tena, hamtapata maumivu wakati mtakapoishi kimwili; wala huzuni isipokuwa kwa dhambi za ulimwengu; na haya yote nitafanya kwa sababu ya kitu ambacho mmetaka kutoka kwangu, kwani mmetaka kwamba mlete roho za watu kwangu, wakati dunia itakaposimama. Na kwa sababu hii mtapata utimilifu wa shangwe; na mtaketi chini katika ufalme wa Baba yangu; ndio, shangwe yenu itajaa, hata vile Baba amenipatia utimilifu wa shangwe; na mtakuwa hata kama nilivyo, nami niko hata vile Baba alivyo, na Baba nami tuko mmoja. Na Roho Mtakatifu hushuhudia mambo ya Baba na Mimi; na Baba huwapa watoto wa watu Roho Mtakatifu kwa sababu yangu. Na ikawa kwamba baada ya Yesu kuzungumza haya maneno, alimgusa kila mmoja wao kwa kidole chake isipokuwa wale watatu ambao walikuwa wa kukawia, na hapo akaondoka.”

**(56) Wako wapi hawa Wanefi watatu wanaotakiwa kuwa wakingojea hadi kuja kwake Yesu mara ya pili?**  
Angalia pia Mormoni 8:10,11; Estheri 12:17.

Mormoni 8:1-5 inasema: “Tazama mimi, Moroni, ninamaliza maandishi ya baba yangu, Mormoni. Tazama, nina vitu vichache tu vya kuandika, vitu ambavyo nimeamriwa na baba yangu. Na sasa ikawa kwamba baada ya vita kubwa na vya kutisha katika Kumora, tazama, Wanefi ambao walitorokea ka- na Walamani, mpaka wote walipoangamizwa. Na baba yangu pia aliuawa na hao, na ni mimi tu nimebaki peke yangu kuandika kisa cha kuhuzunisha cha kuan-gamizwa kwa watu wangu. Lakini tazama, wameenda, na ninatimiza amri ya baba yangu. Na ikiwa wataniua, sijui. Kwa hivyo nitaandika na kuficha maandiko katika ardhi; na haijalishi popote nitakapoenda. Tazama, baba yangu

alibuni haya maandishi, na ameandika kusudi la kufanya hivyo. Na tazama, ningeyaandika pia ikiwa ningekuwa na nafasi kwenye bamba, lakini sina; na mawe ya madini sina hata moja, kwani niko peke yangu. Baba yangu ameuawa vitani, na ukoo wangu wote, na sina marafiki wala popote pa kwenda; na kwa muda gani Bwana atanikubalia kwamba niishi sijui.”

**(57) Inakuwaje anaendelea kuandika baada ya kusema kwamba nafasi kwenye bamba ni ndogo na hakuna nyenzo ya kutengeneza mabamba hayo?**

Mormoni 9:7-10 (401-421 A.D.) inasema: “Na tena ninawazungumzia nyinyi ambao hukataa unabii wa Mungu, na kusema kwamba haifanyiki tena, kwamba hakuna ufunuo, wala unabii, wala vipawa, wala uponyaji, wala kuzungumza kwenye lugha za kigeni, na kutafsiri lugha; Tazama nawaambia, yule anayekana vitu hivi hajui injili ya Kristo; ndio, hajasoma maandiko; na ikiwa ameyasoma, hayaelewi. Kwani si tunasoma kwamba Mungu ni yule yule jana, na leo, na hata milele, na kwake hakuna kubadilika wala kivuli cha kugeukageuka? Na sasa, kama mmejiwazia, mungu anayebadilika, na ambaye ana kivuli cha kugeukageuka, aidha mmejidhanja mungu ambaye si Mungu wa miujiza.”

Moroni anadai yupo peke yake, hana mawe yenye madini (ambayo yatafaa kutengenezea “bamba”), na kwamba asingendelea kutunza rekodi kama angekuwa na nafasi ya kutosha juu ya hizo bamba. Anaendelea kurekodi anachokijua kama Mormoni 8-10, kitabu cha Esta (Esta 1:1-5), na kitabu cha Moroni (jumla yake ni kurasa 51).

**(58) Kwa nini Mormoni 9 (na Mormoni 7:25-29) vina-dai kwamba miujiza haijakoma wakati Agano Jipya linathibitisha kuwa nyakati za miujiza zimekoma katika karne ya kwanza B.K. (1 Wakorintho 13:8-13; Efeso 4:7-**

## **16; Yuda 3)?**

Esta 2:16-17 inasema: “Na Bwana alisema: Nenda ufa-nye kazi na ujenge, aina ya mashua ambayo mmejenga hadi sasa. Na ikawa kwamba kaka ya Yaredi alienda kazini, na pia ndugu zake, na kujenga mashuakama aina ambayo walikuwa wamejenga, kulingana na mafundisho ya Bwana. Na yalikuwa madogo, na yalikuwa mepesi juu ya maji, hata kama wepesi wa ndege arukaye juu ya maji. Na yalijengwa kwa aina moja kwamba yalikuwa yamekazwa sana, kwamba yangeshikilia maji kama vile sahani inavyofanya; na chini yake ilikuwa ya kukazwa sana kama sahani; na pande zilikuwa zimekazwa kama sahani; na ncha zilichungoka; na juu yake ilikuwa imekazwa kama sahani; na urefu wake ulikuwa urefu wa mti; na mlango wake, baada ya kufungwa, ulikazika kama sahani.”

**(59) Ikiwa Bwana ndiye aliyetoa maelekezo ya jinsi ya kujenga mashua, sasa kwaa nini ndugu wa Yaredi waliulizia hali ya mapungufu kama vile ya mfumo wa hewa na mwanga katika mistari ifuatayo?**

Esta 2:18-25 inaeleza: “Na ikawa kwamba kaka ya Yaredi aliomba kwa Bwana, akisema: Ee Bwana, nimefanya kazi ambayo uliniamuru, na nimetengeneza mashua kama vile ulivyoningoza. Na tazama, Ee Bwana, ndani zao hamna mwangaza; tutaijelekeza wapi? Na pia tutaangamia, kwani ndani yao hatuwezikupumua, isipokuwa tu hewa iliyomo ndani yao; kwa hivyo tutaangamia. Na Bwana akamwambia kaka ya Yaredi: Tazama, utatoboa tundu upande wa juu, na pia upande wa chini; na wakati mtakapokosa hewa mtafungua tundu na mpokee hewa. Na ikiwa itakuwa kwamba maji yataingia ndani kwenu, tazama, mtafungua tundu, ili msife katika mafuriko. Na ikawa kwamba kaka ya Yaredi alifanya vile, kulingana na Bwana alivyomwamuru. Na akaomba tena kwa Bwana

akisema: Ee Bwana, tazama nimefanya hata vile ulivyo-niamuru; na nimetayarisha vyombo kwa watu wangu, na tazama hakuna mwangaza ndani yao. Tazama, Ee Bwana, utakubali tuvuke haya maji mengi kwenye giza? Na Bwana akamwambia kaka ya Yaredi: Ungetaka nifanye nini ili muwe na mwangaza kwenye mashua yenu? Kwani tazama, hamwezi kuwa na madirisha, kwani yatavunjwa vipande vipande; wala hamwezi kubeba moto, kwani hamtaenda kwa mwanga wa moto. Kwani tazama, mtakuwa kama nyangumi katikati ya bahari; kwani milima ya mawimbi yatawaangukia. Hata hivyo, nitawarudisha juu tena kutoka kwenye kilindi cha bahari; kwani pepo hutoka katika mdomo wangu, na pia mvua na mafuriko hutolewa na mimi. Na tazama, ninawatayarisha dhidi ya vitu hivi; kwani hamwezi kuvuka hiki kilindi kikubwa isipokuwa niwatayarishie dhidi ya mawimbi ya bahari, na pepo ambazo zimevuma, na mafuriko ambayo yatakuja. Kwa hivyo unataka nikutayarishie nini ili muwe na mwangaza ndani ya kilindi cha bahari?”

**(60) Kwa nini Mungu anawaambia ndugu zake Yaredi kufanya tundu katika uvungu wa mashua? Hili litasaidiaje katika kuingiza hewa ya wao kupumua? Wataizuiaje mashua yenye tundu uvunguni isizame?** Kifungu kinasema ilichukua siku 344 kusafiri hadi Marekani (Esta 6:11).

Esta 8:1-15 inaeleza: “Na ikawa kwamba alimzaa Omeri, na Omeri alitawala badala yake. Na Omeri akamzaa Yaredi; na Yaredi akazaa wana na mabinti. Na Yaredi aliasi dhidi ya baba yake, na akaenda kuishi katika nchi ya Hethi. Na ikawa kwamba aliwadanganya watu wengi, kwa sababu ya ujanja wa maneno yake, mpaka alipopata nusu ya ule ufalme. Na baada ya kupata nusu ya ufalme alifanya vita na baba yake, na akamweka baba yake kwenye utumwa, na akamfanya kutumika katika utum-

wa; Na sasa, katika siku za utawala wa Omeri alikuwa katika utumwa nusu ya maisha yake. Na ikawa kwamba alizaa wana na mabinti, miongoni mwao ambamo walikuwa Esromu na Koriantumuri; Na walikasirika sana kwa sababu ya vitendo vya Yaredi kaka yao, mpaka kwamba waliunda jeshi na kufanya vita na Yaredi. Na ikawa kwamba walifanya vita na yeye wakati wa usiku. Na ikawa kwamba baada ya kuua jeshi la Yaredi walikuwa kariibu kumuua yeye pia; na aliwasihi kwamba wasimuue, na angetoa ufalme kwa baba yake. Na ikawa kwamba walimwachiamasha yake. Na sasa Yaredi alihuzunika sana kwa sababu ya kupoteza utawala, kwani alikuwa ameweka moyo wake kwa ufalme na utukufu wa ulimwengu. Sasa binti wa Yaredi akiwamrembo sana, na aki-ona huzuni wa baba yake, alifikiria kutafuta mpango ambamo kwake angerudisha utawala kwa baba yake. Sasa binti wa Yaredi alikuwa mrembo sana. Na ikawa kwamba aliongea na baba yake, na kusema kwake: Kwa nini baba yangu una huzuni sana? Hujasoma maandishi ambayo babu zetu walileta kutoka ng'ambo ya kilindi kikubwa? Tazama, hakuna historia kuhusu wale wa kale, kwamba wao kwa mipango yao ya siri walipata falme na utukufu mkuu? Na sasa, kwa hivyo, acha baba yangu amtumainie Akishi, mwana wa Kimnori; na tazama, mimi ni mrembo, na nitacheza mbele yake, na nitampendeza, kwamba atatamani kwamba niwe mke wake; kwa hivyo ikiwa atataka kwamba umpatie mimi kama mke wake, ndipo utasema: Nitakupatia tu ikiwa utaniletea kichwa cha baba yangu, mfalme. Na sasa Omeri alikuwa rafiki ya Akishi; kwa hivyo, wakati Yaredi alipokuwa amemtumainia Akishi, binti wa Yaredi alicheza mbele yake kwamba akampendeza, mpaka kwamba alimtaka awe mke wake. Na ikawa kwamba alisema kwa Yaredi: Nipatie mimi awe mke wan-



gu. Na Yaredi akamwambia: Nitamkabidhi kwako, ikiwa utaniletea kichwa cha baba yangu, mfalme. Na ikawa kwamba Akishi alikusanya kwenye nyumba ya Yaredi jamaa zake wote, na kuwaambia: Mtaapa kwangu kwamba mtakuwa waaminifu kwangu kwa kitu ambacho nitataka kutoka kwenu? Na ikawa kwamba wote waliapa kwake, katika yule Mungu wa mbinguni, na pia na mbingu, pia na dunia, na vichwa vyao, kwamba yeyote atakayetofautiana na usaidizi ambao Akishi alitaka atapoteza kichwa chake; na yeyote atakayetoa wazi kitu chochote ambacho Akishi amewafahamisha, huyo huyo atapoteza maisha yake. Na ikawa kwamba hivyo ndivyo walikubaliana na Akishi. Na Akishi alitoa kiapo kwaoambacho kilitolewa na wale wa kale ambao pia walitaka uwezo, ambao ulitolewa hata kutoka kwa Kaini, ambaye alikuwa muuaji kutoka mwanzo.”

**(61) Je, Esta 8:1-15 imechukuliwa kutoka katika habari ya Yohana mbatizaji, na Herodia katika Marko 6:14-29?**

Esta 15:30-31 inaeleza: “Na ikawa kwamba wakati Koriantumuri alikuwa amelalia upanga wake, ili apumzike kidogo, alikata kichwa cha Shizi. Na ikawa kwamba baada ya kukata kichwa cha Shizi, kwamba Shizi alijiinua kwa mikono yake na kisha akaanguka; na baada ya kujitahidikuvuta pumzi, akafa.”

**(62) Ilikuwaje Shizi ahangaike kupumua baada ya kukatwa kichwa?**

Moroni 7:45 inasema: “Na hisani huvumilia, na ni karimu, na haina wivu, na haijivuni, haitafuti mambo yake, haifutuki kwa upesi, haifikirii mabaya, na haifurahii uovu lakini hufurahi katika ukweli, huvumilia vitu vyote, huamini vitu vyote, hutumaini vitu vyote, hustahamili vitu vyote.”

**(63) Kwa nini Mormoni 7:45 inatumia neno “kwa ura-**

## **hisi (easily)” ambalo linapatikana katika tafsiri ya King James, lakini halipatikani katika kifungu cha asili cha lugha ya Kiyunani?**

### **Hitimisho**

Katika kuhitimisha, baada ya kuchunguza kitabu cha Mormoni, unadhani kinaweza kuwa neno la Mungu kweli huku kikiwa na:

(a) Kinapingana na Biblia juu ya mpangilio wa ufunuo wa siri ya Kristo, kipindi sahihi cha nyakati za miujiza, kipindi sahihi cha giza Yesu aliposulibiwa, n.k...

(b) Nukuu nyingi kutoka katika Maandiko ya Agano Jipya ambazo zilikuwa hazijaandikwa bado.

(c) Udumishaji wa makosa ya waandishi wa tafsiri ya Biblia toleo la King James.

(d) Historia ya makosa ya kikronolojia (mpangilio) kama vile Kanisa la Kristo kwamba lilianza kabla ya karne ya kwanza B.K. jina “Mkristo” kwamba walipewa kabla ya Matendo 11:26, n.k ...

(e) Karne kumi na tisa za mjadala wa kitheolojia juu ya ubatizo wa watoto, umilenia, ...

(f) Matukio yasiyo ya kihistoria kama vile Wayahudi kuji-funza kuandika Kimsri kilichorekebisha juu ya bamba ya chuma; Wayahudi kutoka kabila la Manasse kuhudumu kama makuhani na kudai kwamba walitunza sheria ya Musa; kujenga hekalu lililojengwa kama lile la Sulemani likiwa na idadi ndogo ya watu; makutano ambayo yote yaligusa vidonda vya Yesu mmoja baada ya mwingine, jambo ambalo lingechukua masaa kadhaa kukamilika; na kuamini kwamba mababu wa wazawa wa Marekani walikuwa Wayahudi waliokuja kutoka katika ulimwengu wa kale katika miaka ya 600 K.K. Jibu ni **HAPANA** yenye sauti kubwa!

Unaweza kuona kutoka katika uchambuzi huu kwamba **ki-**

**tabu cha Mormon** ni moja kati ya udanganyifu mkubwa ambao haukuwahi kufikiriwa, na walaghai wenye hila walijaribu kugeuza ujumbe wake uonekane kuwa umetoka kwa Mungu.

## Bibliografia

Bales, James. *The Book of Mormon?* Fort Worth, TX: The Manney Company, 1958.

Miller, Dave. “Questions And Answers: “Is there Proof of Bible Inspiration?” (<https://apologeticspress.org/APContent.aspx?category=13&article=1379>). Date accessed: August 5, 2021.

Potter, George (1999). “A New Candidate in Arabia for the “Valley of Lemuel.” *Journal of Book of Mormon Studies*. 8 (1): 54-63.

Summers, Gary. *Mormonism*. ed. David Brown, Spring, TX: Contending For The Faith, 2001.

Tolle, James. *Is The Book of Mormon From God?* San Fernando, CA: Tolle Pub., 1957.

\* Mawazo haya yalichukuliwa na kufupishwa kutoka katika tovuti: <https://www.gotquestions.org/genealogies-Israel.html>.

\*\* Mawazo haya kwa kiasi kikubwa yametoka katika *Braden-Kelley Debate*. The Old Paths Book Club, Rosemead, California, 1955, 22-23.

# Kiambatanisho

**Kiambatanisho hiki kina orodha ya marejeo ya Biblia ambayo mimi binafsi naamini yaliingizwa katika kitabu cha Mormoni. Baadhi ya marejeo ni nukuu, mifano, au vivuli (kopi) kutoka eneo mojawapo la Biblia. Nimejaribu kutenda haki na kuwa makini. Nukuu kutoka Kitabu cha Mormoni zitakuwa upande wa kushoto wa alama “/”, pamoja na kifungu cha Biblia upande wa kulia ambacho nukuu hiyo ilitokea.**

## 1 Nefi

**1 Nefi 1:1/1** Wakorintho 4:1; **1:3/Wagalatia** 6:11; **1:14/Ufunuo** 15:3; **1:18/1** Yohana 1:3; **1:20/Mathayo** 21:33-46; **2:10/1** Wakorintho 15:58; **2:18/Marko** 3:5; **2:24/2** Petro 3:2; **3:21/1** Wakorintho 7:19; **3:27/Ufunuo** 12:6; **4:6/Luka** 4:1; **4:13/Yohana** 11:50; **5:8/Matendo** 12:11; **5:13/Matendo** 3:21; **5:18/Ufunuo** 14:6; **6:4/Yohana** 17:14; **6:8/Marko** 3:5; **7:8/Marko** 3:5; **8:20/Mathayo** 13:38; **10:4/Matendo** 3:22-23; Yohana 4:42; **10:7/Mathayo** 3:3; **10:8/Yohana** 1:23,26-27; Luka 3:16; **10:9/Yohana** 1:28; **10:10/Yohana** 1:29; **10:12/Warumi** 11:17-19; **10:14/Warumi** 11:24; Waebrania 11:6; **10:18/Waebrania** 13:8; Mathayo 25:34; **10:19/Waebrania** 11:6; **10:21/Warumi** 14:10; **11:1/Mathayo** 4:8; **11:7/Yohana** 1:34; **11:19/Ufunuo** 17:3; **11:21/Yohana** 1:29; **11:22/Warumi** 5:5; **11:27/Yohana** 1:24; **11:30/Yohana** 1:51; **11:31/Mathayo** 10:1; **11:35-36/Ufunuo** 21:14; 14:6; **12:1/Ufunuo** 20:8; **12:2/Mathayo** 24:6; **12:7/Yohana** 15:16; Matendo 10:44; **12:9/Ufunuo** 21:14; Mathayo 19:28; **12:10,11/Ufunuo** 7:14; **12:18/Luka** 16:26; **12:21/Mathayo** 24:6; **13:7/Ufunuo** 13:2; 17:4; **13:27/**

Matendo 13:10; **13:34**/Ufunuo 17:5; **13:37**/Mathayo 10:22; Luka 2:10; **13:42**/Mathayo 19:30; **14:10**/Ufunuo 17:5; **14:11**/Ufunuo 17:1; **14:15**/Mathayo 24:6; **14:16**/Ufunuo 17:5; **15:3**/2 Petro 3:16; **15:11**/Mathayo 21:22; **15:13**/Warumi 11:24-25; **15:15**/Yohana 15:1; **15:18**/Luka 1:73; **15:24**/Waefeso 6:16; **15:30**/Ufunuo 14:11; **16:2**/Yohana 6:40; **16:38**/Mathayo 4:11; **17:30**/2 Wakorintho 4:4; **20**/Isaya 48; **21**/Isaya 49; **22:5**/Mathayo 10:22; **22:13**/Ufunuo 19:2; **22:14**/Matendo 13:10; **22:15**/Malaki 4:1; **22:17**/1 Wakorintho 3:15; **22:18**/Matendo 2:19; **22:25**/Yohana 10:16; **22:31**/Mathayo 10:22; 24:13.

## 2 Nefi

**2 Nefi 1:1**/Marko 5:19; **1:18**/2 Timotheo 2:26; **1:23**/2 Wakorintho 6:7; **1:26**/Waebrania 4:12; **2:3**/Wagalatia 4:4-5; **2:5**/Wagalatia 2:16; **2:6**/Yohana 1:14-16; **2:8**/Yohana 10:17-18; **2:13**/Warumi 4:15; **2:14**/Warumi 15:4; **2:26**/Wagalatia 4:4-5; **2:30**/Luka 10:42; **3:5**/1 Wakorintho 4:5; **3:13**/Waebrania 11:34; **4:17**/Warumi 7:24; **4:18**/Waebrania 12:1; **4:35**/Yakobo 1:5; **9:2**/Matendo 3:21; **9:7**/1 Wakorintho 15:51-53; **9:9**/2 Wakorintho 11:14; **9:15**/Yohana 5:24; 2 Wakorintho 5:10; **9:16**/Mathayo 24:35; 25:41; Ufunuo 22:11; 14:11; **9:18**/Waebrania 12:2; Mathayo 25:34; **9:22**/Mathayo 10:22; **9:23**/Matendo 2:38; **9:34**/Luka 10:15; **9:38**/Yohana 8:24; **9:39**/Warumi 8:6; **9:41**/Mathayo 7:13,14; **9:42**/Mathayo 7:8; **9:43**/Mathayo 11:25; **10:4**/Mathayo 11:21; **10:16**/Wagalatia 3:28; **12-24**/Isaya 2-14; **25:4**/Ufunuo 19:10; **25:12**/Mathayo 24:6-7; **25:13**/Malaki 4:2; **25:14**/Matendo 5:39; **25:18**/Yohana 12:48; **25:20**/Matendo 4:12; **25:23**/Waefeso 2:8-9; **25:25**/Warumi 7:4; **25:29**/Mathayo 22:37; Yohana 6:37; **26:4**/Malaki 4:1; **26:5**/Mathayo 21:44; **26:10**/Yohana 3:19; **26:13**/Ufunuo 14:6; **26:24**/Yohana 12:32; **26:27**/Matendo 17:30; **26:30**/1 Wakorintho 13:2; **26:33**/Wagalatia 3:28; **27**/Isaya 29; **27:23**/Waebrania 13:8; **28:7,8**/1 Wakorintho 15:32;

Luka 12:48; **28:11**/Warumi 3:12; **28:15**/Luka 10:15; Matendo 13:10; **28:23**/Ufunuo 20:13; **28:26**/Matendo 2:38; **28:28**/Mathayo 7:24-27; **28:30**/Mathayo 13:12; **30:1**/Luka 13:5; **30:6**/Matendo 9:18; **30:17**/Mathayo 10:26; Waefeso 5:11,13; **31:4**/Yohana 1:29; **31:5,6**/Mathayo 3:15,16; **31:9**/Mathayo 7:13,14; **31:11**/Matendo 2:38; **31:13**/Mathayo 3:11; 1 Wakorintho 13:2; **31:14**/Marko 16:17; Mathayo 3:11; **31:15**/Mathayo 10:22; **31:18**/Mathayo 7:13,14; **31:19**/Wakolosai 2:5; **31:21**/Matendo 4:12; **32:1**/Marko 2:8; **32:4**/Mathayo 7:7; **32:6**/1 Timotheo 3:16; **32:9**/Luka 18:1; **33:9**/Mathayo 7:13,14.

### **Yakobo**

**Yakobo 2:10**/Mathayo 5:8; **3:1-3**/Mathayo 5:8; **3:11**/Ufunuo 21:8 ; **4:8**/Warumi 11:33; **4:15-17**/Mathayo 21:42; **5:9**/Luka 13:7-8; Warumi 11:17; **5:20,22,23,32**/Yohana 12:24; **5:32,35**/1 Wakorintho 13:2; **5:39**/Luka 6:43; **5:42,46,49**/Mathayo 3:10; **5:47**/Luka 13:7-8; **5:63**/Mathayo 19:30; **5:64**/Luka 13:8; **5:66**/Mathayo 3:10; **5:76**/Luka 13:8; **6:3**/2 Petro 3:10; **6:6**/Waebrania 3:7-8; **6:7**/Mathayo 3:10; **6:8**/Matendo 2:38; 1 Wathesalonike 5:17-19; **6:10**/Ufunuo 14:11; 21:8; **6:11**/Mathayo 7:13-14; **7:5**/Mathayo 4:11; **7:14**/Luka 22:42; **7:19**/Mathayo 12:31-32; **7:24**/1 Timotheo 2:4.

### **Enoshi, Yaromu, Omni, na Maneno ya Mormoni**

**Enoshi 1:1**/Waefeso 6:4; **1:2**/Matendo 10:43; **1:5**/Luka 5:20; **1:6**/Tito 1:2; **1:8**/Mathayo 9:22; **1:14**/Wagalatia 1:14; **1:15**/Yakobo 1:6; **1:26**/Warumi 9:1; **1:27**/1 Wakorintho 15:53-54; Mathayo 25:34; Yohana 14:2-3. **Yarom 1:4**/2 Wakorintho 13:14. **Omni 1:25**/1 Wakorintho 12:4-11; **1:26**/Mathayo 10:22. **Maneno ya Mormoni 1:15**/Mathayo 24:34; Tito 1:11; **1:16**/2 Petro 2:1.

## Mosia

**Mosia 1:5**/Wagalatia 1:14; **1:8**/Yohana 20:30; **1:13**/Mathayo 16:4; **1:17/2** Petro 3:2; **2:15**/Matendo 23:1; **2:21**/Matendo 17:24; Luka 17:10; **2:34**/Matendo 3:21; **2:37**/Matendo 13:10; 17:24; **2:38**/Mathayo 3:12; **3:3**/Luka 2:10; **3:5**/Marko 7:37; Ufunuo 19:6; **3:9**/Yohana 1:11; Mathayo 11:18; **3:12**/Matendo 20:21; **3:13**/Matendo 2:38; **3:17**/Matendo 4:12; **3:18/1** Wakorintho 11:29; Mathayo 18:3,4; **3:19/1** Wakorintho 2:7,11,14; **3:21**/Matendo 20:21; **3:26**/Ufunuo 14:10; **3:27**/Ufunuo 20:10,14; **4:7**/Mathayo 25:34; **4:8**/Matendo 4:12; **4:12**/Matendo 2:38; **4:14**/Matendo 13:10; **4:15**/Yohana 13:34,35; **4:20**/Matendo 2:38; 2:17; Tito 1:11; **4:21**/Mathayo 21:22; **4:26**/Mathayo 25:35,36; **4:27/1** Wakorintho 9:24; 14:40; **5:5**/Ufunuo 14:10; **5:8**/Waefeso 1:22,23; Wagalatia 5:1; Matendo 4:12; **5:13**/Waebrania 4:12; **5:15/1** Wakorintho 15:58; Ufunuo 19:6; **8:17/1** Wakorintho 4:5; **12:26**/Matendo 13:10; **13:1**/Matendo 22:22; **13:3**/Matendo 23:3; **13:4**/Wagalatia 4:16; **13:10**/Waebrania 10:1; **13:12-24**/Kutoka 20; **13:31**/Wakolosai 2:17; **14**/Isaya 53; **15:11**/Matendo 3:21; 2:38; **15:13**/Matendo 3:21; **15:19**/Mathayo 25:34; **15:21,22,24**/Ufunuo 20:5-6; **15:26**/Yohana 8:24; 15:28/Ufunuo 5:9; **16:2**/Mathayo 8:12; **16:3**/Ufunuo 12:9; 2 Wakorintho 11:3; Yakobo 3:15; **16:7/1** Wakorintho 15:20,55; **16:8/1** Wakorintho 15:54-55; **16:9**/Yohana 1:4; 8:12; **16:10/1** Wakorintho 15:53-54; **16:11**/Yohana 5:29; **16:14**/Waebrania 10:1; **17:19**/Matendo 7:59; **18:8**/Wagalatia 6:2; **18:9**/Warumi 12:15; Ufunuo 20:5,6; **18:10**/Matendo 2:17; **18:12**/Matendo 2:17; **18:13**/Mathayo 25:34; **18:14**/Matendo 8:39; 2:4; **18:17**/Matendo 20:28; 2:47; **18:18**/Matendo 1:3; **18:19**/Matendo 3:21; **18:20**/Matendo 20:21; **18:21**/Waefeso 4:5; Wakolosai 2:2; **19:3**/Matendo 9:1; **21:13**/Wagalatia 5:1; **23:13**/Wagalatia 5:1; **23:15**/Marko 12:33; **23:22**/Yohana 6:40; **23:23**/Wagalatia 2:4; **25:15**/Matendo 20:21; **25:18**/Matendo 20:28; **25:24**/

Matendo 2:17; **26:21**/Yohana 10:27; **26:22**/Mathayo 16:18; 3:11; **26:27**/Mathayo 7:23; 25:41; **26:31**/Mathayo 6:14-15; **26:37**/Waefeso 5:15; **26:39**/1 Wathesalonike 5:17-19; **27:11-23**/Matendo 9:3-18; **27:10**/Wagalatia 1:13; **27:13**/Matendo 9:4; **27:14**/1 Timotheo 2:4; **27:24**/Yohana 3:7; **27:25**/Yohana 3:7; **27:26**/2 Wakorintho 5:17; 1 Wakorintho 6:9-11; **27:29**/Matendo 8:22-23; **27:31**/Yohana 12:48; Wafilipi 2:10-11; **27:36**/1 Timotheo 2:4.

### Alma

**Alma 1:4**/Yohana 6:44; **1:25**/1 Wakorintho 15:58; 7:19; **1:30**/Wagalatia 3:28; **2:1**/1 Wakorintho 1:20; **2:4**/Wagalatia 1:13; **3:27**/Ufunuo 19:10; **4:13**/Ufunuo 19:10; **4:14**/Matendo 2:38; **4:16**/Matendo 20:17; **4:19**/2 Petro 3:2; **4:20**/Ufunuo 19:10; **5:7**/2 Wathesalonike 1:9; **5:13**/1 Wathesalonike 1:9; **5:14**/1 Yohana 3:9; **5:15**/1 Wakorintho 15:51-53; **5:16**/Mathayo 25:34; Tito 3:5; **5:21**/Ufunuo 7:14; **5:24**/Mathayo 8:11; Ufunuo 7:14; **5:25**/Yohana 8:44; **5:27**/Ufunuo 7:14; **5:28**/Mathayo 3:1,2; **5:34**/Ufunuo 21:6; **5:35**/Mathayo 3:10; **5:37**/Mathayo 9:36; **5:38-41**/Yohana 10:11,14; **5:42**/Warumi 6:23; **5:46**/Waefeso 1:17; **5:47**/Ufunuo 19:10; **5:48**/Yohana 1:14,29; **5:49**/Yohana 3:1-8; **5:50**/Mathayo 3:2; **5:52**/Mathayo 3:10; **5:53**/Waebrania 10:29; **5:54**/Mathayo 3:8; **5:56**/Luka 3:9; **5:57**/2 Wakorintho 6:17; Yohana 10:11; **5:58**/Wafilipi 4:3; **5:59**/Mathayo 12:11; **5:60**/Mathayo 7:15; **5:62**/Mathayo 3:11; Ufunuo 2:7; **6:2**/Matendo 2:38; Mathayo 3:11; **6:8**/Ufunuo 19:10; **7:6**/Matendo 2:38; **7:9**/Mathayo 3:2; **7:14**/Yohana 1:29; Yohana 3:3; 1 Yohana 1:9; **7:15**/Waebrania 12:1; **7:20**/Yakobo 1:17; **7:21**/Matendo 17:24; **7:24**/1 Wakorintho 13:13; **7:25**/Matendo 3:21; Mathayo 8:11; Ufunuo 7:14; **8:10**/Mathayo 3:11; **8:24**/Waefeso 1:17; Ufunuo 19:10; **8:30**/Luka 1:15; **9:2**/Mathayo 24:35; **9:3**/Mathayo 24:35; **9:8**/Mathayo 17:17; **9:15**/Mathayo 11:22; **9:16,17**/Wagalatia 1:14; **9:21**/Matendo 2:38; **9:23**/Mathayo 10:15; **9:25**/Mathayo



3:2; **9:26**/Yohana 1:14; **9:28**/Marko 1:3; **9:30**/Mathayo 3:8; **10:12**/Ufunuo 19:10; **10:17**/Mathayo 17:17; **10:20**/Mathayo 3:2; **10:22,23**/Yakobo 5:16; **11:41**/Ufunuo 20:12; **11:44**/Luka 21:18; Wagalatia 3:28; **11:45**/Yohana 5:24; **12:3**/Matendo 5:4; **12:9/1** Wakorintho 4:1; **12:11/2** Timotheo 2:26; **12:12/1** Wakorintho 15:51-53; **12:14**/Mathayo 12:37; **12:15**/Mathayo 3:8; **12:16**/Yohana 8:24; **12:17**/Ufunuo 14:11; **12:27**/Waebrania 9:27; **12:30**/Waefeso 1:4; **12:34**/Yohana 3:16; Matendo 2:38; Waebrania 4:3; **12:35**/Waebrania 3:11; **12:36**/Waebrania 4:3; **13:3**/Matendo 2:23; **13:5**/Mathayo 25:34; **13:6**/Waebrania 4:3; **13:7**/Waebrania 7:3; **13:9**/Waebrania 7:3; Yohana 1:14; **13:11**/Ufunuo 7:14; **13:13**/Mathayo 3:8; **13:14-18**/Waebrania 7:1-10; **13:20/2** Petro 3:16; **13:22**/Luka 2:10; 13:26/Ufunuo 19:10; **13:28**/Mathayo 26:41; 1 Wakorintho 10:13; **13:29**/Yohana 6:54; **13:30**/Ufunuo 2:11; **13:31**/Yohana 20:30; **14:1**/Yohana 5:39; **14:3**/Mathayo 1:19; **14:11**/Yohana 6:54; **14:14**/Ufunuo 20:10; **14:19**/Yohana 19:10; **14:22,26-28**/Matendo 16:23-27; **14:27**/Mathayo 27:51; **15:11**/Matendo 3:7-10; **15:14**/Mathayo 3:5-6; **16:5**/Ufunuo 19:10; **16:15**/Mathayo 3:5-6; **16:17**/Yohana 15:1-6; **17:2**/Matendo 17:11; 1 Timotheo 2:4; **17:3**/Ufunuo 19:10; Waefeso 1:17; **17:4/1** Timotheo 2:4; **17:31**/Yohana 16:33; **18:32**/Waebrania 4:12; **19:5**/Yohana 11:39; **19:8**/Luka 8:52; **19:10**/Mathayo 8:10; **20:23**/Marko 6:23; **21:16**/Luka 4:1; **21:17/1** Timotheo 2:4; **22:1**/Luka 4:1; **22:6**/Yohana 6:54; **22:14/1** Wakorintho 15:54-55,58; **22:15**/Marko 10:17; **22:18**/Yohana 6:54; **23:6,15/1** Timotheo 2:4; **24:15,16**/Yohana 6:54; **24:30**/Waebrania 6:4; 2 Petro 2:20-22; **26:6**/Yohana 6:54; **26:7**/Yohana 6:40,44; **26:12**/Wafilipi 4:13; **26:20**/Luka 16:26; **26:21/1** Wakorintho 2:11-14; **26:24/1** Timotheo 2:4; **26:30/1** Yohana 1:4; **26:35**/Yohana 1:12; **27:4**/Mathayo 18:27; **27:26/2** Wakorintho 5:17; **27:28/1** Wakorintho 15:54; **29:3**/Wafilipi 4:11; **29:17**/Mathayo 8:11; **30:22**/Matendo 13:10; **30:43,49-50**/Luka 1:18-20;

**31:10**/Luka 22:46; **31:11**/Matendo 13:10; **31:17**/Waebrania 13:8; **31:37**/Mathayo 6:31; **32:8**/Mathayo 11:29; **32:13,15**/Mathayo 10:22; **32:17**/Mathayo 16:1; **32:21**/Waebrania 11:1; **32:28**/Luka 8:11; **32:38**/Mathayo 13:6; **32:41**/Yohana 4:14; **33:2**/Yohana 5:39; **33:19**/Yohana 3:14; **33:23**/Yohana 4:14; **34:13**/Mathayo 5:18; **34:23**/Matendo 13:10; **34:29**/Mathayo 5:13; **34:30**/Luka 3:8; **34:31/2** Wakorintho 6:2; **34:33**/Yohana 9:4; **34:36**/Mathayo 8:11; Ufunuo 7:14; Matendo 17:24; **34:37**/Wafilipi 2:12; **34:38**/Yohana 4:14; **36:3**/Yohana 6:54; **36:18**/Matendo 8:23; **36:23**/Yohana 1:13; **36:24**/Luka 1:15; **36:26**/Yohana 1:13; **36:28**/Yohana 6:54; **37:15**/Luka 22:31; **37:19/1** Timotheo 2:4; **37:33-34**/Mathayo 11:29; **37:37**/Yohana 6:54; **38:2**/Mathayo 10:22; **38:5**/Yohana 6:54; **38:6**/Marko 3:28-29; **38:8**/Matendo 2:38; **38:9**/Mathayo 11:29; Yohana 8:12; **39:8**/Yohana 6:54; **39:9/1** Yohana 2:16; **39:15**/Yohana 1:29; **40:2/1** Wakorintho 15:51-53; **40:13**/Mathayo 13:42-43; **40:14**/Waebrania 10:27; **40:15-17**/Ufunuo 20:6; **40:21**/Ufunuo 20:12; **40:22**/Matendo 3:21; **40:23**/Luka 21:18; **40:24**/Matendo 3:21; **40:25-26**/Mathayo 13:42-43; **41:1**/Matendo 3:21; **41:3**/Ufunuo 20:12; **41:4/1** Wakorintho 15:51-53; **41:11**/Matendo 8:22-23; Waefeso 2:12; **42:6**/Waebrania 9:27; **42:23**/Ufunuo 20:12; **42:26**/Waefeso 1:4; **42:27**/Ufunuo 22:17; **43:2**/Ufunuo 19:10; Waefeso 1:17; **43:10**/Yohana 4:24; **49:7,26**/Wagalatia 5:1; **57:21**/Mathayo 9:29; **58:40**/Wagalatia 5:1; **60:23**/Mathayo 23:26; **60:26/2** Wathesalonike 1:4; **61:9,12,21**/Wagalatia 5:1; **62:45**/Matendo 2:38; **62:46**/Matendo 20:28.

## **Helamani**

**Helamani 3:29**/Waebrania 4:12; Waefeso 6:11; Mathayo 7:13,14; **3:30**/Luka 16:26; Mathayo 8:11; 4:12,24/Ufunuo 19:10; **4:24**/Matendo 17:24; **5:8**/Mathayo 6:20; **5:9**/Matendo 4:12; **5:19**/Wagalatia 1:14; **5:32**/Mathayo 3:2; **5:44/1** Petro

1:8; **5:47/1** Petro 1:20; **5:48**/Marko 1:10,13; **6:1**/Mathayo 5:20; **6:8**/Yakobo 4:13; **6:23**/Warumi 6:23; **6:39**/Mathayo 7:6; **7:4**/Marko 7:8; **7:10**/Mathayo 21:33; **7:18**/Yohana 10:11,27; **8:14,15**/Yohana 3:14,15; **8:17**/Yohana 8:56; **8:24**/Waefeso 1:10; **8:25**/Mathayo 6:19,20; Warumi 2:5; **9:2**/Matendo 12:11; **10:7,8**/Mathayo 16:19; 18:18; **10:9**/Mathayo 21:21; **12:13,17**/Mathayo 17:20; **12:24**/Yohana 1:16; **12:26**/Yohana 5:29; **13:6**/Matendo 20:21; **13:25**/Mathayo 23:30,31; **13:29**/Mathayo 17:17; 23:16; Yohana 3:19; **13:33**/Mathayo 23:30,31; **14:2**/Yohana 1:12; **14:18**/Mathayo 3:10; Ufunuo 21:8; **14:25**/Mathayo 27:52; **15:1-4**/Mathayo 23:38; Luka 23:28-29; 13:3; **15:5**/Waefeso 5:15; **15:6,7/1** Timotheo 2:4; **15:8**/Wagalatia 5:1; **15:11/1** Timotheo 2:4; **15:15**/Mathayo 11:21; **16:10**/Waefeso 5:15; **16:14**/Luka 2:10.

### 3 Nefi

**3 Nefi 1:13**/Yohana 16:33, Matendo 3:21; **1:25**/Mathayo 5:18; **3:19**/Mathayo 6:19; **5:1**/Matendo 3:21; **5:5**/Matendo 9:1; **5:8**/Yohana 21:25; **6:14/1** Wakorintho 15:58; **7:16**/Marko 3:5; **7:19**/Mathayo 10:1; **9:15**/Yohana 14:10,11; 17:5-6; **9:16,17**/Yohana 1:11,12; **9:20**/ Mathayo 3:11; **9:22**/Marko 10:14,15; Yohana 10:17; **10:4,5,6**/Mathayo 23:37; **10:7**/Mathayo 23:38; **10:13**/Matendo 2:19; **11:7**/Mathayo 17:5; **11:11**/Yohana 8:12; 18:11; **11:14**/Yohana 20:27; **11:17**/Mathayo 28:9; **11:25**/Mathayo 28:19; **11:27**/Yohana 17:21; **11:32**/Yohana 7:16; Matendo 17:30; **11:33-34**/Marko 16:16; **11:37**/Mathayo 18:3; **11:38**/Matendo 2:38; **11:39**/Mathayo 16:18; **11:40**/Mathayo 7:24-27; 16:18; **12:1**/Mathayo 3:11; **12:2**/Matendo 2:38; **12-14**/Mathayo 5-7; **15:1**/Yohana 6:54; **15:17**/Yohana 10:16; **16:3**/Yohana 10:3,4; **16:15**/Mathayo 5:13; **17:10**/Luka 7:38; **17:12,21**/Marko 10:13,16; Yohana 11:35; **18:6-11**/Luka 22:17-20; **18:11-16**/Matendo 2:38; Mathayo 7:24-27; **18:18**/Mathayo 26:41; Luka 22:31; **18:20**/Yo-

hana 16:23; **18:28,29**/1 Wakorintho 11:27-29; **19:18**/Yohana 20:28; **19:20**/Yohana 17:6; **19:23**/Yohana 17:20-22; **19:25**/Mathayo 17:2; **19:28-29**/Yohana 17:9; **19:35**/Mathayo 8:10; **20:8**/1 Wakorintho 11:23-25; **21:6**/Matendo 2:38; **23:9**/Mathayo 27:52-53; **26:3**/2 Petro 3:10; **26:5**/Yohana 5:29; **26:17**/Matendo 2:38; Luka 1:15; **26:18**/2 Wakorintho 12:1-3; **26:19**/Matendo 2:44; 26:21; **27:1**/Matendo 2:38; **27:11**/Mathayo 3:10; **27:13**/Yohana 6:38; **27:14**/Yohana 12:32; **27:17**/Mathayo 3:10; **27:22**/Yohana 6:54; **27:28**/Yohana 15:16; **27:29**/Mathayo 7:8; **27:32**/Mathayo 6:19; Yohana 17:12; **27:33**/Mathayo 7:13,14; **28:7**/Mathayo 16:28; **28:8**/1 Wakorintho 15:51-53; **28:10**/Mathayo 8:11; Luka 13:29; **28:13-15**/2 Wakorintho 12:2-4; **28:31**/Warumi 14:10; **28:35**/Mathayo 26:24; **29:7**/Yohana 17:12.

#### 4 Nefi

**4 Nefi 1:1**/Matendo 8:15; 2:38; **1:3**/Matendo 2:44; 4:32; Waebrania 6:4; **1:5**/Mathayo 11:5; Marko 7:37; **1:11**/Mathayo 22:30; **1:30**/Mathayo 27:51; **1:32**/Danieli 3; **1:33**/Danieli 6.

#### Mormoni

**Mormoni 1:15**/1 Petro 2:3; **2:19**/Yohana 6:44; **3:2**/Matendo 2:38; **3:12**/Waebrania 11:6; **3:15**/Warumi 12:19; **3:18**/Mathayo 19:28; Ufunuo 20:13; **3:19**/Mathayo 19:28; **3:20**/2 Wakorintho 5:10; **3:22**/2 Wakorintho 5:10; **5:14**/Mathayo 16:16; Waefeso 3:11; **5:16**/Waefeso 2:12; **5:21**/Yakobo 5:16; **6:21**/1 Wakorintho 15:53; **7:5**/1 Wakorintho 15:54,56; **7:6**/2 Wakorintho 5:10; **7:8**/Matendo 2:38; **7:10**/Mathayo 3:11; **8:17**/Mathayo 5:22; **8:20**/Warumi 12:19; **8:21**/Mathayo 3:10; **8:24**/Mathayo 17:20; **8:30**/Mathayo 24:6-7; **8:31**/Matendo 8:23; 8:34/Ufunuo 1:1; **8:41**/Ufunuo 16:6; **9:2**/2 Petro 3:10; **9:5**/Mathayo 3:12; **9:6**/Ufunuo 7:14; **9:7**/1 Wakorintho 12:10; **9:9**/Waebrania 13:8; Yakobo 1:17; **9:12-13**/1 Wako-

52

rintho 15:21-22; **9:13**/1 Wakorintho 15:52; **9:14**/Ufunuo 22:11; **9:21**/Yohana 16:23; **9:22**/Marko 16:15; **9:23**/Marko 16:16; **9:24**/Marko 16:17; **9:27**/Wafilipi 2:12; **9:28**/Yakobo 4:3; **9:29**/1 Wakorintho 11:27.

## **Etheri**

**Etheri 3:14**/Mathayo 25:34; Yohana 1:12; **3:21**/1 Yohana 1:3; **4:7**/Matendo 26:18; **4:10**/Yohana 6:44; **4:12**/Yohana 12:44; Yohana 8:12; 1:4; **4:13-15**/Mathayo 11:28; Mathayo 25:34; **4:16**/Ufunuo 1:1; **4:18**/Marko 16:16,17; **4:19**/Yohana 6:44/Mathayo 25:34; **5:3**/Matendo 12:11; **5:4**/Mathayo 18:16; Yohana 6:44; **8:7-15**/Marko 6:14-29; **12:4**/Waebrania 6:19; **12:6**/Waebrania 11:1; **12:7**/Yohana 7:4; **12:8**/Waebrania 6:4; **12:10**/Waebrania 7:11; **12:11**/1 Wakorintho 12:31; **12:14**/Mathayo 3:11; **12:17**/Marko 9:1; **12:19**/Waebrania 6:19; **12:26,27**/2 Wakorintho 12:9; **12:28**/1 Wakorintho 13:13; **12:30**/Mathayo 17:20; **12:32**/Yohana 14:2,3; **12:33**/Yohana 10:17; 14:2,3; **12:35**/Mathayo 25:28-29; **12:37**/1 Wakorintho 13:1; Yohana 14:2-3; **12:38**/2 Wakorintho 5:10; **12:41**/Yohana 14:16; **13:3,4**/Ufunuo 21:2; **13:8-9**/2 Petro 3:10; 2 Wakorintho 5:17; **13:10-11**/Ufunuo 7:14; **13:12**/Mathayo 19:30.

## **Moroni**

**Moroni 2:3**/Matendo 8:15-17; 10:45; 11:15; **3:1**/Matendo 20:17; **4:3**/Luka 22:17-20; **5:1,2**/Luka 22:17-20; **6:1**/Luka 3:8; **6:4**/Waebrania 12:2; **6:6**/Luka 22:17-20; **7:1**/1 Wakorintho 13:13; **7:6**/1 Wakorintho 13:3; **7:7**/Warumi 4:3; 7:9/1 Wakorintho 13:3; **7:11**/Yakobo 3:11; **7:18**/Mathayo 7:2; **7:25**/Mathayo 4:4; **7:26**/Yohana 15:16; 16:23; Mathayo 21:22; **7:27**/Waebrania 1:3; **7:31**/Matendo 9:15; **7:34**/Matendo 2:38; **7:35**/Mathayo 24:30; Yohana 6:44; **7:43,44**/Mathayo 11:29; 1 Wakorintho 13:3; **7:45**/1 Wakorintho 13:4-7; **7:46**/1 Wako-

rintho 13:8,13; **7:47**/1 Wakorintho 13:7; Yohana 6:44; **7:48**/1 Yohana 3:2,3; **8:8**/Marko 2:17; **8:12**/Matendo 2:38; Mathayo 18:3; **8:14**/Matendo 8:23; 1 Wakorintho 13:13; **8:16**/1 Yohana 4:18; Matendo 13:10; **8:25**/Matendo 2:38; **9:6**/Matendo 13:10; **9:16**/Marko 8:2-3; **10:8-17**/1 Wakorintho 12:4-11; **10:19**/Waebrania 13:8; **10:26**/Yohana 8:24; **10:32**/Tito 2:12; Mathayo 22:37; 2 Wakorintho 12:9; Wakolosai 1:28; **10:33**/Mathayo 26:28; 2 Petro 3:14.

# Maswali

## Kuhusu

### Mafundisho na Maagano

**Mafundisho na Maagano (*M & M*)** inadaiwa kuwa hiki ni kitabu kingine kilichovuviwa na Mungu kuwa nyongeza juu ya Biblia. Ikiwa *M & M* kimetoka kwa Mungu, basi hatuna budi kukikubali. Hata hivyo, ikiwa hakikutokana na Mungu, basi hatuna budi kukikataa. Tunapaswa kuwa kama Waberoya na kuchunguza ikiwa madai haya ni ya kweli au uongo (Matendo 17:10-12). Nimekisoma mara kadhaa nikapata maswali mengi ya kuwauliza watakatifu hawa wa siku za mwisho. Ni matumaini yanangu kwamba ndugu zangu katika Bwana watayatumia maswali haya kama nyenzo ya kuwasaidia katika kuwasaidia watakatifu wa siku za mwisho kuiona nuru ya kweli ya neno la Mungu (Yohana 8:31-32).

#### **Mafundisho: Unabii wa Malaki**

**(1) Kwa nini malaika Moroni anasema katika *M & M 2* kwamba unabii wa Malaki 4:5,6, ambao ulitolewa kwa Joseph Smith mnamo Septemba 21, 1823 haujatimia bado wakati, kiukweli, umetimizwa na Yohana Mbatizaji?**

**Kwanza**, katika Mathyo 11:1-15, Yesu aliweka wazi kwamba Malaki alitabiri kuhusu Yohana Mbatizaji aliyekuja katika roho ya Eliya.

**Pili**, katika Mathayo 17:1-13, Yesu anawaambia wanafunzi wake kwamba “Eliya” alikwisha kuja.

**Tatu**, katika Luka 1:13-17, malaika aliyemtokea Zakaria, baba mtarajiwa wa Yohana Mbatizaji, alimwambia kwamba mtoto “*atatangulia mbele zake katika roho ya Eliya , na nguvu zake, ili kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na kuwatilia waasi akili za wenye haki, na kumwekea Bwa-*

***na tayari watu waliotengenezwa.”***

Wajumbe na ujumbe wao unaodai kutoka kwa Mungu, ni lazima ukubariane na wajumbe wengine na ujumbe wao wanaotambulika kutoka kwa Mungu (Kumb. 13:1-5; 18:15-22).

Lakini mjumbe huyu, Moroni, ambaye alimtembelea Joseph Smith, Jr, akukubaliana na ujumbe wa wajumbe wengine uliothibitishwa na Mungu, hapa namzungumzia, Yesu, Mathayo, Gabriel, na Luka (Mathayo 11:1-14; 17:10-13; Luka 1:13-17).

Hivyo, mjumbe, Moroni, aliyemtembelea Joseph Smith, Jr hakutoka kwa Mungu (imetoholewa kutoka Free 21).

### **Mafundisho: Kifungu kilichopotea**

*Katika M & M 3, maudhui ya kihistoria yanasema: “Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii, huko Harmony, Pennsylvania, Julai 1828, kuhusiana na upotevu wa kurasa 116 za muswada ulio tafsiriwa kutoka sehemu ya kwanza ya Kitabu cha Mormoni, ambacho kiliitwa kitabu cha Lehi. Nabii huku akisita aliruhusu kurasa hizi kutoka mikononi mwake na kwenda katika mikono ya Martin Harris, ambaye alitumika kwa kipindi kifupi kama mwandishi katika tafsiri ya Kitabu cha Mormoni. Ufunuo huu ulitolewa kupitia Urimu na Thumimu.”*

Somo hili la muswada ulilopotea litaletwa tena katika *M & M* 10. Angalia pingamizi la kiungu alilopewa Joseph Smith katika *M & M* 10:31-33 kwamba asitafsiri tena kilichokwisha potea: **“Kwani, tazama, hawatatimiza njama zao hizo za uovu katika kudanganya dhidi ya maneno yale. Kwani, tazama, kama wewe utayatoa tena maneno yale yale watasema kwamba umedanganya na ya kwamba unajidai kuwa unatafsiri kumbe umejichanganya mwenyewe. Na, tazama, wao watayachapisha haya, na Shetani ataishupaza mioyo ya watu kwa kuwachochea wakukasirikie wewe, kiasi kwamba hawatayaamini maneno yangu. Na hivyo ndivyo**



**Shetani awazavyo ili kuushinda ushuhuda wako katika kizazi hiki, kwamba kazi hii isije katika kizazi hiki.”**

Kinachofurahisha hapa ni kwamba, kuna kisa cha tukio katika historia ya Biblia ambapo neno la Mungu liliharibiwa. Katika Yeremia 36:20-32, kuna gombo alililopewa mfalme, hakupenda ujumbe wake, akakikata na kisu na kukitupa katika moto. Je, Mungu alishindwa kuyaandika upya maneno yake? Hapana! Soma hapo: “... *Ndipo neno la Bwana likamjia Yeremia, hapo mfalme alipokuwa amekwisha kuliteketeza gombo lile, na maneno yale aliyoyaandika Baruku, yaliyotoka katika kinywa cha Yeremia, kusema, Haya! Twaa wewe gombo lingine, ukaandike ndani yake maneno yote ya kwanza, yaliyokuwa katika gombo la kwanza, ambalo Yehoyakimu, mfalme wa Yuda, ameliteketeza. Na katika habari za Yehoyakimu, mfalme wa Yuda, utasema, Bwana asema hivi, Umeliteketeza gombo hili, ukisema, Mbona umeandika ndani yake, ukisema, Bila shaka mfalme wa Babeli atakuja, na kuiharibu nchi hii, na kukomesha mwanadamu na mnyama pia ndani yake? Basi, Bwana aseme hivi, katika habari za Yehoyakimu, mfalme wa Yuda; Hatakuwa na mtu wa kukaa katika kiti cha enzi cha Daudi; na mzoga wake utatupwa nje wakati wa mchana upigwe kwa hari, na wakati wa usiku upigwe kwa baridi. Nami nitamwadhibu yeye, na wazao wake, na watumishi wake, kwa sababu ya uovu wao, nami nitaleta juu yao, na juu ya wenyeji wa Yerusalemu, na juu ya watu wa Yuda, mabaya yote niliyoyatamka juu yao, lakini hawakukubali kusikiliza. Ndipo Yeremia akatwaa gombo lingine, akampa Baruku, mwanishi, mwana wa Neria, naye akayaandika maneno yote yaliyotoka katika kinywa cha Yeremia, ya kitabu kile alichokiteketeza Yehoyakimu, mfalme wa Yuda, katika moto; tena maneno mengi zaidi kama yale yakatiwa ndani yake.”*

Ingawa Yehoyakimu alichukuwa gombo na kulitupa moto-

ni, neno liliandikwa upya na Yeremia, akiwa nabii wa kweli wa Mungu, alikuwa na uwezo wa kuliandika upya. Kwa kuwa mungu wa watakatifu wa siku za mwisho anadai kuwa yeye ndiye Mungu wa Biblia, bila shaka yeye na Smith wasingekuwa na shida ya aina yoyote kutafsiri upya maneno hayo.

**(2) Kwa nini mungu wa watakatifu wa siku za mwisho hakumruhusu Smith kutafsiri upya muswada uliopotea kama alikuwa na uwezo wote wa kufanya hivyo katika siku za Yeremia?**

### **Mafundisho: Yohana Mtume**

Muktadha wa kihistoria unatolewa katika *M & M 7* kama ifuatavyo: *“Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii na Oliver Cowdery, huko Harmony, Pennsylvania, Aprili 1829, wakati walipoulizia kupitia Urimu na Thumimu kama ikiwa Yohana, mwanafunzi kipenzi, alikuwa bado yu hai au amekufa. Ufunuo huu ni tafsiri ya simulizi ya kumbukumbu iliyoandikwa na Yohana kwenye karatasi ya ngozi na kufichwa na yeye mwenyewe.”*

*M & M 7:3* inasema: **“Na Bwana akaniambia: Amini, amini, ninakuambia, kwa sababu wewe umetaka hili na wewe utaishi mpaka nitakapokuja katika utukufu wangu, na utatoa unabii kwa mataifa, makabila, lugha na watu.”**

Ebu ona kwamba katika *M & M 7* matarajio ya Yohana ni kuendelea kuishi kwa ajili ya Bwana ili kwamba apate kuzidi kuitimiliza huduma yake. Kweli, Yesu anasema kwamba Yohana ataendelea kuishi mpaka kurudi kwake. Zingatia jinsi hii inayodhaniwa kuwa karatasi ya ngozi kutoka kwa Yohana inavyogusia maelezo ya kihistoria ya Yohana 21. Ona jinsi kifungu katika Yohana 21 kinachogusia hitimisho tofauti na lile la *M & M 7* kwamba Yohana angekufa kimwili.

Morris anasema: “Yohana anaendelea kukabiliana na kosa lililojitokeza. Taarifa ilisambaa miongoni mwa ndugu,

kwamba mwanafunzi huyu asingekufa. Kwamba Yohana angeishi hadi kurudi kwake Yesu mara ya pili. Mtu angeweza kuona jinsi tafsiri hiyo ilivyojitokeza. Lakini Yohana anawataka wasomaji wake kujua wazi kuwa ilikuwa ni tafsiri tu. Sivyo ndivyo Yesu alivyosema. Hakusema kwamba, 'Yohana hatakufa.' Aliuliza tu kwamba ilimhusu nini Petro ikiwa huyo (Yohana) angebaki hai hadi kurudi kwa Kristo. Yohana anatutaka tuwe wazi kuhusu yale aliyoyasema Yesu na yale ambayo akuyasema." (Morris 878).

Moja kati ya mafundisho makuu ya watakatifu wa siku za mwisho ni fundisho la ukuhani. Ni muhimu sana kuelewa fundisho hili.

Kulingana na tovuti rasmi ya Watakatifu wa Siku za Mwisho: "Kwa mujibu wa tovuti inayotambulika ya watakatifu wa siku za mwisho, inasema: "kuna tofauti gani kati ya ukuhani na funguo za ukuhani? Ukuhani ni nguvu au mamlaka ya Mungu. Funguo za ukuhani ni haki ya kuitumia nguvu au mamlaka ya Mungu kwa njia zilizo sahihi."

"Nani anashikilia funguo za ukuhani?"

Majibu ya tovuti ni: "Yesu Kristo amekuwa ndiye mwenye mamlaka juu ya funguo zote za ukuhani. Alipowaita mitume wake kumi na wawili wa kwanza, Yesu aliwapa wote ukuhani (angalia Yohana 15:16). Kabla hajasulibiwa, Kristo aliwapa Petro, Yakobo, na Yohana funguo za ukuhani. Hili lilifanyika katika Mlima alipogeuka sura yake na kung'aa. (Angalia mafundisho ya Nabii Joseph Smith, Sel. Joseph Fielding Smith [1976], 158; Mathayo 17:1-9). Hata hivyo, katika karne zilizofuata mitume walipokufa, funguo hizi zilipotea; na kabla wanadamu hawajachukua tena ukuhani, ilitakiwa funguo hizi zirudishwe. Kwa sababu hii Bwana alimtuma Petro, Yakobo, na Yohana kwa Nabii Joseph Smith kurudisha ukuhani wa Melkizedeki na funguo za ukuhani huo (angalia M & M 27: 12-13).

Funguo hizi takatifu zimekabidhiwa Mitume wote na manabii wa Kanisa na zimetunzwa na manabii na Mitume wa Kanisa leo.”\*

Kwa mujibu wa tovuti, watu wote wanaopewa funguo za ukuhani wa watakatifu wa siku za mwisho ni watu walio na haki ya kutumia nguvu/mamlaka ya Mungu katika njia zilizo sahihi. Petro, Yakobo, na Yohana walikabidhiwa funguo hizo za ukuhani wa watakatifu wa siku za mwisho na Yesu Kristo ambao ulidaiwa na Joseph Smith. Hivyo, walikuwa na haki ya kutumia nguvu/mamlaka katika njia zilizo sahihi.

Ikiwa watu wote walioruhusiwa waliokabidhiwa funguo za ukuhani wa watakatifu wa siku za mwisho walikufa, basi funguo za ukuhani wa watakatifu wa siku za mwisho zimepotea. Mitume ambao ndio watu walioruhusiwa na kukabidhiwa funguo za ukuhani huo walikufa kama inavyodaiwa na watakatifu wa siku za mwisho. kwa maana hiyo funguo za ukuhani wa watakatifu wa siku za mwisho zilipotea.

Hata hivyo, ikiwa baadhi ya watu walioruhusiwa waliokabidhiwa funguo za ukuhani wa watakatifu wa siku za mwisho hawakufa, basi funguo za ukuhani wa watakatifu wa siku za mwisho hazikupotea. Mtume Yohana ambaye alikuwa miongoni mwa watu walioruhusiwa na kukabidhiwa funguo za ukuhani HAKUFA, jambo linalodaiwa na *M & M 7*. Kwa maana hiyo funguo za ukuhani wa watakatifu wa siku za mwisho hazikupotea.

Hatimaye, kishindo chenye matokeo mabaya dhidi ya msingi wa kanisa la watakatifu wa siku za mwisho ni: Ikiwa funguo za ukuhani wa watakatifu wa siku za mwisho hazikupotea, [kwa sababu Yohana hakufa (*M & M 7*)]; basi hakukuwa na sababu ya Joseph Smith kuwa chombo cha kutumiwa kuleta urejesho wa Injili ya kweli na yote yanayoambatana nayo.

**(3) Kwa nini Joseph Smith alihitajika ikiwa Yohana Mbatizaji alikuwa bado hai ambaye ndiye aliyekuwa na**

**kibali cha kuwa na funguo za ukuhani? Kungekuwaje na upotofu kama watu wote walioruhusiwa kuwa na funguo za ukuhani hawakuwa wamekufa (kama Yohana)?**

**Mafundisho: Ukuhani wa Haruni**

Hapa tuna muktadha mwingine wa kihistoria wa “ufunuo” mwingine (*M & M* 13) ambao ulitolewa: “*Dondoo kutoka katika historia ya Joseph Smith inayoeleza kutawazwa kwa Nabii na Oliver Cowdery kwenye Ukuhani wa Haruni jirani na Harmony, Pennsylvania, 15 Mei 1829. Kutawazwa huko kulifanywa kwa mikono ya malaika ambaye alijitambulisha kama Yohana, yule yule ambaye anaitwa Yohana Mbatizaji katika Agano Jipya. Malaika alieleza kwamba yeye alikuwa akiyafanya haya chini ya maelekezo ya Petro, Yakobo na Yohana, Mitume wa kale walioshikilia funguo za ukuhani mkuu, ambao uliitwa Ukuhani wa Melkizedeki. Ahadi ilitolewa kwa Joseph na Oliver kwamba katika wakati upasao ukuhuni huu mkuu utatunukiwa kwao. (Ona sehemu ya 27:7–8, 12. Funguo na uwezo wa Ukuhani wa Haruni zinatolewa).”*

*M & M* 13:1 inasema: “**Juu yenu ninyi watumishi wenzangu, katika jina la Masiya ninawatunukia Ukuhani wa Haruni, ambao hushikilia funguo za huduma za malaika, na za injili ya toba, na za ubatizo kwa uzamisho kwa ajili ya ondoleo la dhambi; na hizi kamwe hazitaondolewa tena kutoka duniani, mpaka wana wa Lawi watakapotoa tena matoleo kwa Bwana katika haki.”**

Katika Biblia, ukuhani wa Haruni, waligawanyika katika makundi matatu, yote yakiwa ni kutoka kabila la Lawi: (1) Kuhani mkuu (ambayo ndiyo ofisi ya juu kabisa; aliwawakilisha Waisraeli mbele za Mungu; aliingia Patakatifu pa Patakatifu mara moja tu kila mwaka katika siku ya upatanisho – Lawi 16); (2) Makuhani (ambao walitakiwa kutoka katika wana wa Haruni; walihudumu katika dhabihu ya madhabahu – Law. 1-7);

na (3) Walawi walioshughulika na huduma za hema (Hesabu 3:12, 13, 41; 8:14-17; Kumb. 15:19). Makuhani wote walikuwa Walawi, lakini si Walawi wote walikuwa ni makuhani.

Ikiwa ukuhani wa Haruni ulirejeshwa katika huduma ya Yohana Mbatizaji, basi ukuhani wa Haruni unahitaji masharti maalum A, B, C n.k.

**Moja ya masharti muhimu ingekuwa kwamba kila kuhani aliatakiwa kuwa Mwisraeli mzawa wa kabila la Lawi na atokane na uzao wa Haruni (Kutoka 29:9, 29, 30; Hesabu 3:5-13).**

Kutoka 29:9 inasema: “*Nawe uwakaze mishipi, Haruni na wanawe, na kuwavika kofia; nao watakuwa na huo ukuhani kwa amri ya milele; nawe utawaweka Haruni na wanawe kwa kazi takatifu.*”

Kutoka 29:29,30 inasema: “*Na hayo mavazi matakatifu ya Haruni yatakuwa ya wanawe baada yake, wayavae watakapotiwa mafuta, na watakapowekwa kwa kazi takatifu. Huyu mwanawe atakayekuwa kuhani badala yake atayavaa muda wa siku saba, hapo atakapoingia ndani ya hiyo hema ya kukutania, ili atumike ndani ya mahali patakatifu.*”

Hesabu 3:5-13 inasema: “*Kisha Bwana akanena na Musa, na kumwambia, Ilete karibu kabila ya Lawi, ukawaweke mbele ya Haruni kuhani, ili wapate kumtumikia. Nao wataulinda ulinzi wake, na ulinzi wa mkutano wote mbele ya hema ya kukutania, ili watumike utumishi wa maskani. Nao watavitunza vyombo vyote vya hema ya kukutania, na kulinda ulinzi wa wana wa Israeli, ili watumike utumishi wa maskani. Nawe utawapa Haruni na wanawe hao Walawi wawe nao; amepewa watu hao kabisa kwa ajili ya wana wa Israeli. Nawe utawaweka Haruni na wanawe, nao wataushika ukuhani wao, na mgeni atakayekaribia atauawa. Kisha Bwana akanena na Musa, na kumwambia, Mimi, tazama, nimewatwaa Walawi na kuwatoa kati ya wana wa*

***Israeli badala ya wazaliwa wa kwanza wote wafunguao tumbo katika wana wa Israeli; na hao Walawi watakuwa wangu; kwa kuwa hao wazaliwa wa kwanza wote ni wangu; katika siku ile niliyowapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri nikajiweka wakfu wazaliwa wa kwanza wote wa Israeli, wa wanadamu na wa wanyama; watakuwa wangu; mimi ndimi Bwana.***”

Kama unavyoweza kuona, haiwezekani kutimiza sharti hili la kutokea katika uzao wa Haruni moja kwa moja ili uweze kurudisha ukuhani wa Walawi. Mungu aliruhusu ukuhani wa Haruni kwa Haruni mwenyewe na wanawe. Ukimya wa Mungu katika Maandiko unakataza ukoo mwingine wowote kuhudumu katika ukuhani wa Lawi (Waeberenia 7:14; 2 Nya-kati 26:16-21).

Hata hivyo, Smith alikosa sifa kabisa za ukuhani wa Lawi kwa mujibu wa “nabii” Brigham Young.

Katika moja ya mahubiri yake, Young alieleza: “Chukua familia yenye watoto kumi, kwa mfano, na unaweza kugundua kuwa tisa katia yao ni asili ya Mataifa kabisa, na mwana au binti mmoja katika familia hiyo akiwa ni wa damu safi ya Efraim. Ilikuwa katika mishipa ya baba au mama, ikazalishwa katika mishipa ya huyo mwana au binti, huku wengine wote waliosalia wakiwa na damu ya Mataifa. Unaweza kufikiri hii ni ajabu lakini ni kweli. Tulikuwa tunafuatilia nyumba ya Israeli, hatujali kwamba hapo kwanza walitokea mashariki, kaskazini, magharibi, au kusini; kutoka Uchina, Urusi, Uingereza, California, Amerika ya Kaskazini au Kusini, wala eneo lingine lolote; na ni kijana yule yule ambaye baba yetu Yakobo alimweka mikono, kwamba ndiye atakayeiokea nyumba ya Israeli. Kitabu cha Mormoni kilikuja kwa Efraim, kwa sababu Joseph Smith alikuwa Mwefraim kamili, na kitabu cha Mormoni kilifunuliwa kwake, na alipokuwa hai alikifanya kuwa ndio biashara yake kuwatafuta wale walioi-

amini injili.” (Young, “Preaching and Testimony,” [Kuhubiri na Ushuhuda], 268-269).

Tunajua kutoka katika Biblia kwamba Yusufu, mwana wa Yakobo alikuwa na wana wawili walioitwa Manasse na Efraimu (Mwanzo 41:50-52). Ni katika kitabu cha Mormoni ndipo tunapokuja kugundua kuwa Smith alitokana na “matunda ya viuno” vya Yusufu katika Misri (2 Nefi 3:1-16), bila shaka kutoka uzao wa Efraimu kulingana na Brigham Young. Hata hivyo, isingewezekana kwake kupata sifa za ukuhani wa Lawi kwa namna yoyote bila kumkosea Mungu!

Katika *M & M* 107:13-16: **“Ukuhani wa pili unaitwa Ukuhani wa Haruni, kwa sababu ulitolewa kwa Haruni na uzao wake, katika vizazi vyao vyote. Kwa nini unaitwa ukuhani mdogo ni kwa sababu ni kiambatanisho kwa ule mkubwa, au Ukuhani wa Melkizedeki, na unao uwezo wa kuhudumu katika ibada za nje. Uaskofu ni urais wa ukuhani huu, na unashikilia funguo, au mamlaka hayo. Hakuna mtu aliye na haki kisheria kwenye ofisi hii, kushikilia funguo za ukuhani huu, isipokuwa ni mzaliwa halisi wa ukoo wa Haruni.”**

Hili linashangaza kwa sababu hili lingeondoa kila mtu maana hakuna ambaye angeweza kupata kizazi chake kurudi nyuma mpaka kwa Haruni.

**(4) Hivi kitabu cha Mormoni kinaelewa kwa dhati kifungu kinamaanisha nini kinapotumia neno “ofisi”?**

Watu wote walioruhusiwa walio na sifa za kuwa wa ukuhani wa Haruni ni watu wanaopaswa kutokana na kabila la Lawi ambalo linakubalika pia na *M & M* 107:16. Lakini Joseph Smith hakutokana na kabila la Lawi. Kulingana na 2 Nefi 3:1-16 na Hotuba ya Young, inaonekana alitokana na ukoo wa Efraimu. Hivyo, Joseph Smith hana sifa za kuwa na ukuhani wa Haruni.

**Sharti muhimu la pili lingekuwa kwamba ilitakiwa makuhani kutoa dhabihu ya dhambi ya wanyama (Wae-**



**brania 10:1-4; Kutoka 29:38-44; Lawi 1-7).**

Waebrania 10:1-4 inaeleza: *“Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wo wote kuwakamilisha wakaribiao. Kama ndivyo, je! Dhabihu hazingekoma kutolewa; kwa maana waabuduo, waki-isha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi? Lakini katika dhabihu hizo liko kumbukumbu la dhambi kila mwaka. Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi.”*

**Sharti muhimu la tatu lingekuwa kwamba makuhani walipaswa kuwekwa wakfu sawa sawa na masharti ya Bwana (Kutoka 29:1-29).**

Hata hivyo, watakatifu wa siku za mwisho hawashiki masharti haya ya ukuhani wa Haruni.

Kama ukuhanu wa Haruni ulirudishwa, basi masharti muhimu yalitimizwa katika kurejesha ukuhani wa Haruni. Hata hivyo, masharti muhimu [uzao sahihi, majukumu ya kutoa wanyama katika madhabahu, na kuwekwa wakfu] yaliyohitajika chini ya ukuhani wa Haruni hayakutimizwa. Hivyo, ukuhani wa Haruni haukurejeshwa.

Kama mwandishi wa Waebrania 7:11-14 anavyoeleza: *“Basi, kama ukamilifu ulikuwapo kwa ukuhani wa Lawi; (maana watu wale waliipata sheria kwa huo); kulikuwa na haja gani tena ya kuhani mwingine ainuke, kwa mfano wa Melkizedeki, wala asihesabiwe kwa mfano wa Haruni? Maana ukuhani ule ukibadilika, hapana budi sheria nayo ibadilike. Maana yeye aliyenenwa hayo alikuwa mshirika wa kabila nyingine, ambayo hapana mtu wa kabila hiyo aliyeihudumia madhabahu. Maana ni dhahiri kwamba Bwana wetu alitoka katika Yuda, kabila ambayo Musa hakunena neno lo lote juu yake katika mambo ya ukuhani.”*

Waefeso 2:14-16 inafundisha wazi wazi kwamba sheria ya

Musa iliondolewa, jambo ambalo lilitakiwa kuhusisha pia na ukuhani wa Haruni. Biblia inaeleza: ***“Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga. Naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake; ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake; akafanya amani. Akawapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuufisha ule uadui kwa huo msalaba.”***

Kwa kuja kwake Yesu katika ulimwengu huu kujitoa kama dhabihu moja ya milele ili kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi za mwanadamu, Yesu alipaswa kuwa ameiondoa sheria ile ya kale kwa kuigongomea katika msalaba (Wakolosai 2:14-17) na kuleta Agano ambalo dhambi za mwanadamu zingesamehewa kabisa.

Waebrania 10:5-10 inasema: ***“Kwa hiyo ajapo ulimwenguni, asema, Dhabihu na toleo hukutaka, Lakini mwili uliniwekea tayari; Sadaka za kuteketezwa na sadaka za dhambi hukupendezwa nazo; Ndipo niliposema, Tazama, nimekuja (katika gombo la chuo nimeandikiwa) Niyafanye mapenzi yako, Mungu. Hapo juu asemapo, Dhabihu na matoleo na sadaka za kuteketezwa na hizo za dhambi hukuzitaka, wala hukupendezwa nazo (zitolewazo kama ilivyoamuru torati), ndipo aliposema, Tazama, nimekuja niyafanye mapenzi yako. Aondoa la kwanza, ili kusudi alisimamisha la pili. Katika mapenzi hayo mmepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu.”***

Yesu alisimamisha Agano lililo bora. Si kwamba alisimamisha Agano lililo bara tu, bali lilikuwa Agano la milele (Waebrania 13:20), lililothibitishwa kwa ishara, miujiza, na maajabu (Waebrania 2:3-4). Agano hili lilisimamishwa katika mwaka wa 30 (au 33) B.K., baada ya Yesu kufa pale msalabani ambapo mapenzi yake yalianza kufanya kazi (Waebrania 9:15-17).

**(5) Kwa nini ukuhani wa Haruni ulihitaji kurejeshwa ikiwa uliondolewa na Yesu na kubadilishwa na Agano bora zaidi?**

**Mafundisho: Ofisi ya Utume**

Katika *M & M* 21:1,10, inasema: “*Tazama, patakuwa na kumbumbu itakayotunzwa miongoni mwenu [Joseph Smith]; ambamo ndani yake utaitwa mwonaji, mfasiri, nabii, mtume wa Yesu Kristo, mzee wa kanisa kwa njia ya mapenzi ya Mungu Baba, na neema ya Bwana wenu Yesu Kristo, ... Kwa hiyo nimeona ni muhimu kwa yeye kutawazwa na wewe, Oliver Cowdery mtume wangu.*”

Madhehebu ya watakatifu wa siku za mwisho yalitaka kurejeshwa ofisi ya utume, lakini Agano Jipya linafundisha kwamba ilikuwa ofisi ya muda tu katika kanisa (kama itakavyoonekana kutoka katika masharti muhimu). Ili madhehebu ya watakatifu wa siku za mwisho yarudishe ofisi ya utume, basi lazima zirejeshwe hali zinazohitajika ambazo zimewekwa na Agano Jipya lenyewe.

Ikiwa ofisi ya kitume ilirejeshwa kupitia Watakatifu wa Siku za Mwisho, basi ofisi ya kitume inahitaji masharti ya lazima A, B, C, nk.

**Sharti la kwanza la lazima lilikuwa kwamba mitume wawe mashahidi waliomwona Kristo aliyefufuka (1 Yohana 1:1-4; Mdo. 1:21,22; 22:14,15).**

**(6) Je, “mitume” wa sasa wa Watakatifu wa siku za mwisho wamemwona Kristo aliyefufuliwa?**

**Sharti la pili la lazima lilikuwa kwamba mitume waliitwa na kuchaguliwa na Kristo mwenyewe (Luka 6:13; Matendo 1:2; 9:6; 24:16-18).**

**Sharti la tatu la lazima lilikuwa kwamba mitume walipewa Injili kwa ufunuo wa papo kwa hapo kwa njia ya Roho Mtakatifu (Yohana 14:26; 16:7-13; Wagalatia 1:12).**

**Sharti la nne la lazima lilikuwa kwamba mitume walikuwa na agizo lenye mamlaka kwa ulimwengu wote (Mathayo**

**28:18-20; 1 Wakorintho 4:17; Warumi 1:14-16).**

**Sharti la tano muhimu lilikuwa kwamba mitume walikuwa na uwezo wa kufanya miujiza ili kushuhudia utume wao na kuthibitisha ukweli wa mafundisho yao (Matendo 2:43; 2 Wakorintho 12:12; Waebrania 2:1-4).**

**Sharti la sita la lazima lilikuwa kwamba mitume walikuwa na uwezo wa kugawa vipawa vya kufanya miujiza kwa wale waliowawekea mikono juu yao (Matendo 8:14-18; 19:1-6; 2 Timotheo 1:6; Warumi 1:11).**

**Sharti la saba la lazima ni kwamba mitume walilijenga kanisa juu ya msingi wa Yesu Kristo (1 Wakorintho 3:11). Tazama pia Waefeso 2:20; 1 Wakorintho 12:28; Ufunuo 21:14).\*\***

**(7) Kwa nini mtu yeyote angetaka kubomoa msingi ili kuweka “mitume wapya” (yaani msingi mpya)?**

Baadhi ya “mitume” hawa wa Watakatifu wa Siku za Mwisho wanaweza kusema kwamba wanatimiza masharti muhimu kama vile kushuhudia kwamba wamemwona Kristo aliyefufuka, n.k., lakini kuna angalau masharti mawili yanayoonesha kuwa wao ni mitume wa uongo: yaani hawawezi kufanya miujiza ya kweli wala kutoa karama za miujiza kwa wengine. Kwa hiyo, ni waongo (Ufunuo 2:2)!

Moja ya pingamizi ambalo kanisa la Watakatifu wa Siku za Mwisho hutumia wakati wengine wanaposema kuwa “zama za miujiza” zimepita (1 Wakorintho 13:1-13; Waefeso 4:7-16; Yuda 3), wanawafananisha na wale Mafarisayo walioomba muujiza kutoka kwa Yesu. Pingamizi hili sasa litajibiwa.

Katika Kumbukumbu la Torati 13:1-5, majaribio kadhaa yalitolewa ili kubaini kama mtu fulani alikuwa nabii wa kweli au nabii wa uongo.

Jaribio la kwanza lilikuwa kufanya muujiza wa kweli. Jaribio la pili lilikuwa kwamba nabii asingeweza kupinga ufunuo uliopita ambao ulikuwa umetolewa.

Kumbukumbu la Torati 13:1-5 inasema: “***Kukizuka katikati***

*yako nabii, au mwotaji wa ndoto, akikutolea ishara au aja-bu, ikatukia hiyo ishara au hiyo ajabu aliyokuambia akise-ma, Na tuifuata miungu mingine usiyojua, tuitumikie hiyo; wewe usiyasikize maneno ya nabii yule, au yule mwotaji wa ndoto, kwa kuwa Bwana, Mungu wenu, yuawajaribu, apa-te kujua kwamba mwampenda Bwana, Mungu wenu, kwa mioyo yenu yote na roho zenu zote. Tembeeni kwa kumfua-ta Bwana, Mungu wenu; mcheni na kushika maagizo yake na kuisikia sauti yake, nanyi mtumikieni na kushikamana naye. Na yule nabii, au yule mwotaji wa ndoto, na auawe, kwa kuwa amesema yaliyopotoka juu ya Bwana, Mungu wenu, aliyewatoa katika nchi ya Misri, akakukombo-a katika nyumba ya utumwa, apate yule mtu kukupotoa katika njia aliyokuamuru Bwana, Mungu wako, uiendee. Ndivyo utakavyoondoa uovu utoke katikati yako.”*

Kwa mfano, katika 1 Wafalme 18, Eliya alidhihirisha kuwa yeye ni nabii wa kweli wa Mungu na si manabii wa Baali. Eliya alishinda jaribu la kwanza ambalo Mungu wa kweli wa hali ya hewa (Mungu wa Israeli) alifanya muujiza kupitia kwake. Jaribio la pili pia lilipitishwa na Eliya kwa sababu alikuwa akifundisha mambo yaliyokubaliana na ufunuo uliopita - kuna Mungu mmoja ambaye ni YHWH (Kumbukumbu la Torati 6:6-8). Manabii wa Baali walikuwa manabii wa uongo.

Katika Mathayo 12:38-39, Biblia inasema: *“Hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako. Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta [kuendelea kuomba – SF] ishara, wala hakitapewa ishara, ila ishara ya nabii Yona.”*

Hili halikuwa ombi moja tu, bali maombi mengi yaliyotolewa na Mafarisayo ili Yesu afanye muujiza ingawa walikuwa wameona ishara ya kweli kutoka kwa Mungu moja baada ya nyingine.

Katika Mathayo 16:1-4: *“Wakamjia Mafarisayo na Masadukayo, wakamjaribu, wakamwomba awaonyeshe ishara itokayo*

*mbinguni. Akajibu, akawaambia, [Kukiwa jioni, mwasema, Kutakuwa na kianga; kwa maana mbingu ni nyekundu. Na asubuhi, mwasema, Leo kutakuwa na dhoruba; kwa maana mbingu ni nyekundu, tena kumetanda. Enyi wanafiki, mwajua kuutambua uso wa mbingu; lakini, je! Ishara za zamani hizi hamwezi kuzitambua? Kizazi kibaya na cha zinaa chataka ishara; wala hakitapewa ishara, isipokuwa ishara ya Yona. Akawaa-cha, akaenda zake.”* Mara nyingine tena, tunaona neno “kutaka” linatumika katika maana ya tendo linaloendelea.

Katika 1 Korintho 1:22-23, inaelezwa: “*Kwa sababu Wayahudi wanataka ishara, na Wayunani wanatafuta hekima; bali sisi tunamhubiri Kristo, aliyesulibiwa; kwa Wayahudi ni kikwazo, na kwa Wayunani ni upuzi.*” Neno “ombi” linatumika katika maana ya aina ya kitenndo kinachoendelea. Wayahudi waliendelea kuomba ishara!

Haikuwa kosa kuomba kuona muujiza mara moja. Kulikuwa na mamlaka kutoka katika Kumbukumbu la Torati 13:1-5 kuomba ishara kutoka kwa mtu aliyedai kuwa yeye ni nabii. Kosa ni kuomba kurudiwarudiwa kwa muujiza wakati muujiza wa kweli ulikuwa tayari umefanywa mbele ya macho yao. Kwa hiyo ninaomba kwa unyoofu kwamba muujiza wa kweli ufanyike kama ulivyofanyika katika karne ya kwanza B.K.

Mshirika wa kundi la Watakatifu wa siku za Mwisho, ikiwa unasoma hili, muombe mmoja wa wale mitume 52 wa Watakatifu wa Siku za Mwisho afanye muujiza leo. Akikataa au wakikataa, basi waulize: “Kwa nini husifanye muujiza?”

Jaribio la pili ambalo ni lazima lipitishwe ni kuwauliza mitume wa Watakatifu wa Siku za Mwisho: “Kwa nini hamkubaliani na ufunuo uliopita, ambao ni Biblia?”

Ikiwa ofisi ya kitume ilirejeshwa, basi masharti ya lazima yaliyohitajika ili kurejesha ofisi ya kitume yalitimizwa. Lakini baadhi ya masharti ya lazima, kama lile la mtu kuwa na uwezo wa kufanya miujiza, kuweka mikono yake juu ya mtu

mwingine ili kumpa karama za miujiza, lakini masharti hayo yanayohitajika katika ofisi ya kitume hayakutimizwa. Kwa hiyo, ofisi ya kitume haikurejeshwa.

### **Mafundisho: Adhabu ya Ufahamu wa Milele**

Katika *M & M* 19:6, inakanusha kufahamu adhabu ya milele. Hapa kuna maandishi: **“Hata hivyo, haikuandikwa kwamba hapatakuwa na mwisho wa mateso haya, bali imeandikwa mateso yasiyo na mwisho.”**

Ona anachosema msomi wa Watakatifu wa Siku za Mwisho, Casey Griffiths: “Bwana anatatua mahangaiko ya Martin kwa kueleza kwamba maneno ‘isiyo na mwisho’ na ‘milele’ kama yalivyotumiwa katika vifungu hivi ni nomino na si vivumishi. Jina la Bwana halina mwisho na ni la milele, na Anasimamia ukarabati wa wanaume na wanawake katika maisha ya baada ya kifo. Maneno haya yanaashiria umiliki wake wa adhabu ya waovu, na wala si muda wa adhabu wenyewe.”\*\*\* Hilo linapingana na Biblia (Danieli 12:2; Mathayo 25:41,46; Marko 9:10; 44-48; Yohana 5:28,29; 2 Wathesalonike 1:7-9; Ufunuo 14:9-11; 20:10).

**(8) Je, unapatanishaje hili na ufunuo uliopita - Biblia - ambayo inafundisha ufahamu wa adhabu ya milele?**

### **Mafundisho: “Kijiti cha Efraimu”**

Katika *M & M* 27:1-9, inasema: **“Sikilizeni sauti ya Yesu Kristo, Bwana wenu, Mungu wenu, na Mkombozi wenu, ambaye neno lake ni la haraka na lenye nguvu. Kwani, tazama, ninawaambia, kwamba si muhimu ni nini utakachokunywa au utakachokula wakati unapopokea sakramenti, ili mradi kwamba unafanya hayo kwa jicho likiwa kwenye utukufu wangu pekee—mkikumbuka kwa Baba mwili wangu uliotolewa kwa ajili yenu, na damu yangu iliyomwagwa kwa ondolea la dhambi zenu. Kwa hiyo, amri**

ninakupa, kwamba usinunue divai wala kinywaji kikali cha adui zako; Kwa hiyo, msipokee chochote isipokuwa kimetengenezwa upya miongoni mwenu; ndiyo, katika huu ufalme wa Baba yangu ambao utajengwa hapa duniani. Tazama, hii ni hekima kwangu; kwa hiyo, usistaa-jabie, kwani saa yaja ambayo nitakunywa matunda ya mzabibu pamoja nanyi duniani, na pamoja na Moroni, ambaye nilimtuma kwako kufunua Kitabu cha Mormoni, chenye utimilifu wa injili yangu isiyo na mwisho, ambaye nimemkabidhi funguo za kumbukumbu ya fimbo ya Efraimu; Na pia Eliya, ambaye nimemkabidhi funguo za kukamilisha urejesho wa mambo yote yaliyonenwa kwa vinywa vya manabii watakatifu tangu mwanzo wa ulimwengu, kuhusu siku za mwisho; Na pia Yohana mwana wa Zakaria, Zakaria ambaye yeye (Eliya) alimtembelea na kumpa ahadi kwamba atapata mwana, na jina lake litakuwa Yohana, na yeye atakuwa amejazwa na roho ya Eliya; Yohana ambaye nimekwisha mtuma kwenu ninyi, watumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na Oliver Cowdery, kuwatawaza ninyi katika ukuhani wa kwanza ambao mmeupokea, ili kwamba muwe mmeitwa na kutawazwa kama ilivyokuwa hata kwa Haruni. Na pia Eliya, ambaye kwake nimemkabidhi funguo za uwezo wa kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na mioyo ya watoto kwa baba, ili kwamba dunia yote isiweze kupigwa kwa laana.”

Mjadala mkuu wa kwanza ni kutambua kwamba “ufunuo” huu unasema kwa uwazi kwamba Kitabu cha Mormoni kimeunganishwa na “fimbo ya Efraimu” katika Ezekieli 37.

Ukimuuliza mtakatifu wa Siku za Mwisho swali hili: “Je, kuna ushahidi wowote kwamba Kitabu cha Mormoni kingekuja kama ufunuo wa siku za mwisho kutoka kwa Mungu ambao unashuhudia Injili?” Mojawapo ya majibu yao ya



kawaida ni Ezekieli 37:15-23.

LeGrands Richards, “mtume” wa zamani wa kanisa la Wakatoliki wa Siku za Mwisho aliandika: “Je, ahadi hii inaweza kutimizwa kwa njia rahisi na kamilifu zaidi kuliko ilivyokuwa kupitia ujio wa kitabu cha Mormoni? Mungu aliongoza tawi la nyumba ya Yusufu hadi Marekani na kuwaamuru kutunza kumbukumbu za matendo yao yote. Kisha alimwamuru nabii wake, Moroni, kuficha maandiko haya matakatifu katika kilima cha Kumora katika sehemu ya magharibi ya jimbo la New York, Marekani. Karne kadhaa baadaye alimtuma Moroni arudi kuwasilisha kumbukumbu kwa Joseph Smith na kumpa uwezo wa kutafsiri kwa kutumia maandiko hayo kwa msaada wa Urimu na Thumimu. Sasa rekodi hizi mbili zimeunganishwa pamoja, zikijumuisha utimilifu kamili wa unabii mwingine mkuu...Mpaka mtu aweze kueleza iko wapi rekodi ya Yusufu, Kitabu cha Mormoni kinasimama bila kukanushwa madai yake kuwa kitabu hicho ndicho ‘fimbo ya Yusufu’” (Richards 67-68).

Scott alitoa tafsiri ya Hugh Nibley ya Ezekieli 37: “‘Fimbo ya Yuda’ ni Biblia, kwa sababu iliandikwa na wazao wa Yuda, Wayahudi; na kwamba ‘fimbo ya Efraimu’ ni Kitabu cha Mormoni, kilichoandikwa na Wanefi ambao walitokana na Efraimu” (Scott 58).

Acha tuchunguze kwa makini Ezekieli 37:15-23.

**Kwanza**, Ezekieli alitakiwa kuchukua vile vijiti viwili na kuandika juu yake: “*Kwa Yuda, na kwa wana wa Israeli wenzake; kisha, twaa kijiti cha pili; ukaandike juu yake, Kwa Yusufu, kijiti cha Efraimu, na kwa nyumba yote ya Israeli wenzake.*” Ni hayo tu! Hakukuwa na kitu kingine chochote ambacho Ezekieli alipaswa kuandika kwenye vijiti hivi. Kitabu cha Mormoni na Biblia vina maandiko mengi zaidi ya haya!

**Pili**, Ezekieli ndiye mwandishi wa kuandika juu yao. “Mwanadamu” (inatoka karibu mara 90 katika Ezekieli)

kumrejelea Ezekieli mwenyewe. Lakini Ezekieli hakuandika Kitabu cha Mormoni!

**Tatu**, Ezekieli atachukua vijiti viwili navyo vinawakilisha mataifa mawili, si rekodi mbili. Angalia maandisko yanase-  
ma nini tena: *“Na wana wa watu wangu watakapokuambia, wakisema, Je! Hutatuonyesha maana ya mambo hayo uten-  
dayo? Waambie, Bwana MUNGU asema hivi; Tazama, ni-  
takitwaa kijiti cha Yusufu, kilicho mkononi mwa Efraimu, na kabila za Israeli wenzake, nami nitawaweka pamoja na-  
cho, yaani, pamoja na kijiti cha Yuda, na kuvifanya kuwa kijiti kimoja; navyo vitakuwa kimoja mkononi mwangu.”*

**Nne**, Ezekieli anatuonesha tafsiri yake ni: *“Navyo vijiti, am-  
bavyo uliandika juu yake, vitakuwa mkononi mwako mbele ya macho yao. Ukawaambie, Bwana MUNGU asema hivi; Taza-  
ma, nitawatwaa wana wa Israeli toka kati ya mataifa walikok-  
wenda, nami nitawakusanya pande zote, na kuwaleta katika nchi yao wenyewe; nami nitawafanya kuwa taifa moja katika nchi hiyo, juu ya milima ya Israeli; na mfalme mmoja atakuwa mfalme wao wote; wala hawatakuwa tena mataifa mawili, wala hawatagawanyikana kuwa falme mbili tena, hata milele. Wala hawatajitia uchafu tena kwa vinyago vyao, wala kwa vitu vyao vichukizavyo, wala kwa makosa yao mojawapo; lakini nitawa-  
okoa, na kuwatoa katika makao yao yote, ambayo wamefanya dhambi ndani yake, nami nitawatakasaa; basi watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao.”*

Unabii huo unahusu kabila la Efraimu (kwa kuwa lilikuwa kabila mashuhuri lililowakilisha ufalme wa Kaskazini), kwa maana baadhi yao walipaswa kurudi Yerusalemu kutoka utumwani. Pia inahusu Yuda (kwa kuwa ulikuwa ufalme mashuhuri unaowakilisha ufalme wa Kusini), ambao pia ungerudi katika nchi yao, ili kuunganishwa pamoja kuwa taifa moja. Hawakupaswa tena kugawanywa katika mataifa mawili. Kwa kuwa Yesu angekuja kuwa “mwana wa Daudi,” angetawala juu ya Israeli mpya (yaani,

watu wake wa pekee – kanisa – Warumi 9:6; 11:26; Wagalatia 6:16; Waebrania 8:8–10).

Kinachofanya mambo kuwa mabaya zaidi ni kwamba kulingana na Kitabu cha Mormoni, babu wa Lehi alikuwa Manase, si Efraimu (Alma 10:2,3)!

Ikiwa kitabu cha *M & M* kimevuviwa na Mungu, basi “kijiti cha Efraimu” katika Ezekieli 37:15-23 ni Kitabu cha Mormoni (*M & M* 27:5). Lakini “fimbo ya Efraimu” katika Ezekieli 37:15-23 sio Kitabu cha Mormoni. Kwa hiyo, *M & M* haijavuviwa na Mungu.

**(9) Kwa nini kitabu cha *M & M* kinathibitisha kwamba “kijiti cha Efraimu” katika Ezekieli 37 ni Kitabu cha Mormoni wakati, kwa kweli, kuna ushahidi wa kutosha unaotetea madai hayo?**

### **Mafundisho: “Elia” na “Eliya”**

Mzozo mkubwa wa pili, pia utaoneshwa kutoka katika kifungu hiki hiki. Tafadhali soma tena *M & M* 27:1-9.

**Kutoka katika tovuti rasmi ya Watakatifu wa Siku za Mwisho, hiki ndicho kinachosemwa kuhusu “Elias”:** “Kuna matumizi kadhaa ya neno hili katika maandiko.

(1) Eliya (neni / jina) ni muundo wa Agano Jipya (Kigiriki), (Kiebrania), kama katika Luka 4:25–26; Yakobo 5:17; na Mt. 17:1–4. Elias katika matukio haya anaweza tu kuwa nabii wa kale Eliya ambaye huduma yake imeandikwa katika 1 na 2 Wafalme. Udadisi wa neno JST Marko 9:3 haimaanishi kuwa wakati Elias anageuka sura alikuwa Yohana Mbatizaji, ila hilo liliongezeka kwa Eliya nabii, Yohana Mbatizaji alikuwepo (ona Marko 9:4).

(2) Elia pia ni cheo cha mtu ambaye ni mtangulizi; kwa mfano, Yohana Mbatizaji, kama katika JST Mt. 11:13–15; Mt. 17:10–14, na JST Yohana 1:20–28 (Nyongeza). Vifungu hivi vimefafanuliwa vya kutosha ili kuonesha kwam-

ba hapo kale Elias wawili walizungumziwa kuwa, mmoja kama mtayarishaji na mwingine mrejeshaji. Yohana alitumwa kuandaa njia kwa ajili ya Yesu, Yesu Mwenyewe akiwa Mrejeshaji aliyerudisha Injili na Ukuhani wa Melkizedeki kwa Wayahudi katika siku zake (sona Yohana 1:20–28). Katika tukio hili mahususi kunaoneshwa pia kazi za kulinganisha za Ukuhani wa Haruni na Melkizedeki.

(3) Cheo, Elia pia kimetumiwa kwa wengine wengi kwa ajili ya kazi mahususi au kazi za urejesho ambazo wanapaswa kutimiza; kwa mfano, Yohana Mdhihirishaji (M&M 77:14) na Nuhu au Gabrieli (Luka 1:11–20; M&M 27:6–7).

(4) Mtu anayeitwa Elia inaonekana aliishi katika maisha ya duniani katika siku za Ibrahimu, ambaye alikabidhi maongozi ya injili ya Ibrahimu kwa Joseph Smith na Oliver Cowdery katika Hekalu la Kirtland (Ohio) mnamo Aprili 3, 1836 (M & M 110:12). Hatuna habari mahususi kuhusu maelezo ya maisha yake duniani wala huduma yake.”\*\*\*\*

Angalia kanisa la Watakatifu wa Siku za Mwisho linaamini kutakuwa na Eliasi wawili - mmoja alikuwa mtayarishaji na mwingine ni mrejeshaji. Angalia katika fasiri yao ya tatu wanadai kwamba “Elias” ni cheo.

Katika *M & M* 27, kuna utofauti wa dhairi kati ya “Eliya” na “Elias” kwa kutumia neno “pia” ambalo ni kielezi kinachomaanisha “pamoja na.”

Yeyote aliye na ujuzi wowote wa Biblia angeelewa kwamba wasomi wa toleo la King James walitafsiri jina hilo katika Kiingereza kama “Eliya” katika Agano la Kale na “Elias” katika Agano Jipya (ambalo limethibitishwa katika makala iliyo hapo juu). KJV ilitumika katika wakati huo wa Joseph Smith. Hata hivyo, ni ujinga kabisa kwa upande wa Smith kudai kwamba kuna tofauti kati ya “Elias” na “Eliya.” Tafadhali soma mistari hii katika KJV kuhusiana na unabii wa Agano la Kale kuhusu Yohana Mbatizaji kuwa utimilifu wa kielelezo

cha “Eliya/Elias”:

(1) Malaki 3:1: *“Angalieni, namtuma mjumbe wangu, naye ataitengeneza njia mbele yangu; naye Bwana mnayemtafuta atalijilia hekalu lake ghafula; naam, yule mjumbe wa agano mnayemfurahia, angalieni, anakuja, asema Bwana wa majeshi.”*

(2) Marko 1:1-4: *“Mwanzo wa Injili ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Kama ilivyoandikwa katika nabii Isaya, Tazama, namtuma mjumbe wangu Mbele ya uso wako, Atakayeitengeneza njia yako. Sauti ya mtu aliaye nyikani, Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito yake. Yohana alitokea, akibatiza nyikani, na kuuhubiri ubatizo wa toba liletalo ondoleo la dhambi.”*

(3) Mathayo 11:10: *“Huyo ndiye aliyeandikiwa haya, Tazama, mimi namtuma mjumbe wangu Mbele ya uso wako, Atakayeitengeneza njia yako mbele yako.”*

(4) Mathayo 17:10-13: *“Wanafunzi wake wakamwuliza, wakisema, Basi kwa nini waandishi hunena ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza? Naye akajibu, akawaambia, Kweli Eliya yuaja kwanza, naye atatengeneza yote, ila nawaambia, ya kwamba Eliya amekwisha kuja, wasimtambue, lakini wakamtenda yote waliyotaka. Vivyo hivyo Mwana wa Adamu naye yuaenda kuteswa kwao. Ndipo wale wanafunzi walipofahamu ya kuwa amesema nao habari za Yohana Mbatizaji.”*

Yohana Mbatizaji alikuwa mtayarishaji/mtangulizi na mrejeshaji katika kipindi cha karne ya kwanza A.D., kabla ya Yesu kuanza huduma yake. Alikuwa mtangulizi katika maana ya kwamba hapo kale msafara wa mfalme ulipokuwa ukisafiri kando ya barabara, kungekuwa na wanaume ambao wangesafisha barabara na kuhakikisha kwamba msafara unaenda vizuri bila vizuizi vyovyote njiani. Yohana alikuwa anatayarisha njia kwa ajili ya Mfalme mkuu - Yesu. Pia alikuwa

mrejeshaji kwa sababu aliwahubiria wana wa Israeli kubadili njia zao na kurejeshwa katika uhusiano mzuri na Mungu. Alihubiri ubatizo wa toba kwa ondoleo la dhambi (Marko 1:4).

Mtu yeyote akitaka kunipinga, kosa kama hilo linafanywa tena katika *M & M* 110. Huu hapa ni muktadha wa kihistoria: “*Maono yaliyoonyeshwa kwa Joseph Smith Nabii na Oliver Cowdery katika hekalu huko Kirtland, Ohio, 3 Aprili 1836.*”

Inaeleza katika mistari ya 11-16: “**Baada ya maono haya kufungwa, mbingu zilitufungukia tena; na Musa akatokea mbele yetu, na kutukabidhi funguo za kukusanyika kwa Israeli kutoka pande nne za dunia, na kuongozwa kwa makabila kumi kutoka nchi ya kaskazini. Baada ya hili, Eliya alitokea, na kutukabidhi kipindi cha injili ya Ibrahimu, akisema kwamba kupitia sisi na uzao wetu vizazi vyote baada yetu sisi vitabarikiwa. Baada ya maono haya kufungwa, maono mengine makubwa na matukufu yakatukia juu yetu; kwani Eliya nabii, aliyechukuliwa mbinguni bila ya kuonja mauti, alisimama mbele yetu, na kusema: Tazama, wakati umetimia kikamilifu, ambao ulinenwa kwa kinywa cha Malaki—ukishuhudia kwamba yeye [Eliya] lazima atatumwa, kabla ya kuja kwa siku ile iliyo kuu na ya Bwana—Kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na ya watoto iwaelekee mababu, dunia yote isije ikapigwa kwa laana— Kwa hiyo, funguo za kipindi hiki zimekabidhiwa mikononi mwenu; na kwa hili ninyi mpate kujua kwamba siku ile iliyo kuu na ya kutisha ya Bwana i karibu, hata milangoni.**”

Kosa lile lile linafanywa tena katika *M & M* 138, ambalo lilikuwa “ufunuo” uliotolewa kwa Joseph F. Smith mnamo Oktoba 3, 1918.

*M & M* 138:44-48 inaeleza: “**Danieli, ambaye aliona na kutabiri juu ya kuanzishwa kwa ufalme wa Mungu katika siku za mwisho, ambao kamwe hautaharibiwa wala kutolewa**

kwa watu wengine; Eliya, aliyekuwa pamoja na Musa juu ya Mlima [ambapo Yesu aligeuka sura]; Na Malaki, nabii aliye-shuhudia juu ya kuja kwa Eliya— ambaye pia Moroni alim-sema kwa Nabii Joseph Smith, akisema kwamba yeye lazima atakuja kabla ya kuja kwa siku ile iliyo kuu na ya kutisha ya Bwana—pia walikuwepo pale. Nabii Eliya alikuwa apande katika mioyo ya watoto ahadi zilizotolewa kwa baba zao. Ikio-neshwa dalili ya kazi kuu itakayofanyika katika mahekalu ya Bwana katika kipindi cha utimilifu wa nyakati, kwa ajili ya ukombozi wa wafu, na kuwafunga watoto kwa wazazi wao, isije dunia yote ikapigwa kwa laana na kuharibiwa kabisa wakati wa kuja kwake.”

**(10) Kwa nini kitabu cha *M & M* kinaonekana kuchan-ganyikiwa kuhusu “Elias” na “Eliya” kuwa ni manabii wawili tofauti?**

#### **Mafundisho: Zekaria 13:6**

Katika *M & M* 45:50-53, inasema: “Na majanga yatamfu-nika mwenye kudhihaki, na mwenyedharau atakoma; na wote watazamiao uovu watakatiliwa mbali na kutupwa ka-tika moto. Na ndipo Wayahudi watanitazama mimi na kuse-ma: Je, haya majeraha katika mikono yako na katika miguu yako ni nini? Ndipo watakapojua kuwa Mimi ndimi Bwana; kwani nitawaambia: Majeraha haya ni majeraha niliyotiwa katika nyumba ya marafiki zangu. Mimi ndiye yule aliyeinu-liwa. Mimi ni Yesu ambaye alisulibiwa. Mimi ni Mwana wa Mungu. Na ndipo watakapolia kwa sababu ya uovu wao; ndi-po watakapoomboleza kwa sababu walimtesa mfalme wao.”

Kuna maelezo chini yanayosema kwamba mstari wa 52 un-arejezea Zekaria 13:6: “*Na mtu atamwambia, Je! jeraha hizi kati ya mikono yako ni nini?*’ Naye atajibu, *Ni zile nilizoje-ruhiwa katika nyumba ya Mungu rafiki zangu.*”

Mtu anahitaji kukumbushwa kuhusu muktadha wa jumla wa Zekaria. Inatumia maneno “katika siku ile” kurejelea wakati

ujao wa Kimasihi (Zekaria 2:11; 3:10; 9:16; 12:3,4,6,8,9,11; 13:1,2,4; 14:4,6,8,9,13,20,21).

Katika Zekaria 13, anatabiri juu ya kupatikana (Warumi 3:23; 1 Yohana 2:1,2) kwa uwezo wa chemchemi ambayo itatolewa kwa ajili ya utakaso wa dhambi na uchafu, ambayo ni nguvu ya damu ya Mwokozi ambayo inaweza kuwahesabia haki wenye dhambi (Warumi 5:8,9), kuwakomboa wenye dhambi (Waefeso 1:7), kupatanisha wenye dhambi na Mungu (Warumi 5:10), na kuwasafisha wenye dhambi (1 Wakorintho 6:9-11).

Zekaria anatabiri kwamba jina la sanamu litaondolewa katika nchi, manabii, na pepo wachafu pia wataondoka katika nchi. Kuhusiana na pepo wachafu. Mungu alimruhusu Shetani kuwa na nguvu zaidi katika enzi ya miujiza ya karne ya kwanza BK, ili kuonesha kuwa Yesu anaweza kushida hata katika ulimwengu wa kiroho kwa kuondoa pepo kutoka kwa watu (Mathayo 12:25-28).

Wakati ujumbe wa Mungu kwa mwanadamu ulikamilika kwa njia ya ujio wa Kristo na ufunuo wa Agano Jipya, hakuna manabii tena waliotumwa na Mungu. Ikiwa kuna mtu anayedai kuwa yeye ni nabii, basi mtu huyo anapaswa kujaribiwa (1 Yohana 4:1). Sifa za nabii wa kweli zilikuwa kwamba hatapingana na ufunuo uliopita (Kumbukumbu la Torati 13:1-5) na awe na uwezo wa kufanya miujiza ya kweli (Yohana 3:2).

Zekaria 13:2-6 inasema: ***“Kisha itakuwa katika siku hiyo, asema BWANA wa majeshi, nitakatilia mbali majina ya sanamu katika nchi, yasikumbukwe tena; pia nitawafukuza manabii, na roho ya uchafu, watoke katika nchi. Tena itakuwa ya kwamba, mtu awaye yote atakapotoa unabii, basi baba yake na mama yake waliomzaa watamwambia, Hutaishi; kwa maana unanena maneno ya uongo kwa jina la Bwana; na baba yake na mama yake waliomzaa watamtumbua atoapo unabii. Tena itakuwa siku hiyo, ya kwamba manabii, kila mmoja wao, atayaonea haya maono yake***



*atoapo unabii; wala hawatavaa joho ya nywele ili kudanganya watu; bali atasema, Mimi si nabii kamwe; mimi ni mkulima wa nchi; kwa maana nalifanywa mtumwa tokea ujana wangu. Na mtu atamwambia, Je! Jeraha hizi ulizo nazo kati ya mikono yako ni nini? Naye atajibu, Ni jeraha nilizotiwa katika nyumba ya rafiki zangu.”*

Je, nini kifanyike kwa mtu aliyepatikana kuwa nabii wa uongo chini ya sheria ya Musa? Andiko la Kumbukumbu la Torati 13:6-9 linasema hivi: *“Atakapokushawishi kwa siri ndugu yako, mwana wa mamaako, au mwana wako, au binti yako, au mke wa kifuani mwako, au rafiki yako aliye kama moyo wako, akikuambia, Twende tukaabudu miungu mingine usiyojua wewe wala baba zako; katika miungu ya mataifa yaliyo kando-kando yenu karibu nawe au mbali nawe, tokea ncha moja ya dunia hata ncha ya pili ya dunia; usimkubalie wala usimsikize; wala jicho lako lisimwonee huruma, wala usimwache, wala usimfiche; mwue kweli; mkono wako na uwe wa kwanza juu yake katika kumwua, na baadaye mikono ya watu wote.”*

Tunaona mfano katika 1 Wafalme 18:40: *“Eliya akawaambia, ‘Wakamateni manabii wa Baali! Asiokoke hata mmoja.’ Wakawakamata; na Eliya akawachukua mpaka kijito cha Kishoni, akawaua huko.”*

Je, tuwaue wale wanaojidai kuwa ni manabii leo? Zekaria alikuwa akiwasiliana na wasikilizaji wake kwa lugha ya “Agano la Kale.” Kwa kuwa Zekaria alikuwa akielekeza kwenye enzi ya Agano Jipya; ebu tuangalie 1 Wakorintho 5:12,13 ambayo ilikuwa katika muktadha wa kumwadhibu mwasherati: *“Maana yanihusu nini kuwahukumu wale walio nje? Ninyi hamwahukumu hao walio ndani? Laki ni hao walio nje Mungu atawahukumu. Ninyi mwondoeni yule mbaya miongoni mwenu.”*

Utaona kwamba Paulo ananukuu kutoka katika Kum-

bukumbu la Torati chini ya Sheria ya Musa ambayo ilikuwa imetumia adhabu ya kifo kwa manabii wa uongo (Kum. 13:6), waabudu sanamu (17:7), mashahidi wa uongo (19:19), watoto waasi (21:21), na watekaji nyara (24:7).

Je, Paulo alikuwa akisema mwasherati alipaswa kuuawa kimwili? Hapana. Kwa sababu tunajifunza kwamba mtu huyo alitubu baadaye (2 Wakorintho 2:1-11). Alipaswa kuondolewa katika ushirika kwa sababu alikuwa amekufa kiroho machoni pa Mungu (rej. Luka 15:32). Hii pia ingetumika kwa wale wanaojidai kuwa ni manabii leo. Wanapaswa kutengwa na ushirika ili waweze kurudi nyuma na kutubu.

Baadhi ya manabii wa uongo wanaweza kufanya jaribio la kuonekana kuwa ni wa kweli kwa kuvaa mavazi ya manyoya kama vile Eliya ambaye alikuwa nabii wa kweli wa Mungu (2 Wafalme 1:8). Ikiwa mtu fulani angeuliza kuhusu majeraha waliyopata, basi wangekubali kwamba walijitia wenyewe kama vile manabii wa uongo wa Baali walivyojifanyia wenyewe (1 Wafalme 18:28). Zekaria 13:6 haimhusu Yesu Kristo hata kidogo! Inajadili wale wanaodai kuwa manabii na kumbe ni manabii wa uongo!

**(11) Kwa nini kitabu cha *M & M* 45:52,53 kinalitumia vibaya hili kwa majeraha ya kusulibiwa kwa Kristo inapojadili manabii wa uongo katika muktadha wa Zekaria 13?**

### **Mafundisho: Karama za Miujiza**

Kitabu cha *M & M* 46 kinajadili karama tisa za miujiza ambazo zilitajwa pia katika 1 Wakorintho 12. Muktadha unaweka wazi kwamba karama hizi zitatumika katika kanisa la Watakatifu wa Siku za Mwisho. “Ufunuo” huu ulitolewa mnamo Machi 8, 1831. Kitabu cha Mormoni pia kilidhani kwamba enzi ya miujiza ingerejeshwa (Mormoni 8–9; Moroni 10).

**(12) Ikiwa hivyo ndivyo iliivyo, basi kwa nini muujiza wa kweli haufanyiki ili kuonesha kwamba Watakatifu wa**

## Siku za Mwisho wnazungumza kwa niaba ya Mungu?

### Mafundisho: Lusifa

Katika *M & M* 76:25-29, inasema: “**Na hii tuliona, na tunaishuhudia, kwamba malaika wa Mungu aliyekuwa mwenye mamlaka katika uwepo wa Mungu, ambaye aliasi dhidi ya Mwana Pekee ambaye Baba alimpenda na ambaye alikuwa katika kifua cha Baba, alitupwa chini kutoka katika uwepo wa Mungu na Mwana, Na aliitwa Mpotevu, kwa kuwa mbingu zililia juu yake— alikuwa Lusifa, mwana wa asubuhi. Nasi tuliona, naye ameanguka! ameanguka, hata yule mwana wa asubuhi! Na wakati tukiwa bado katika roho, Bwana alituumuru kuwa tuyaandike maono haya; kwani tulimwona Shetani, yule nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi, ambaye alimwasi Mungu, na alitafuta kuutwaa ufalme wa Mungu wetu na Kristo wake. Kwa hiyo, yeye hufanya vita na watakatifu wa Mungu, na kuwazingira.”**

Kuna mkanganyiko kati ya Biblia na kitabu cha *M & M* kuhusiana na utambulisho wa Lusifa. Mwandishi wa kitabu cha *M & M* anamtambulisha Lusifa kama Shetani. Tukio pekee la Lusifa unapochunguza katika Biblia linapatikana katika Isaya 14:12. Hata haimrejelei Shetani, bali Babeli Isaya 13-14. Tazama Isaya 13:1.

Chakuvutia, Alden anatoa historia jinsi Lusifa alivyokuja kujulikana kama Shetani. Aliandika hivi: “Tertullian, akitoa maelezo juu ya Isaya 14:12, alisema, ‘Hii lazima inamaanisha Ibilisi...’ Origen, pia, alitambulisha kwa urahisi ‘Lusifa’ na Shetani. Kitabu cha John Milton’s *Paradise Lost* (Paradiso ya John Milton iliyopotea) kimechangia kueneza dhana hii potofu...Kutokana na hayo kumezuka upotoshaji maarufu wa jina zuri la Lusifa ili kumaanisha Ibilisi” (Alden 35-36).

**(13) Kwa nini kitabu cha *M & M* kilikosea utambulisho wa**

## **Lusifa kuwa Shetani kama kweli kimevuviwa na Mungu?**

### **Mafundisho: “Esaya” na “Isaya”**

Katika *M & M* 76:100, inasema: **“Hawa ndiyo wale ambao husema kuna wale wa huyu na wengine wa mwingine—wengine wa Kristo na wengine wa Yohana, na wengine wa Musa, na wengine wa Elia, na wengine wa Esaya, na wengine wa Isaya, na wengine wa Henoko.”**

Kama ilivyosemwa kuhusu Eliya na Elias hapo awali, ni kosa lile lile lililofanywa hapa kwa kuwa neno “Isaya” limetumika katika Agano la Kale la KJV (Isaya 1:1) na “Esaya” limetumika katika Agano Jipya toleo la KJV (Mathayo 3:3; 4:14; 8:17; 12:17).

**(14) Kwa nini kitabu cha *M & M* kinachanganyikiwa kinapowasilisha “Isaya” na “Esayas” kama manabii wawili tofauti inaporejelea nabii yule yule?**

### **Mafundisho: Mkusanyiko wa Watakatifu**

Mojawapo ya uthibitisho wa ndani na wa makusudi wa uvuvio wa Biblia ni unabii wa kutabiri. Kulikuwa na majaribio yaliyotolewa ambayo nabii alipaswa kupitia ili kusimama kama nabii wa kweli.

Fox anasema: “Mwenyezi Mungu alikuwa amewakataza Wana wa Israeli kumkubali nabii bila ya ushahidi wa kuto-sha. Kulikuwa na mahitaji mawili ya kukubalika kwa nabii: Kwanza, nabii hapaswi kufundisha chochote ambacho kinapingana na Neno lolote la Mungu (Kum. 13:1-5). Pili, nabii lazima afanye ishara ambayo itatimia (Kum. 13:1–5 ; 18:20–22). Wana wa Israeli hawakutarajiwa kuukubali ujumbe uliokuja kwa ‘maneno matupu’ isipokuwa ule ambao ulikuja na nguvu (1 Thes. 1:5)” (Fox 479-480).

Sztanyo anatafakari kwa usahihi kuwa unabii unaotabiriwa ni alama ya uvuvio kwa sababu Mungu anajua kabla juu ya mambo mahususi ya wakati ujao. Anaandika hivi kwa kurejelea Isaya

41:21-23: “Angalia Bwana asema kwamba, kama mtu angeweza kutangaza mambo yatakayokuja, watu wangejua kwamba yeyote anayetabiri hivyo atakuwa miungu. Alisema tu kwamba, kama masharti haya yangetimizwa, (tungejua) kwamba ninyi ni miungu. Hoja hiyo hiyo ambayo ingethibitisha utambulisho wa kimungu kwa miungu ya uwongo (sanamu) ingethibitisha pia kwamba Bwana, Yehova ndiye Mungu.” Anaendelea kusema katika muktadha huo huo kwamba, yale ambayo miungu ya uwongo (na manabii wao) wasingeweza kufanya, kwa hakika angeweza kuyatimiza, kwani Yeye ni mjuzi wa yote (yaani hana kikomo katika maarifa)” (Sztanyo 222).

Daima unabii wa kweli utakuwa na vipengele vitatu muhimu vifuatavyo: (1) wakati muhimu, (2) maelezo mahususi, na (3) utimilifu wa 100%.

Ili kutoa mfano kutoka katika Biblia, soma Mika 5:2 – unabii wa sehemu ambayo Yesu angezaliwa: “**Lakini wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa maelfu ya Yuda, lakini kutoka kwako utanitokea Mmoja atakayekuwatawala katika Israeli, Ambaye matokeo yake ni tangu zamani za kale, tangu milele.**” Nabii Mika aliishi miaka 700 hivi kabla ya Yesu kuzaliwa, jambo ambalo linatimiza takwa muhimu la kuweka wakati.

Anatoa habari mahususi na kutaja mji mahususi ambao Yesu angezaliwa. Kulikuwa na Bethlehemu mbili kwa hakika - (1) Bethlehemu ya Zabuloni katika sehemu ya kaskazini ya Palestina (Yoshua 19:15; Waamuzi 12:8,10) na (2) Bethlehemu ya Yuda [mahali alipozaliwa Daudi - 1 Samweli 16:4; 17:12,15; 2 Samweli 23:14,16]. Mika alielewa mji huo! Unabii huu ulitimia hakika!

Ikiwa Mungu wa Biblia ndiye Mtunzi yule yule wa kitabu cha **M & M**, kilicho na unabii, basi ilitakiwa unabii uliotimia sawa sawa.

Walakini, shida ni kwamba kitabu cha **M & M** kina idadi

kubwa ya unabii ambao haujawahi kutimia ama kwa wakati maalum ambao ulipaswa kutokea haukufanyika, ama maelezo hayakuwa sahihi, au hayakutimizwa hadi mwisho.

Kesi maalumu zingekuwa hekalu ambalo lingejengwa huko Independence, Missouri (Jackson County, MO) kwenye sehemu maalum ambayo ilihusisha kipande maalumu cha ardhini na kutambua wakati maalumu wa unabii; hekalu lingejengwa ndani ya kizazi hicho hicho kilichosikia unabii wa Joseph Smith. Ingechukua takribani miaka mia moja kwa kizazi hicho kufa. Kwa hivyo unabii huu ulipaswa kuwa umeimizwa hivi karibuni zaidi kufikia miaka ya 1930s.

***M & M 57:1–3 inasema: “Sikilizeni, Enyi wazee wa kani-sa langu, asema Bwana Mungu wenu, ninyi mliojikusanya pamoja, kulingana na amri zangu, katika nchi hii, ambayo ni nchi ya Missouri, nchi ambayo nimeiteua na kuiweka wakfu kwa ajili ya kukusanyika watakatifu. Kwa hiyo, hii ni nchi ya ahadi, na mahali pa mji wa Sayuni. Na hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu wenu, kama mnataka hekima hapa ndipo penye hekima. Tazama, mahali ambapo sasa panaitwa Independence ni katikati, na eneo kwa ajili ya hekalu linalala upande wa magharibi, kwenye kiwanja ambacho hakiko mbali na nyumba ya mahakama.”***

Mnamo mwaka wa 1832, Smith aliingia katika maelezo mahususi zaidi kuhusu unabii ule ule katika “ufunuo” mwingine aliopewa kuhusu kusimamishwa kwa hekalu hili jipya wakati wa kizazi cha sasa.

***M & M 84:1-5: “Ufunuo wa Yesu Kristo kwa mtumishi wake Joseph Smith, Mdogo, na wazee sita, kama vile walivyunganisha mioyo yao na kupaza sauti zao juu. Ndiyo, neno la Bwana kuhusu kanisa lake, lililoanzishwa katika siku hizi za mwisho kwa ajili ya urejesho wa watu wake, kama alivyonena kwa vinywa vya manabii wake, na kwa ajili ya kuwakusanya watakatifu wake ili wasimame***

**juu ya Mlima Sayuni, ambao utakuwa mji wa Yerusalemu Mpya. Mji ambao utajengwa, kuanzia sehemu ya kiwanja cha hekalu, mahali ambapo pameteuliwa kwa kidole cha Bwana, katika mipaka ya Jimbo la Missouri, na kuwekwa wakfu kwa mkono wa Joseph Smith, na wengine ambao Bwana alipendezwa nao sana. Amini hili ndilo neno la Bwana, kwamba mji wa Yerusalemu Mpya utajengwa kwa kukusanyika kwa watakatifu, kuanzia mahali hapa, hata mahali pa hekalu, hekalu ambalo litainuliwa katika kizazi hiki kwani amini kizazi hiki chote hakitapita hadi nyumba itakapojengwa kwa Bwana, na wingu litatulia juu yake, wingu ambalo litakuwa na utukufu wa Bwana, ambalo litaijaza nyumba.”**

Hili lingesimama kama jaribu la kweli kuthibitisha kama Smith alikuwa nabii wa Mungu au la. Unabii ulishindwa kwa sababu historia inarekodi kanisa la Watakatifu wa Siku za Mwisho lilifukuzwa kutoka Jimbo la Jackson, Missouri na walowezi walioishi huko mnamo 1833 (Van Waggoner 142-159).

Kulikuwa na viongozi kadhaa wa Watakatifu wa Siku za Mwisho, ambao miaka mingi baadaye, walidai kwamba Bwana angetimiza unabii huo, lakini bado haujatokea wakati wa uandishi huu mnamo 2022.

**Mnamo 1858**, Heber C. Kimball alisema: “...lakini ikiwa huwezi kujifunza kushika amri za Mungu katika Jiji la Great Salt Lake City, unawezaje kujifunza kuzishika wakati inabidi ukimbilie milimani? Na kama huwezi kuziweka hapa, unatarajia kuziwekaje katika Jimbo la Jackson?—kwani tuna uhakika wa kurudi huko kama tulivyo” (Kimball, “Organization,” 134).

**Mnamo 1859**, Heber C. Kimball alisema: “Ni mahali patakatifu, na patachukuliwa kuwa patakatifu hata kama Kaunti ya Jackson; na hakuna mtu anayeishi huko lakini kwa siku hii ana roho ya hofu juu yake na anatazamia kwamba itamlaz-

imu kuandamana siku fulani; na, hadi leo, hakuna mtu aliyethubutu kulima au kujenga juu ya Kitalu cha Hekalu. Nabii Joseph aliweka wakfu ardhi hiyo, ... na bado nitaiona siku ambayo nitarudi huko, pamoja na kaka Brigham na pamoja na maelfu na mamilioni ya wengine, na tutaenda sawasawa na wakfu wa Mtume wa walio hai. Mungu. Zungumza nami kuhusu kuwa na shaka lolote akilini mwangu kuhusu mambo haya kutimizwa! Nina uhakika nayo kama nilivyo kwamba nimeitwa kuwa mwokozi wa wanadamu, na hakuna nguvu inayoweza kuizuia” (Kimball, “Increase,” 190).

**Mnamo 1861**, George Smith alisema: “Ni nani aliye tayari kwa harakati hii ya kurudi kwenye Kigingi cha Kati cha Sayuni, na wako wapi wasanifu majengo miongoni mwetu ambao wana sifa za kusimamisha hekalu hili na jiji ambalo litalizunguka?... Acha niwakumbushe kwamba ilitabiriwa kwamba kizazi hiki hakitapita hadi hekalu litakapojengwa, na utukufu wa Bwana ukae juu yake, kulingana na ahadi” (Smith, 71).

**Mnamo 1864**, George Q. Cannon alisema: “Siku imekaribia ambapo Hekalu litakuwa iliyolelewa katika Kigingi cha Kati cha Sayuni, na Bwana amesema utukufu wake utakaa juu ya Nyumba hiyo katika kizazi hiki, ambacho ni katika kizazi ambacho ufunuo huo ulitolewa, ambao ni zaidi ya miaka thelathini iliyopita” (Cannon 344).

**Mnamo Aprili 1870**, Orson Pratt alisema: “Tuna imani kama hiyo katika kurudi katika mji wa Jackson na ujenzi wa mji mkuu kuu...Kuna watu wengi wa zamani, ambao walipitia dhiki hizo zote nilizozitaja, bado wanaishi, ambao imani yao ya kurejea katika Jimbo la Jackson, na mambo yajayo, ni thabiti na thabiti kama kiti cha enzi cha Mwenyezi” (Pratt, “The Latter-Day Kingdom,” 138).

**Mnamo Mei 1870**, Orson Pratt alisema: “Natumaini hili, kwa sababu Mungu aliahidi katika mwaka wa 1832 kwam-



ba tunapaswa, kabla ya kizazi kilichoishi wakati huo kupita, kurudi na kujenga Mji wa Sayuni katika Wilaya ya Jackson; ili turudi na kulijenga hekalu la Aliye Juu Zaidi, pale tulipoweka jiwe la pembeni hapo kwanza. Alituahidi kwamba atajidhihirisha Mwenyewe juu ya hekalu hilo, ili utukufu wa Mungu uwe juu yake. Tunaamini katika ahadi hizo kama vile tunavyoamini ahadi yoyote ambayo imewahi kutolewa kwa kinywa cha Yehova. Watakatifu wa Siku za Mwisho vile vile wanatarajia kupokea utimilifu wa ahadi hiyo wakati wa kizazi kilichokuwako katika 1832 kama wanavyotazamia kwamba jua litachomoza na kutua kesho. Kwa nini? Kwa sababu Mungu hawezi kusema uwongo. Atatimiza ahadi zake zote. Amesema, lazima itimie. Hii ndiyo imani yetu” (Pratt, “The Latter-Day Work,” 362).

Orson Pratt alisema **katika 1874**: “Mungu alisema, katika mwaka wa 1832, kabla hatujafukuzwa kutoka Wilaya ya Jackson, katika ufunuo utakaoupata hapa katika kitabu hiki, kwamba kabla ya vizazi hivyo kupita vyote, nyumba ya Bwana inapaswa kujengwa katika eneo hilo, (Kaunti ya Jackson), “Juu ya mahali palipowekwa wakfu, kama nilivyo-teua; na utukufu wa Mungu, naam, wingu mchana na ngu-zo ya miali ya moto usiku vitakaa juu yake.” Katika sehemu nyingine, katika ufunuo huo huo, akizungumzia ukuhani, anasema kwamba wana wa Musa na wana wa Haruni, wale ambao walikuwa wamepokea ukuhani wawili, wanapaswa kujazwa na utukufu wa Mungu juu ya Mlima Sayuni, katika nyumba ya Bwana, na wapate kufanywa upya miili yao, na baraka zake Aliye juu zinapaswa kumwagwa juu yao kwa wingi sana. Hili lilitolewa miaka arobaini na miwili iliyopita. Kizazi kilichoishi wakati huo hakikuwa tu cha kuanzisha nyumba ya Mungu katika Jimbo la Jackson, Missouri, bali pia kilipaswa kukamilisha nyumba ile ile, na itakapokamili-ka utukufu wa Mungu utatakiwa kukaa juu yake. Sasa, je,

ninyi Watakatifu wa Siku za Mwisho mnaamini hivyo? Ni-naamini, na ikiwa unaamini katika mafunuo haya unatarajia vile vile utimilifu wa ufunuo huo kama ufunuo mwingine wowote ambao Mungu amewahi kutoa katika nyakati hizi za mwisho, au katika enzi zilizopita. Tunatazamia, sawasawa na hili kutokea, kulingana na neno la Bwana, kama vile Wayahudi wanavyotazamia kurudi Palestina, na kujenga upya Yerusalemu juu ya mahali pale iliposimama hapo awali. Wanatarajia kujenga Hekalu huko, na kwamba utukufu wa Mungu utaingia ndani yake; vivyo hivyo na sisi Watakatifu wa Siku za Mwisho tunatarajia kurudi Jackson County na kujenga Hekalu hapo kabla ya kizazi kilichokuwa kikishi miaka arobaini na miwili iliyopita yote hayajapita. Vizuri, basi, lazima muda uwe umekaribia sana ambapo tutaanza kazi hiyo” (Pratt, “Interest,” 111).

Orson Pratt baadaye aliandika katika kitabu chake kilichochapishwa mwaka wa **1891**: “Joseph Smith sio tu anakiri, kupitia njia ya malaika, kuwa amepokea kipindi cha Injili, na uwezo na mamlaka ya utume, lakini pia anakiri kuwa amepokea kwa njia ya ufunuo na amri kutoka kwa Mungu, kipindi cha kuwakusanya Watakatifu kutoka mataifa yote. Sasa fundisho la kukusanywa kwa Watakatifu katika siku za mwisho lazima liwe la uwongo au la kweli; ikiwa ni uongo, basi Joseph Smith atakuwa ni mlaghai. Haijalishi jinsi gani angeweza kuwa sahihi katika mambo mengine yote ya mfumo wake, ikiwa jambo hili moja la fundisho la mkusanyiko litakuwa la uwongo, lazima awe mdanganyifu. Kwa nini? kwa sababu anakiri kuwa amepokea fundisho hili kwa ufunuo wa moja kwa moja na amri. Kwa upande mwingine, ikiwa fundisho la kusanyiko la Watakatifu litakuwa fundisho la kweli na la kimaandiko, huu utakuwa ushahidi mwingine wa dhahiri kwamba Bw. Smith alitumwa na Mungu” (Pratt, *Orson Pratt's Works*, 16).

Haijawahi kutokea! Orson Pratt alisema wazi kwamba kama Smith alikosea juu ya unabii huu, basi alikuwa mlaghai na mdanganyifu.

Watetezi wa Watakatifu wa Siku za Mwisho hutoa majibu mawili. Jibu la kwanza wanasema hii ilikuwa ni amri, sio unabii. Jibu la pili wanadai neno “kizazi” kwa kweli linamaanisha “kipindi.”

Kuhusiana na kuwa ni amri, elewa kwamba kanisa la kwanza la WSM, waliomjua Joseph Smith hasa, walielewa jambo hili kama unabii pia.

Hebu tumruhusu Joseph Smith aeleze “kizazi” kilimaanisha nini: “Na sasa niko tayari kusema kwa mamlaka ya Yesu Kristo, kwamba haitapita miaka mingi kabla ya Marekani kuwasilisha tukio la umwagaji damu ambalo halijawahi kutokea katika historia ya taifa letu; tauni, mvua ya mawe, njaa, na tetemeko la ardhi vitafagia waovu wa kizazi hiki kutoka kwenye uso wa nchi, kufungua na kuandaa njia kwa ajili ya kurudi kwa makabila yaliyopotea ya Israeli kutoka nchi ya kaskazini. Watu wa Bwana, wale ambao wametii mahitaji ya Agano Jipya, tayari wameanza kukusanyika pamoja Sayuni, iliyo katika jimbo la Missouri; kwa hivyo ninawatangazia onyo ambalo Bwana ameamuru kutangazwa kwa kizazi hiki, nikikum-buka kwamba macho ya Muumba wangu yako juu yangu, na kwamba kwake ninawajibika kwa kila neno ninalolisema, bila kutamani chochote kibaya kwa wanadamu wenzangu zaidi ya wokovu wao wa milele; kwa hiyo, “Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja.” Tubuni ninyi, tubuni, na kulikumbatia agano la milele na mkimbilie Sayuni, kabla ya mapigo yanayofurika kuwajieni, kwani kuna wale wanaoishi sasa duniani ambao macho yao hayatafungwa katika kifo hadi waone mambo yote niliyoyasema yametimia” (Smith, *History*, Vol. 1, 315-316).

**(15) Kwa kuwa unabii wa Smith ni wa uwongo, je, hatupaswi kuhitimisha kuwa alikuwa nabii wa uwongo?**

## **Mafundisho: Hekalu la Magharibi ya Mbali, MO**

Baadaye, Smith alipokea “ufunuo” mwingine huko Magharibi ya mbali, Missouri mnamo Aprili 26, 1838 kujenga hekalu kwa ajili ya kuwakusanya watakatifu huko.

***M & M 115:7-12: “Acha mji wa Magharibi ya mbali, uwe mji mtakatifu na uliowekwa wakfu kwangu; nao utaitwa mtakatifu sana, kwani ardhi ambayo juu yake umesimama ni takatifu. Kwa hiyo, nakuamuruni kunijengea nyumba, kwa ajili ya kukusanyika pamoja watakatifu wangu, ili wapate kuniabudu. Na acha uwepo mwanzo wa kazi hii, na msingi, na kazi ya maandalizi ya kiangazi hiki kijacho; Na acha mwanzo ufanyike siku ya nne ya Julai ijayo; na tangu wakati ule na kuendelea acha watu wangu wafanye kazi kwa bidii kuijenga nyumba katika jina langu; Na katika mwaka mmoja kuto-ka siku hii acha waanze kuweka msingi wa nyumba yangu. Hivyo acha kuanzia tangu wakati ule na kuendelea wafanye kazi kwa bidii hadi itakapomalizika, kutoka jiwe lake la kona hadi juu yake, hadi pasiwepo na kitu chochote kitakachobakia bila kumalizika.”***

Hata hivyo, haikufanikiwa kwa sababu Watakatifu wa Siku za Mwisho waliondolewa kabisa nje ya Far West (Albanes 145-169).

**(16) Kwa kuwa unabii wa Smith ni wa uwongo, je, hapaswi kuchukuliwa kuwa ni nabii wa uwongo?**

**Mafundisho: Unabii wa Vita vya wenyewe kwa wenyewe**

***M & M 87:1–8: “Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kuhusu vita ambavyo karibu vitatokea, kuanzia kwenye uasi wa Carolina ya Kusini, ambao hatimaye utaishia kati-ka vifo na huzuni kwa watu wengi; Na wakati utakuja ambao vita vitamwagika juu ya mataifa yote, kuanzia mahali hapa. Kwani tazama, Majimbo ya Kusini yatagawanyika dhidi ya Majimbo ya Kaskazini, na Majimbo ya Kusini***

yatayaita mataifa mengine, hata taifa la Uingereza, kama linavyoitwa, na pia watayaita mataifa mengine, ili kujilinda wenyewe dhidi ya mataifa mengine; na ndipo vita vitamwagwa juu ya mataifa yote. Na itakuwa, baada ya siku nyingi, watumwa watainuka dhidi ya mabwana wao, ambao wataandaliwa na kufundishwa kwa ajili ya vita. Na itakuwa pia mabaki ya waliosalia katika nchi watajipanga wenyewe, na watakuwa wakali kupita kiasi, na watawaudhi Wayunani kwa maudhi makali. Na hivyo, kwa upanga na kwa umwagaji damu ya wakazi watakatifu, na damu ya watakatifu, kitakoma kuja katika masikio ya Bwana wa Sabato, kutoka duniani, kulipiza kisasi kwa adui zao. Kwa hiyo, simameni katika mahali pa takatifu, na wala msiondoshwe, hadi siku ya Bwana itapofika; kwani tazama, yaja haraka, asema Bwana. Amina.”

Unabii wa tatu ulioshindwa ni pale Smith alipotabiri mnamo 1832 Vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Marekani ambavyo vingetokea miaka thelathini baadaye. Kama Barfield na Martin wanavyoelezea, huu haukuwa unabii hata kidogo.

Barfield asema: “Ikiwa Smith alitoa unabii wake mnamo Desemba 25, 1832, alionesha tu maoni ya umma yaliyoenea [kwa sababu kulikuwa na tetesi za vita wakati huo]. Kilichofaa kuzingatiwa ni tahariri ya ukurasa wa mbele katika Painesville Telegraph na Geauga Free Press, gazeti lililochapishwa maili chache kutoka makazi ya muda ya Smith huko Kirtland, Ohio. Siku nne kabla ya unabii wa Smith, karatasi hiyo ilikosoa Georgia na Carolina Kusini, ikibaini hatua yao ‘inalenga moja kwa moja uasi wa silaha na vita vya wenyewe kwa wenyewe.’ Hivyo, kama vile Jonas aelezavyo: ‘Wakati Smith alipotoa unabii wake, taifa lilitazamia vita kati ya kaskazini na kusini vianze katika uasi wa Carolina Kusini’” (Barfield 219).

Martin anaandika: “Katika Historia ya Kanisa, Vol. I, ukurasa wa 301, ‘Joseph Smith anasema, ‘Kuonekana kwa ma-

tatizo miongoni mwa mataifa kulionekana zaidi msimu huu kuliko ilivyokuwa hapo awali tangu kanisa lilipoanza safari yake kutoka nyika...Watu wa Carolina Kusini, katika mkutano wanakusanyika (katika Novemba), walipitisha sheria, ikitangaza taifa lao kuwa taifa huru na lenye kujitegemea.’ Kutokana na hili tunajua ya kwamba Smith angeweza kuwa na ufahamu wa kujitenga kwa Carolina ya kusini mapema Novemba 1832. Ikiwa sio katika mwezi Novemba, basi Boston Daily Advertiser & Patriot, Desemba 10, 1832, inaweza kuwa rasilimali yake. Siku kumi na tano kabla ya unabii wa Smith, Mtume wa Mormoni Orson Hyde alikuwa Boston wakati karatasi hiyo ilichapishwa. Siku tano kabla ya unabii wa Smith, Bw. Hyde aliwasili katika nyumba ya Smith huko Ohio” (Martin 222).

Smith alikuwa amekusanya habari hii kutoka katika maoni ya umma yaliyoenea wakati huo. Zaidi ya hayo, Smith alikosea maelezo, kama vile: (1) vita “vingemiminwa juu ya mataifa yote” (*M & M* 87:2), (2) kuhusika kwa Uingereza na mataifa mengine (*M & M* 87:3), na (3) uasi wa watumwa dhidi ya mabwana zao (*M & M* 87:4).

**(17) Kwa kuwa unabii wa Smith ni wa uwongo, je, hapaswi kuonwa kuwa ni nabii wa uwongo?**

### **Mafundisho: Nyoka na Sumu**

Katika *M & M* 84:65-73, inasema: “**Na ishara hizi zitawafuata hao wanaoamini— Katika jina langu watafanya miujiza mingi; Katika jina langu watawafukuza pepo wabaya; Katika jina langu watawaponya wagonjwa; Katika jina langu watafungua macho ya vipofu, na kuzibua masikio ya viziwi; Na ulimi wake aliye bubu utasema; Na kama mtu yeyote atawawekea sumu haitawadhuru; Na sumu ya nyoka haitakuwa na uwezo wa kuwadhuru. Lakini amri ninaitoa kwao, kwamba wasijivune wenyewe kwa mambo haya,**

wala kuyanena mbele za walimwengu; kwani mambo haya yametolewa kwenu kwa faida na wokovu wenu.”

**(18) Je, ni kwa nini sasa ishara hizi hazifanywi na wale wa-naoamini (yaani, WSM)?**

**(19) Kwa nini WSM hawashiki nyoka?**

**(20) Kwa nini WSM hawanywi sumu?**

Ninataka kuwaonya washirika wa WSM kutoshika nyoka wala kunywa sumu. Kwa miaka mingi, kumekuwa na vifo vingi vya kusikitisha kutokana na wahubiri wa madhehebu kushika nyoka katika mkusanyiko wa ibada - kwa masikitiko makubwa wameumwa na nyoka na kufa. Wengi wa hawa “washika nyoka” watajaribu kuelekeza kwenye Maandiko ili kuhalalisha matumizi yao ya kushika nyoka leo, kama vile Marko 16:17-18: *“Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watahika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.”*

Wakati kanisa lilipokua hadi kukomaa wakati wa enzi za miujiza katika karne ya kwanza B.K., Matendo 28:3-6 inataja kisa ambapo ahadi ya Marko 16:17-18 ilitimizwa: *“Paulo alipokuwa amekusanya mzigo wa kuni, na kuuweka motoni, nyoka akatoka kwa ajili ya ule moto akamzonga-zonga mkononi. Wenyaji walipomwona yule nyoka akilewa-lewa mkononi, wakaambiana, Hakosi mtu huyu ni mwuaji; ambaye ijapokuwa ameokoka katika bahari haki haimwachi kishi. Lakini yeye akamtukusia motoni asipate madhara. Wao wakadhani ya kuwa atavimba au kuanguka chini kwa kufa ghafula; na wakiisha kumwangelia sana, na kuona kwamba halimpat dhara lo lote, wakageuka, wakasema kwamba yeye ni mungu.”* Wazawa wa kisiwa kile walipoona kwamba Paulo hakudhurika, walikuwa tayari kuupokea ujumbe wa Paulo.

Kuna tofauti kubwa kati ya “washika nyoka” wa sasa na mtume kwa kuwa Paulo hakuwa akimjaribu Mungu makusudi

kwa “kushika nyoka,” na hata hakuathiriwa kwa kugongwa na nyoka huyo mwenye sumu kali.

**(21) Kwa nini “washika nyoka” wa kimadhehebu wana-kufa kwa nyoka wenye sumu kali wanaowashika, lakini Paulo aliondoka bila ya kudhuurika?**

Moja ya kanuni za hermeneutics (sayansi ya kufasiri Maandiko) ni kwamba kuna tofauti ya wazi kati ya enzi ya miujiza na ukweli kwamba Mungu hafanyi miujiza leo. Miujiza ilifanyika katika siku hizo za kanisa la kwanza ili kuhalalisha na kuthibitisha ujumbe mpya wa ufunuo wa Mungu, ambao umetolewa katika ukamilifu wake (2 Petro 1:3; 1 Wakorintho 13:8-13). Ahadi ya ulinzi dhidi ya kuumwa na nyoka wenye sumu ilihusishwa moja kwa moja na kusudi la enzi ya miujiza ya kuthibitisha neno la Mungu (Marko 16:20; Waebrania 2:3-4). Neno la Mungu limethibitishwa na miujiza iliyorekodiwa katika Maandiko.

### **Mafundisho: Neno la Hekima**

Katika *M & M* 89, kile kinachojulikana kama Neno la Hekima ilitolewa. Kinachofurahisha ni historia ya jinsi ilivyokuja “kufunuliwa” mnamo **Februari 27, 1833**.

Brigham Young anasema: “Nafikiri ninafahamu vizuri hali ambazo zilisababisha kutolewa kwa Neno la Hekima kama mwanadamu yeyote Kanisani, ingawa sikuwapo wakati huo kuzishuhudia. Shule ya kwanza ya manabii ilifanyika katika chumba kidogo kilichokuwa juu ya jiko la Nabii Joseph, katika nyumba ambayo ilikuwa ya Askofu Whitney, na ambayo iliunganishwa na duka lake, duka ambalo pengine lingeweza kuwa kama futi kumi na tano za mraba. Nyuma ya jengo hili kulikuwa jikoni, labda futi kumi kwa kumi na nne, zenye vyumba na pantries. Juu ya jiko hili palikuwa na chumba ambapo Mtume alipokea wahyi/ufunuo na ambamo aliwaelekeza ndugu zake. Ndugu walifika mahali hapo kutoka mamia ya maili kuhudhuria shule katika chumba kidogo



pengine kisichozidi kumi na moja kwa kumi na nne. Walipokusanyika pamoja katika chumba hiki baada ya kifungua kinywa, cha kwanza walichofanya ni kuwasha kiko zao, na, wakati wakivuta sigara, walizungumza juu ya mambo makuu ya ufalme, na kutema mate chumba kizima, kwa sababu ya kutafuna sana tumbaku. Mara nyingi Mtume alipoingia chumbani kutoa maelekezo ya shule alijikuta kwenye wingu la moshi wa tumbaku. Jambo hili, na malalamiko ya mke wake kuhusu kusafisha sakafu chafu namna ile, vilimfanya Mtume afikirie juu ya jambo hilo, na akamuuliza Bwana kuhusiana na mwenendo wa wazee wa kutumia tumbaku, na ufunuo unaojulikana kama Neno la Mungu. Lijulikanalo kama Hekima lilikuwa matokeo ya uchunguzi wake. Unajua ni nini, na unaweza kukisoma kwa kujiburudisha” (Young, “School,” 158).

***M & M* 89:1-21 inasomeka hivi: “Neno la Hekima, kwa manufaa ya baraza la makuhani wakuu, waliokusanyika Kirtland, na kanisa, na pia watakatifu katika Sayuni— Kwa kutuma salamu; siyo kwa amri au kwa lazima, ila kwa ufunuo na neno la hekima, ambalo huonesha mpango na mapenzi ya Mungu katika wokovu wa kimwili wa watakatifu wote katika siku za mwisho— Limetolewa kwa kanuni yenye ahadi, na kuchukuliwa kwa kiwango cha wadhaifu na wadhaifu zaidi ya watakatifu wote, ambao ni au wanaweza kuitwa watakatifu. Tazama, amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwenu: Kwa sababu ya uovu na njama ambazo zipo na zitaendelea kuwepo katika mioyo ya watu wenye kula njama katika siku za mwisho, nimewaonya, na ninawaonya mapema, kwa kuwapa ninyi hili neno la hekima kwa ufunuo— Kwamba ikiwa mtu yeyote anakunywa divai au kinywaji kikali miongoni mwenu, tazama hivyo si vyema, wala haifai machoni pa Baba yenu, isipokuwa tu katika kukusanyika kwenu pamoja kutoa sakramenti mbele zake. Na, tazama, hii yapasa kuwa di-**

vai, ndiyo, divai halisi ya tunda la mizabibu, mliyotengeneza ninyi wenyewe. Na, tena, vinywaji vikali si kwa ajili ya tumbo, ila kwa kuosha miili yenu. Na tena, tumbaku si kwa ajili ya mwili, wala kwa tumbo, na si nzuri kwa mwanadamu, bali ni dawa kwa ajili ya majeraha na ng'ombe wote wagonjwa, itumiwe kwa kipimo na ujuzi. Na tena, vinywaji vya moto si kwa ajili ya mwili au tumbo. Na tena, amini ninawaambia, majani yote ya mimea Mungu ameiweka kwa ajili ya maumbile, sura, na kwa matumizi ya mwanadamu— Kila mmea katika majira yake, na kila tunda katika majira yake; vyote hivi vitumiwe kwa busara na kwa shukrani. Ndiyo, pia nyama ya wanyama na ya ndege wa angani, Mimi, Bwana, nimeviweka kwa matumizi ya wanadamu kwa shukrani; hata hivyo vitumike kwa uangalifu; Na yapendeza kwangu ikiwa havitatumiwa, isipokuwa tu nyakati za baridi, au katika baridi, au njaa. Nafaka zote zimewekwa kwa ajili ya matumizi ya mwanadamu na wanyama, kuwa chakula cha kutegemewa, si tu kwa mwanadamu bali hata kwa wanyama wa mashambani, na ndege wa angani, na wanyama wote wa porini wale watembeo au watambao juu ya dunia; Na hivi Mungu amevitengeneza kwa matumizi ya mwanadamu tu katika nyakati za ukame na njaa kali. Nafaka zote ni nzuri kwa chakula cha mwanadamu; pia kama vile mzao wa mizabibu; ule utoao matunda, iwe katika ardhi au juu ya ardhi— Hata hivyo, ngano kwa mwanadamu, na mahindi kwa ng'ombe, na mtama kwa farasi, na uwele kwa ndege na kwa nguruwe, na kwa wanyama wote wa mashamba, na shayiri ni kwa wanyama wote watumikao, na kwa vinywaji laini, kama vile nafaka nyinginezo. Na watakatifu wote ambao wanakumbuka kushika na kutenda maneno haya, wakitembea katika utii kwa amri hizi, watapata afya mwilini mwao na mafuta mifupani mwao; Na watapata hekima na hazina kubwa ya maarifa, hata hazina zilizofichika; Nao watakimbia na wasichoke, na watatembea wala hawataz-

**imia hadi kwao, kwamba malaika mwangamizaji atawapita, kama wana wa Israeli, na hatawaua. Amina.”**

**(22) Je, WSM hula nyama ya wanyama na ndege wa angani wakati wa majira ya baridi kali tu, baridi, au njaa?\*\*\*\*\***

Mnamo Novemba 1837, mkutano ulirekodiwa: “Baada ya maelezo machache kutoka kwa Sidney Rigdon, kusanyiko lilipiga kura kwa kauli moja kutounga mkono stoo na maduka ya kuuza vileo vyenye pombe, chai, kahawa, au tumbaku” (Smith, *History*, Vol. 2, 524).

Inafurahisha, hata hivyo, kuona ni mara ngapi kanuni za Neno hili la Hekima zilikiukwa katika historia ya kanisa la WSM. Hapa kuna mifano miwili tu, ingawa mingine inaweza kutajwa.

Mnamo **Desemba 22, 1841**, huko Nauvoo, IL, Smith alisema: “Siku hii nilianza kupokea usambazaji wa kwanza wa mboga kwenye duka jipya. Mabeheva kumi na tatu yaliwasili kutoka Warsaw, yakiwa yamepakia sukari, molasi, glasi, chumvi, chai, kahawa, n.k, iliyonunuliwa huko St. Louis” ( Smith, *History*, Vol. 4, 483).

**Juni 25, 1843** - Joseph Smith aliandika: “Iliripotiwa kwangu kwamba baadhi ya ndugu walikuwa wamekunywa whiskey siku hiyo kinyume cha Neno la Hekima. Niliwaita ndugu ndani na kuichunguza kesi hiyo, na nikaridhika kwamba hakuna ubaya wowote uliokuwa umefanywa, na nikawapa dola kadhaa, zikiwa na maelekezo ya kuijaza chupa ili kuwachangamsha katika uchovu wa safari yao ya kukosa usingizi” (Smith, *Millennial Star*, 283).

**(23) Je, inaonekana walilichukulia Neno la Hekima kwa uzito? Ikiwa sivyo, kwa nini?**

### **Mafundisho: Unabii wa Yoeli**

Muktadha wa kihistoria wa kitabu cha *M & M* 95, ni: “*Ufun-*

*uo uliotolewa kupitia Joseph Smith nabii, huko Kirtland, Ohio, Juni 1, 1833. Ufunuo huu ni muendelezo wa uongozi wa kiungu kujenga nyumba ya ibada na mafunzo, nyumba ya Bwana (angalia katika sehemu ya 88:119-36)."*

Katika *M & M* 95:4, inasema: "Kwa maandalizi pale ambapo napanga kuwaandaa mitume wangu kusafisha shamba langu la mizabibu kwa mara ya mwisho, ili kwamba niweze kuhitimisha tendo langu la kigeni, kwamba niweze kumimina Roho yangu juu ya wote wenye mwili."

**(24) Je, hili halikuhitimishwa katika miaka 1800 iliyopita?**

**(25) Je, katika Matendo 2:16,17 Petro hakusema kwamba unabii wa Yoeli ulikuwa umetimia?**

### **Mafundisho: Maana ya "Sabaoth"**

Katika kitabu cha *M & M* 95:7 inasema: "Na kwa sababu hii niliwapa ninyi amri ya kwamba yawapasa kuitisha kusanyiko lenu la kiroho, ili kufunga kwenu na kuomboleza kwenu kuweze kupaa juu masikioni mwa Bwana wa Sabato, ambaye kwa tafsiri, ni muumba wa siku ya kwanza, mwanzo na mwisho."

Isaya 1:9 inaeleza: "*Kama Bwana wa majeshi asingelichilia mabaki machache sana, tungalikuwa kama Sodoma, tungalifanana na Gomora.*"

Warumi 9:29 inasema: "*Tena kama Isaya alivyotangulia kunena, Kama Bwana wa majeshi [sabaoth] asingalituachia uzao, Tungalikuwa kama Sodoma, tungalifananishwa na Gomora.*"

Kulingana na Isaya 1:9 na Warumi 9:29, Paulo akiongozwa na Roho Mtakatifu akinukuu kwa Isaya, anatuonesha nini maana ya neno "sabaoth", ambalo ni "majeshi," SI "Muumba wa siku ya kwanza, mwanzo. na mwisho.

**(26) Kwa nini kitabu cha *M & M* kinatoa tafsiri isiyo sahihi ya neno "sabaoth"?**

## **Mafundisho: Ukuhani wa Melkizedeki**

Katika *M & M* 107:1,2, panasema: **“Katika kanisa, kuna aina mbili za ukuhani, ambazo ni wa Melkizedeki na Haruni, pamoja na ukuhani wa Lawi. Kwa nini ukuhani wa kwanza uliitwa Ukuhani wa Melkizedeki, ni kwa sababu Melkizedeki alikuwa kuhani mkuu aliye mkuu.”**

Bitton na Alexander walielezea kuhusu ukuhani huu: “Ukuhani mkuu ambao kila mwanaume mkubwa mwenye thamani anastahiki. Unapatikana kwa kuwekewa mikono na wale walioko kwenye mamlaka (Makala ya Imani namba 5). Nafasi (au vyeo) zilizopo ndani ya ukuhani wa Melkizedeki ni pamoja na wazee, kuhani mkuu, mababa, sabini, na mitume. Kama sehemu ya lazima ya kurejzwa kwa injili, Joseph Smith na Oliver Cowdery walipokea ukuhani wa Melkizedeki mwaka 1829 au mapema 1830 wakati mtume wa kale Petro, Yakobo na Yohana walipowatokea na kuwakabidhi” (Bitton na Alexander, “Ukuhani wa Melkizedeki,” 137).

Hoja kuu kuhusu mtazamo wa Watakatifu Wa Siku Za Mwisho ni kwamba Yesu kwa uwazi alipewa ukuhani huu kwa mfano wa Melkizedeki kulingana na (Zaburi 110; Waebrania 5:1-10; 6:20; 7:1-28). Ikiwa mtu amechunguza matendo ya wanaume washirika wa Watakatifu wa Siku za Mwisho wanayofanya wanapoingia katika ukuhani wa Melkizedeki, mtu ataona tofauti kubwa kati yake na namna ambavyo mwandishi wa Waebrania anavyoielezea.

Hoja zinazorejea fundisho hili la Watakatifu wa Siku za mwisho “Hakukuwa na kitu kama hicho katika kanisa la Agano Jipya; ni fundisho jipya, zao la ufunuo mpya na unaoendelea, na unaangukia kwanye hukumu ya Wagalatia 1:8. Mfumo huo wa ofisi za ukuhani haukijulikana katika kipindi cha Biblia, hauwezi kurejzwa, haiwezekani kurejeza kitu ambacho hakikuwepo mwanzo” (Free 231).

## **Mafundisho: Fundisho la Adamu-Mungu**

Nimekuwa nikisubiri kutambulisha fundisho hili linalopatikana katika kitabu cha Mafundisho na Maagano ambapo mistari yote kuhusu fundisho hili itatolewa. *M & M* 27:10-11 inasema: “**Pia pamoja na Yusufu na Yakobo, na Isaka, na Ibrahimu, baba zenu, ambao kwa njia yao ahadi zinabaki; na pia pamoja na Mikaeli, au Adamu, baba wa wote, mkuu wa wote, mzee wa siku.**”

Katika *M & M* 107:41,42,50-54: “**Mfano huu ulianzishwa katika siku za Adamu, na ulikuja chini kwa kurithi katika namna ifuatayo: Kutoka Adamu hadi Sethi, ambaye alitawazwa na Adamu akiwa na umri wa miaka sitini na tisa, na alibarikiwa naye miaka mitatu kabla ya kifo chake (cha Adamu), na kupokea ahadi ya Mungu kupitia baba yake, kwamba uzao wake watakuwa wateule wa Bwana, na kwamba kitahifadhiwa hadi mwisho wa dunia;.. Methusela alikuwa na umri wa miaka mia moja wakati alipotawazwa chini ya mkono wa Adamu. Lameki alikuwa na umri wa miaka thelathini na mbili wakati alipotawazwa chini ya mkono wa Sethi. Nuhu alikuwa na umri wa miaka kumi wakati alipotawazwa chini ya mkono wa Methusela. Miaka mitatu kabla ya kifo cha Adamu, alimwita Sethi, Enoshi, Kenani, Mahalaleli, Yaredi, Henoko, na Methusela, ambao wote walikuwa makuhani wakuu, pamoja na mabaki ya uzao wake waliokuwa wenye haki, katika bonde la Adamu-ondi-Amani, na huko akawawekea juu yao baraka zake za mwisho. Na Bwana akawatokea, nao wakainuka na kumbariki Adamu, na wakamwita Mikaeli, mtawala, malaika mkuu.**”

Katika *M & M* 116:1, panasema: “*Spring Hill Bwana alipaita Adamu-ondi-Amani, kwa sababu, alisema, ndipo mahali ambapo b Adamu atakuja kuwatembelea watu wake, au Mzee wa Siku atakapokaa, kama ilivyonenwa na Danieli nabii.*”

Katika *M & M* 128:21, inasema, “**Na tena, sauti ya Mun-**

**gu ndani ya chumba cha Baba mzee Whitmer, huko Fayette, wilaya ya Seneca, na nyakati nyingine mbalimbali, na mahali mbali mbali wakati wa misafara yote na taabu za hili Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho! Na sauti ya Mikaeli, malaika mkuu, sauti ya Gabrieli, na ya Rafaeli, na malaika mbalimbali, kutoka Mikaeli au Adamu kuja chini hadi wakati huu, wote wakitangaza vipindi vyao, haki na utukufu wao, na nguvu za ukuhani wao; wakitoa mstari juu ya mstari, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na kule kidogo; wakitupa faraja kwa kutangaza kile kitakachokuja, wakithibitisha matumaini yetu!”**

Hivyo kulingana na *M & M* 27:10,11, Mikaeli ni Adamu na pia mzee wa siku. Kulingana na *M & M* 107, Adamu ni Mikaeli malaika mkuu. Kulingana na *M & M* 116, Adamu ni mzee wa siku. Kulingana na *M & M* 128, Mikaeli ni Adamu.

Brigham Young, alisema baadhi ya mafundisho ya kipekee ambayo yameandikwa kwenye vitabu vya kumbukumbu ya mahubiri vinavyojulikana kama Jarida la mijadala.

Mojawapo ya fundisho la kipekee ambalo limekuja kujulikana na wengi ni fundisho la Adamu-Mungu. Kabla hatujaendelea zaidi, inatakiwa ijulikane kuwa kanisa la Watakatifu wa Siku za Mwisho ambalo lipo katika mji wa Salt Lake City (Mji wa Ziwa la Chumvi), Utah haulitambui fundisho hili kama fundisho la msingi la Imani yao. Katika mkutano mkuu ambao ulifanyika Oktoba 1976, Raisi Spencer W. Kimball alisema kwenye hotuba yake iliyokuwa na kichwa cha habari kinachosema: “Liahona yetu wenyewe” inasema: “Jambo jingine. Tunatumaini kwamba ninyi mnaofundisha katika taasisi mbalimbali, ikiwa ni katika vyo vikiu au katika ibada zetu, mara zote tutafundisha ukweli halisi. Tumewaonya kuhusu usambazaji wa mafundisho ambayo hayalingani na maandiko na ambayo yanadaiwa kufundishwa na baadhi ya

mamlaka kuu ya vizazi vilivyopita. Kwa mfano, nadharia ya Adamu-Mungu. Tunalaani kwamba nadharia na matumaini kwamba kila mmoja atatahadharishwa kuhusu hili na aina nyingine ya fundisho la uongo.”\*\*\*\*\*

Hii haiendani sana kwa sababu fundisho la kanisa la Watakatifu wa Siku za Mwisho linasema kwamba Raisi ni msemaji wa Mungu asiyekosea.

Kwa mfano, Joseph Smith, Raisi wa kwanza. Aliyedai: “Ni lini nimewahi kufundisha uwongo hapa niliposimama? Nili-changanyikiwa lini?...Sijawahi kuwaambia mimi ni mkamili-fu, lakini hakuna kosa katika ufunuo ambao nimeufundisha.” (Smith, *History*, Vol. 6, 366).

**(27) Kwa nini kanisa la Watakatifu wa Siku za Mwisho halikubali kile ambacho Young – raisi wa pili alichosema?**

**(28) Je, ilikuwa ya kuudhi, ya kigeni, na uongo?** Jihukumu mwenyewe na uone kile ambacho Brigham Young alifundisha.

Alisema mwanzoni mwa hotuba yake: “Hotuba yangu inayofuata itakuwa inawahusu wote, mtakatifu na mwenye dhambi. Kitu kimoja tu kimebaki siri katika ufalme huu hadi leo. Ni kuzingatia kuhusu sifa za Mwana mpendwa wa Mungu, ambaye somo ambalo wazee wa Israeli wana migogoro katika maoni Swali ambalo lipo na mara nyingi limeulizwa ni, nani ambaye alimzaa mwana wa Bikira Mariamu Sasa sikieni, enyi vizuizi vya dunia, Wayahudi na Mataifa, Watakatifu na wenye dhambi! Wakati baba yetu Adamu alipokuja katika Bustani ya Edeni, alikuja na mwili wa mbinguni, na kumleta Hawa, mmojawapo wa wake zake, pamoja naye, alisaidia kutengeneza na kupanga huu ulimwengu. Yeye ni Mikaeli, malaika mkuu, mzee wa siku! Ambaye watu watakatifu wameandika na kumzungumzia – Ni Baba yetu na Mungu wetu, na Mungu pekee ambaye [tunapaswa kumwamini]. Kila mtu duniani, atabirie ukristo



au asiyetabiri, lazima aisikie, na aijue mapema au baadaye” (Young, “Self-Government,” 50).

Tafadhali usikose habari za muhimu za hotuba yake. Alise ma kwamba, (a) Adamu alikuwa ni Mungu, (b) Mungu alileta mmoja wa wake zake pamoja naye aliyeitwa Hawa, (c) Hivi ndivyo jansi jamii ya binadamu ilivyoanza kwa Mungu kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Hawa, (d) Anajulikana kama Mikaeli, mzee wa siku, na (e) Yeye ni Baba na Mungu wetu wa Mbingun.

Young akaelezea zaidi: “Wakati Bikira Mariam alipobeba mimba ya mtoto Yesu. Baba akamzaa akiwa amefanana naye. Hakuwa amepatikana kwa Roho Mtakatifu. Na Baba ni nani? Ni wa katika familia ya mwanadamu; na alipolichukua hekalu, lilitolewa na Baba aliye mbinguni, baada ya tabia ile ile kama hema la Kaini, Habili na watoto wa kiume na wa kike wa Adamu na Hawa; kutoka katika matunda ya dunia, hekalu la kwanza ulimwenguni lilitengenezwa na Baba, na wengine katika ku-liendeleza. Ninaweza kukuambia mengi zaidi kuhusu hili; lakini mimi nilitakiwa kukwambia ukweli wote, kufuru itakuwa ni bure kwake, katika makadirio ya ushirikina na kuwa na haki kupita kiasi kwa mwanadamu. Hata hivyo nimekwambia ukweli kiasi nilichoweza” (Young, “Self-Government,” 50).

Angalia kulingana na Young, Adamu alikutana kimwili na Mariamu ambaye baadaye alimzaa Yesu Mwana wa Mungu na kwamba hakupatikana kwa nguvu za Roho Mtakatifu (ambayo inapingana na ushuhuda uliovuviwa wa Mathayo [Mathayo 1:20]).

Young akaelezea zaidi: “Tena, watajaribu kuelezea jinsi utatu wa Yesu umeunganishwa na uanadamu wake, na kucho-sha uwezo wao wote wa akili, na kumalizia na lugha ya kina, ikielezea roho ya mwanadamu, ‘ni katika dutu isiyoonekana!’ Ni wazo la namna gani la kujifunza! Yesu, kaka yetu mkubwa, alizaliwa katika mwili kwa sifa zile zile zilizokuwa katika

bustani ya Edeni, na ambaye ni baba yetu wa mbinguni. Sasa, wote watakaoyasikia mafundisho haya wasubiri kabla haya-jawapa nuru au kuwatendea tofauti, kwa kuwa yatathibitisha wokovu au kuangamia kwao. Nimekupa vitu vichache vya kukuongoza kuhusu somo hili, lakini bado mambo makubwa hayajaelezwa. Sasa kumbuka kuanzia kipindi hiki, hata milele kwamba Yesu Kristo hakuzaliwa na Roho Mtakatifu” (Young, “Self-Government,” 50-51).

Kama mshirika wa Watakatifu wa Siku za Mwisho, unaweza kusema, “kanisa la Watakatifu wa Siku za Mwisho la kisasa halikubali fundisho hili kama fundisho la kweli. Kwa nini un-aendelea kulirudisha?

Ni kwa sababu Raisi wako alisema kwamba manabii hawa wengine hawatalipotosha kanisa kamwe. Hawatafundisha fundisho la uongo kamwe. Pia tuna mfano wa wazi kutoka kwenye chanzo cha Watakatifu Wa Siku za Mwisho chenyewe ambacho Brigham Young alifundisha fundisho la uongo.

**(29) Pia unafanya nini kwa sehemu hizi za fundisho na Agano ambazo zinamtambua Adamu kama Mikaeli na mzee wa siku?**

**(30) Mtu anakataaje fundisho la Adamu-Mungu ambalo Young alifundisha lakini bado akashika kile kinachofundishwa na *M & M*?**

### **Mafundisho: Ufunuo wa siku hizi**

Katika *M & M* 121:26, panasema, “**Mungu atakupa maarifa kwa njia ya Roho wake Mtakatifu, ndiyo, kwa kipawa chake kisichosemeka cha Roho Mtakatifu, maarifa ambayo hayajafunuliwa tangu ulimwengu kuwepo hadi sasa.**”

**(31) Je, sivyo ilivyo kwamba mitume waliongozwa katika kweli YOTE katika karne ya kwanza B.K. (Yohana 16:13)?**

**(32) Sasa inakuwaje kwamba kuna ukweli zaidi wa ku-funuliwa?**

### **Mafundisho: Nyumba ya Nauvoo**

Katika *M & M* 124:56-60 panasema: “**Na sasa ninawaambia, kwa kuhusiana na nyumba yangu ya kuishi ambayo nime-waamuru kuijenga kwa ajili ya kuishi wageni, acheni ijen-gwe kwa jina langu, na acheni jina langu litajwe juu yake, na mtumishi wangu Joseph na nyumba yake wapate nafasi ndani yake, kutoka kizazi hadi kizazi. Kwani mpako huu wa mafuta nimeuweka juu ya kichwa chake, ili baraka zake pia ziwekwe juu ya uzao wake baada yake. Na kama vile nilivyo-sema kwa Ibrahimu kuhusu makabila za dunia, hivyo ndivyo ninavyosema kwa mtumishi wangu Joseph: Katika wewe na katika uzao wako kabila zote za dunia zitabarikiwa. Kwa hiyo, acheni mtumishi wangu Joseph na uzao wake baada yake yeye wapate nafasi katika nyumba hiyo, kutoka kizazi hadi kizazi, milele na milele, asema Bwana. Na acheni jina la nyumba hiyo iitwe Nyumba ya Nauvoo; na acheni iwe maka-zi ya kupendeza kwa mwanadamu, na mahali pa kupumzi-ka kwa msafiri aliyechoka, ili apate kutafakari utukufu wa Sayuni, na utukufu wa hili, jiwe lake lakona.”**

Joseph Fielding Smith alisema: “Nyumba ya Nauvoo, am-bayo ilianza katika siku za Joseph Smith, haijawahi kwisha, na kwa sababu ya muda kuta ziliangushwa na Bw. Lewis C. Bidamon, mume wa pili wa Emma Smith, na yaliyomo katika jiwe hili la msingi, ambalo kwa muda mrefu limewekwa wazi kwa vipengele, limeonekana kukaribia kuharibiwa. Baadhi ya Makala, hata hivyo, zimetunzwa na kusambazwa kwa wingi” (Joseph F. Smith 584).

**(33) Kwa nini Nyumba ya Nauvoo bado haijasimama kama nyumba ya wasafiri waliochoka? Je, haikupaswa kuwa kama Mungu alivyosema iwe?**

### **Mafundisho: Ubatizo wa wafu**

*M & M* 124, 127 na 128 inazungumzia ubatizo wa wafu.

***M & M* 128:15-16 inasema: “Na sasa, wapendwa ndugu na dada zangu, acheni nikuhakikishieni kwamba kanuni hizi zihusianazo na wafu na walio hai kwamba haziwezi ku-puuzwa, kwa vile zinahusu wokovu wetu. Kwa kuwa wokovu wao ni wa lazima na ni muhimu kwa wokovu wetu, kama vile Paulo asemavyo juu ya mababu—kwamba wao pasipo sisi hawakamiliki—wala sisi hatuwezi kuwa wakamilifu pasipo wafu wetu. Na sasa, kuhusu ubatizo kwa ajili ya wafu, nitakupeni dondoo nyingine ya Paulo, 1 Wakorintho 15:29: Au je! Wenye kubatizwa kwa ajili ya wafu watafanyaje, kama wafu hawafufuliwi kamwe? Kwa nini kubatizwa kwa ajili ya wao?”**

Watakatifu wa Siku za Mwisho wanatumia kifungu cha 1 Wakorintho 15:29 nje ya mazingira yake na kutumia katika matendo ya kidini ya maisha ya sasa (wakala wa ubatizo – mtu anayeishi anabatizwa kwa niaba ya mtu ambaye amekwisha-ufa ili wapokee wokovu) Mungu hajakusudia hilo.

Je, kifungu hiki kina maana gani?

Kumbuka muktadha hapa ni mfalme. Paulo alikuwa akizungumzia ufufuo wa kimwili wa Yesu Kristo kutoka katika wafu na jinsi inavyoingana na ufufuo halisi wa wenye haki na waovu kwenye ukamilifu wa wakati, ambao baadhi katika Korintho walikuwa wakiukataa. Paulo alianza kwa kuonesha uthibitisho kwamba kuna mashahidi wengi walioshuhudia kwa macho kuonekana kwa Yesu Kristo baada ya kufufuka (1 Wakorintho 15:1-11). Pia alikabiriwa na mtazamo hatarishi wa, vipi kama ufufuo wa Yesu Kristo haujatokea (1 Wakorintho 15:12-19).

Kilichofuata, Paulo alizungumzia athari za mantiki ya ukweli kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu (1 Wakorintho 15:20-28). Katika kipengele hiki, chenye mistari ya kutatanisha (1 Wakorintho 15:29-34), Paulo alikuwa akionyesha kwamba fundisho na mwenendo wa mitume (pamoja

na mashahidi wengine) wa ufufuo, vyote vimetolewa kama ushahidi wa ufufuo wa Yesu Kristo. Maana yoyote ambayo mstari huu unamaanisha, unazungumzia somo la ufufuo halisi wa baadaye. wa kimwili.

(1) Neno “wao” hapa labda linazungumzia wale waliokataa ufufuo wa wafu.

(2) Neno “kwa” limetokana na neno la Kiyunani, huper, lenye maana “kwa kuzingatia.”

(3) Neno “wafu” lipo katika hali ya wingi, lenye maana “waliokufa.”

(4) Walipobatizwa katika Kristo, wanatoka katika hali ya kufa kiroho (Waefeso 2:1,2) na kuwa katika hali ya kuwa hai kiroho (Warumi 6:1-10). Wamefufuliwa ili waenende katika upya wa uzima (Warumi 6:4). Kwa wao kubatizwa, kwa uwazi pia unaendana na ufufuo wa baadaye wa kimwili wa wafu.

“Vinginevyo, (wale waliokataa fundisho la ufufuo wa wafu) watafanya nini wale waliobatizwa (kwa kumbukumbu) kwa ajili ya wafu, ikiwa wafu hawatafufuka tena? Sasa kwa nini wanabatizwa kwa ajili ya wafu?”

Tukiweke hiki kifungu kwa maneno mengine rahisi: “Au kwa nini waliokataa ufufuo wa waliobatizwa wakati ubatizo ni kivuli cha ufufuo halisi wa baadaye wa wafu? Kama hakuna ufufuo wa baadaye wa wafu, kwa nini wajitoe katika tendo linaloendana na ufufuo wa baadaye wa wafu (wale)?”

Lipscomb na Sewell waliandika: “Wote waliozikwa pamoja na Kristo katika ubatizo wanathibitisha kwa tendo hilo kwamba wanaamini kwamba wamekufa na kufufuka tena; na kwa kuamini kwamba amefufuka, sisi kwa wakati ule ule tunaamini kwa matendo yetu tunathibitisha imani yetu katika ufufuo wa wafu wote. Kwa hiyo, kwa kuzamishwa kwetu, tunathibitisha kwa tendo hilo kwamba tunaamini katika ufufuo wa wafu wote, [ufufuo] wa Kristo kwanza na kupitia Yeye wengine wote. Ikiwa Yesu hakufufuka kutoka kwa wafu, kuz-

ikwa pamoja naye katika ubatizo kutakuwa hakuna maana; na kama hakufufuka, basi wengine hawatafufuka pia, na dini ya Yesu mwishowe itakuwa imeshindwa” (Lipscomb and Sewell 165).

Pia ndivyo ilivyo kwamba “ubatizo wa wafu” fundisho linapingana na Kitabu cha Mormoni Soma Alma 34:32-35; 42:4,13,28; Helamani 13:38; 2 Nefi 9:24,25,27.

**(34) Kwa nini kitabu cha Mafundisho na Maagano kinapotosha 1 Wakorintho 15:29, na kwa nini pia kinapingana na kitabu chenye “kilichovuviwa” Kitabu cha Mormoni – ambacho kinafundisha hakuna nafasi ya pili ya wokovu baada ya kifo cha kimwili (Alma 34:32-35)?**

### **Mafundisho: Kushikana Mikono na Roho**

Katika *M & M* 129:1-9 inasema: “**Kuna viumbe wa aina mbili mbinguni, nao ni: Malaika, ambao ni watu waliofufuka, wenye miili ya nyama na mifupa—Kwa mfano, Yesu alisema: Nishikenishikeni na mwone, kwa kuwa roho haina a mwili na mifupa, kama mnavyoniona mimi kuwa nayo. Ya pili, ni roho za watu wenye haki waliokamilika, wale ambao hawajafufuka, lakini wanarithi utukufu huo huo Wakati mjumbe akija akisema anao ujumbe kutoka kwa Mungu, mpe mkono wako na mwombe mshikane mikono. Kama yeye atakuwa malaika atafanya hivyo, nawe utausikia mkono wake. Kama atakuwa roho ya mtu mwenye haki aliyekamilika yeye atakuja katika utukufu wake; kwa kuwa hiyo ndiyo njia pekee anayoweza kuonekana—Mwombe mshikane mikono, lakini yeye hatafanya lolote, kwa sababu ni kinyume cha utaratibu wa mbinguni kwa mtu mwenye haki kudanganya; lakini yeye bado atatoa ujumbe wake—Lakini ikiwa ni ya a ibilisi akiwa kama malaika wa nuru, ukimwomba kushikana mikono naye atakupa mkono wake, na wewe hutasikia chochote; nawe**

**utaweza kumgundua. Hizi ndizo funguo kuu tatu ambazo kwa njia hiyo ninyi mtaweza kujua iwapo huduma yoyote yatoka kwa Mungu.”**

**(35) Je, Watakatifu Wa Siku Za Mwisho kwa dhati wanaamini huu “ufunuo” umetoka kwa Mungu?**

Mojawapo la fundisho la kanisa la Watakatifu Wa Siku Za Mwisho ni, wanaamini kuwa malaika wa mbinguni ni binadamu. Lakini Biblia inafundisha kuwa malaika na binadamu ni tofauti.

Kwanza, wanadamu wameumbwa kwa mfano wa Mungu (Mwanzo 1:26-27). Pili, wanadamu wameumbwa wadogo kidogo kuliko malaika (Zaburi 8:4-6). Tatu, wanadamu watawahukumu malaika (1 Wakorintho 6:3). Nne, Mungu ameruhusu mpango wa kumwokoia mwanadamu, si malaika (Waebrania 2:15-16; 2 Petro 2:4; Yuda 6). Tano, Mungu aliumba malaika kabla ya siku ya sita ya uumbaji (Ayubu 38:7). Wanadamu wameumbwa katika siku ya sita ya uumbaji (Mwanzo 1:26-27).

Katika *M & M* 130:22, inasema: “**Baba ana mwili wa nyama na mifupa wenye kushikika kama wa mwanadamu; na Mwana vile vile; lakini Roho Mtakatifu hana mwili wa nyama na mifupa, bali ni mtu wa Kiroho. Kama isingekuwa hivyo, Roho Mtakatifu asingeweza kukaa ndani yetu.”**

**(36) Je, baba hutunza miili hii ya nyama na mifupa milele?**

### **Mafundisho: Mitala**

